**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

**AFISI YA RAIS KAZI UCHUMI NA UWEKEZAJI**

# HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**ILIYOSOMWA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**NA**

**WAZIRI WA NCHI, AFISI YA RAIS, KAZI UCHUMI NA UWEKEZAJI**

**MHE. MUDRIK RAMADHAN SORAGA (MBM)**

**MEI, 2023**



**MHE. MUDRIK RAMADHAN SORAGA (MBM)**

**WAZIRI WA NCHI, AFISI YA RAIS,**
**KAZI UCHUMI NA UWEKEZAJI**

# YALIYOMO

YALIYOMO........................................................... i
VIFUPISHO VYA MANENO ..........................................iv
HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024.......................... 1
1.0 UTANGULIZI ...................................................... 1
2.0 MIKAKATI YA KUKUZA SEKTA YA KAZI, UWEZESHAJI NA UWEKEZAJI.............................. 5
2.1 UKUAJI WA SEKTA YA KAZI, UWEZESHAJI NA UWEKEZAJI ........................................................ 5
3.0 MAFANIKIO, CHANGAMOTO NA UTATUZI WA CHANGAMOTO...............................................10
3.1 MAFANIKIO...........................................................10
3.2 CHANGAMOTO ....................................................14
3.3 UTATUZI WA CHANGAMOTO ..................................14
4.0 UTEKELEZAJI WA MALENGO YA AFISI YA RAIS, KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023..............................................16
5.0 MUHTASARI WA MAPATO NA MATUMIZI KWA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 KWA FUNGU A07 (KAZI NA UWEZESHAJI) NA FUNGU A08 (UCHUMI NA UWEKEZAJI) ................18
5.1 MUHTASARI WA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA2022/2023...............................................18
5.1.1 FUNGU A07 (KAZI NA UWEZESHAJI) .................18
5.2 MUHTASARI WA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023...........................................19
5.2.1 MUHTASARI WA MATUMIZI KWA FUNGU A07 (KAZI NA UWEZESHAJI) ...................................19
5.2.2 MUHTASARI WA MATUMIZI KWA FUNGU A08 (UCHUMI NA UWEKEZAJI) ..............................22

6.0 UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA FUNGU A07 (KAZI NA UWEZESHAJI) ........................................24
6.1 PROGRAMU KUU PA0702: USIMAMIZI WA SHERIA ZA KAZI, UKAGUZI KAZI NA KAZI ZA STAHA KWA WOTE...............................................24
6.1.1 Programu Ndogo SA070201: Uratibu wa Upatikanaji wa Ajira za Staha ............................24
6.1.2 Programu Ndogo SA070202: Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini.....................................24
6.1.3 Programu Ndogo SA070203: Usimamizi wa Viwango vya Kazi vya Kitaifa na Majadiliano ya Pamoja Kazini...............................................30
6.2 PROGRAMU KUU PA0703: UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI .........................................35
6.2.1 Programu ndogo SA070301: Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. ..........................................36
6.2.2. Programu Ndogo: SA070302: Usimamizi na Uimarishaji wa Vyama vya Ushirika. ................43
6.2.3. Programu Ndogo SA070303: Uratibu na Uendelezaji wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. ........................................44
6.3 PROGRAMU KUU PA0703: UENDESHAJI NA URATIBU WA AFISI YA RAIS, KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI. ................................................56
6.3.1 Programu ndogo SA070301: Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Afisi. ............................................56
6.3.2 Programu Ndogo SA070502: Utawala na Uendeshaji. ................................................64
6.3.3 Programu Ndogo SA070503: Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Afisi Pemba................67
7.0 UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA FUNGU A08 (UCHUMI NA UWEKEZAJI) ...............................72

7.1 PROGRAMU KUU: PA0801 KUIMARISHA UWEKEZAJI NA MASHIRIKIANO BAINA YA SEKTA YA UMMA NA SEKTA BINAFSI ..................72
7.1.1 Programu ndogo SA080101: Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. .........73
7.1.2 Programu ndogo SA080102: Maendeleo ya Ukuaji wa Uchumi kupitia Uwekezaji. ..................76
7.2 PROGRAMU KUU PA0802: UENDESHAJI NA URATIBU WA AFISI KATIKA UCHUMI NA UWEKEZAJI. ................................................81
7.2.1 Programu ndogo SA080201: Utawala na Uendeshaji. ................................................81
7.2.2 Programu Ndogo SA080201: Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Afisi ............................... 83
7.2.3 Programu Ndogo SA080203: Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Afisi Pemba. .......... 87
8.0 VIPAUMBELE VYA AFISI KWA MWAKA WA FEDHA2023/2024.............................................94
9.0 MUELEKEO WA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024.........96
9.1 FUNGU A07 KAZI NA UWEZESHAJI ......................96
9.2 FUNGU A08 UCHUMI NA UWEKEZAJI ...................98
10.0 HITIMISHO .................................................99
11.0 VIAMBATANISHO ............................................102

## VIFUPISHO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| ADB: | Benki ya Maendeleo ya Afrika. |
| ARKUU: | Afisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji. |
| BOA: | Bank of Afirica: Benki ya Afrika. |
| COSTECH: | Commission for Science and Technology (Tume ya Sayansi na Teknolojia). |
| CRDB: | Cooperative and Rural Development Bank (Benki ya Maendeleo ya Ushirika. |
| CSR: | Corporate Social Responsibility. |
| DTB: | Diamond Trust Bank. |
| FAO: | Food and Agriculture Organization (Shirika la Kimataifa la Kilimo na Chakula). |
| ILO: | International Labour Organization (Shirika la Kazi Duniani). |
| JKU: | Jeshi la Kujenga Uchumi. |
| KCB: | Kenya Commercial Bank (Benki ya Biashara ya Kenya). |
| NEET: | Not in Education, Employment and Training (Vijana Wasio kwenye Ajira, Elimu na Mafunzo). |
| PBB: | Program Based Budget (Bajeti inayotumia Mfumo wa Programu) |
| PBZ: | People's Bank of Zanzibar (Benki ya Watu wa Zanzibar). |
| SMIDA: | Small and Medium Industrial Development Agency (Wakala wa Viwanda Vidogo vidogo na vya Kati). |
| TEHAMA: | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TCB: | Tanzania Commercial Bank (Benki ya Biashara Tanzania). |
| UNDP: | United Nations Development Program (Shirika la Kimataifa la Maendeleo) |

ZANEMA: Zanzibar Employer Association
(Jumuiya ya Waajiri Zanzibar).

ZATUC: Zanzibar Trade Union Congress
(Shirikisho la Wafanyakazi Zanzibar).

## HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

## 1.0 UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** Naomba kutoa hoja kwa Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili iweze kupokea, kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

2. **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote nachukua fursa hii adhimu kumshukuru Allah (Subhanahu Wataala) kwa Rehma zake na kwa kutujaalia uzima wa afya pamoja na kuibariki Nchi yetu kuwa na amani na utulivu. Ni dhahiri kwamba hali hiyo imezidi kuimarika kwa kipindi hiki chote chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi ambaye amekuwa akisisitiza umuhimu wa kudumisha Amani kila anapokutana na wananchi. Aidha, namuomba Mwenyezi Mungu amjaalie afya njema, busara na uwezo zaidi wa kuiongoza Zanzibar na kuleta maendeleo makubwa.

3. **Mheshimiwa Spika,** nachukua fursa hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 – 2025 na Mipango ya Maendeleo ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa. Katika kipindi hiki wananchi wa Zanzibar wameshuhudia maendeleo makubwa hasa katika kuimarisha uwekezaji na uwezeshaji jambo ambalo linaibua upatikanaji wa fursa za ajira kwa wananchi na

kuchangia katika ukuaji wa uchumi Zanzibar ambapo kwa hivi sasa umekua kwa asilimia 1.7 kutoka asilimia 5.1 mwaka 2021 hadi asilimia 6.8 mwaka 2022. Pia, tunampongeza kwa utoaji wa mikopo nafuu ambayo imewajengea wananchi matumaini baada ya athari za janga la korona, uwezo wa kujiajiri na kuimarisha kipato chao pamoja na kuchangia katika ukuaji wa uchumi wa nchi.

4. **Mheshimiwa Spika,** Aidha, nazipongeza juhudi za Mheshimiwa Rais za kufuatilia kwa karibu utendaji wa taasisi za Serikali kupitia maagizo, maelekezo, ziara na majadiliano ya ana kwa ana na watendaji wa Serikali, Mfumo wa Sema na Rais (SNR- Mwinyi) pamoja na Taasisi ya Ufuatiliaji wa utekelezaji wa Vipaumbele vya Mheshimiwa Rais (PDB). Hatua hizo zimeweza kuimarisha ufanisi katika utendaji, uwajibikaji, usimamizi na ufuatiliaji wa karibu wa majukumu ya Wizara na taasisi za Serikali. Aidha, naendelea kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuimarisha maslahi ya wafanyakazi kwa kupandisha viwango vya mishahara katika Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, Kuongeza Pensheni ya Wastaafu kwa asilimia 100 na Pensheni ya Wazee kwa asilimia 150 hali ambayo imesaidia kuimarisha hali za maisha za watendaji, wastaafu, wazee na familia zao.

5. **Mheshimiwa Spika,** Pia, nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa juhudi za pamoja wanazochukua katika kukuza uchumi wa nchi ikiwemo kutangaza vivutio

vya fursa zilizopo Tanzania vya uwekezaji pamoja na kusimamia ipasavyo zoezi la Sensa ya Watu na Makaazi kwa amani na utulivu na mafanikio makubwa. Napenda kushukuru sana kwamba matokeo ya Sensa hiyo tayari yametolewa na yameanza kutumika katika upangaji wa shughuli mbali mbali za maendeleo nchini. Sambamba na hilo nawapongeza kwa juhudi zao za dhati za kusimamia masuala ya kidiplomasia yanayopelekea kuimarisha mashirikiano mazuri na mema baina ya nchi yetu na mataifa mbali mbali duniani yanayosaidia kukuza uchumi wa nchi yetu.

6. **Mheshimiwa Spika,** Nawapongeza kwa dhati Viongozi Wakuu wa Kitaifa Makamu wa Kwanza waRais, Mheshimiwa Othman Masoud Othman na Makamuwa Pili wa Rais, Mheshmiwa Hemed Suleiman Abdulla pamoja na Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi Mhandisi Zena Ahmed Said kwa kufanya kazi bega kwa bega na Mheshimiwa Rais katika kumsaidia na kumshauri katika masuala mbali mbali ya kuiletea maendeleo Nchi yetu.

7. **Mheshimiwa Spika,** naomba nikupongeze wewe binafsi kwa namna unavyoliongoza Baraza hili kwa umahiri mkubwa. Chini ya uongozi wako Baraza hili limekuwa tulivu jambo ambalo limewafanya Wajumbe kuwa huru, kuchangia hoja na kutoa mawazo yao pasi na kikwazo kwa muda wote wa vikao vya Baraza. Aidha, nampongeza Naibu Spika, Wenyeviti na Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa namna wanavyotoa hoja na michango inayopelekea kuongeza ufanisi na uwajibikaji wa Watendaji wa Taasisi mbali mbali hali inayopelekea kuharakisha maendeleo ya nchi, namuomba Mwenyezi

Mungu awazidishie uwezo wa utendaji, hekima na busara.

8. **Mheshimiwa Spika,** Kwa niaba ya Wafanyakazi wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji napenda kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi ya Baraza la Wawakilishi Mheshimiwa Sabiha Filfil Thani kwa namna anavyosimamia kwa makini kazi za Kamati pamoja na utekelezaji wa majukumu ya Wizara zilizochini ya Kamati yao kwa lengo la kuleta maendeleo endelevu ya nchi yetu. Pia, nawapongeza Wajumbe wote pamoja na Makatibu wa Kamati kwa kuwa karibu sana na Afisi kwa kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yetu, chini ya uongozi wake mahiri, hodari, shupavu ambapo shughuli zetu nyingi zimefanikiwa.

9. **Mheshimiwa Spika,** nawashukuru kwa dhati Wananchi wa Jimbo la Bububu kwa kuendelea kuniamini na kuimarisha Amani na Utulivu pamoja na kuniunga mkono katika kazi zangu za uwaziri na uwakilishi hadi leo. Naahidi kuwa nitaendelea kuwatumikia kwa moyo wangu wote na kuwashirikisha katika maamuzi yatakayoleta maendeleo jimboni mwetu. Mwisho kabisa, namshukuru kwa dhati barafu ya Moyo wangu, Mke wangu Mpenzi pamoja na familia yangu yote kwa kuendelea kunivumilia na kuwa nami bega kwa bega kwa kipindi chote hichi.

## 2.0 MIKAKATI YA KUKUZA SEKTA YA KAZI, UWEZESHAJI NA UWEKEZAJI.

10. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji ina lengo la kuimarisha hali za kijamii na kiuchumi za wananchi wa Zanzibar kwa kutoa na kutumia fursa za kiuchumi zilizopo na zitakazokuja, kushajihisha utamaduni na uwezo wa ujasiriamali, kukuza uwekezaji wa ndani na nje, kuimarisha upatikanaji wa kazi za staha na kuzingatia sheria na viwango vya kazi. Dhamira hii itafikiwa kwa kutekeleza na kuimarisha Sekta ya Uwekezaji, Sekta ya Kazi na Ajira na Sekta ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, kwa kuzingatia Sera na Mikakati ya Kisekta, Kitaifa, Kikanda na Kimataifa.

## 2.1 UKUAJI WA SEKTA YA KAZI, UWEZESHAJI NA UWEKEZAJI

11. **Mheshimiwa Spika;** Sekta ya Kazi, Uwezeshaji na Uwekezaji inaendelea kukua na katika mwaka wa fedha 2022/2023 imepata mafanikio makubwa na kuchangia katika ukuaji wa uchumi na pato la Taifa. Sekta ya Kazi na Ajira inatoa mchango mkubwa wa kujikimu kwa maisha ya wananchi. Utafiti wa Watu Wenye Uwezo wa Kufanya Kazi wa Mwaka 2020/2021 – Zanzibar unaonesha kwamba kiwango cha ukosefu wa ajira kimeongezeka hasa kwa vijana kutoka Asilimia 21.3 mwaka 2014/2015 hadi Asilimia 27.4 mwaka 2020/2021 (ILFS 2020/2021). Hali hii inatokana na athari ya mripuko wa maradhi ya Korona na vita vya Urusi na Ukraine ambavyo vimepelekea kuteteresha hali ya kiuchumi duniani na Zanzibar na wananchi kukosa ajira. Ili kupambana na hali hii, ARKUU kwa kushirikiana na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF)

imeanzisha Fao la Upotevu wa Ajira ambalo litasaidia wananchi waliopoteza ajira kupata mafao na kupunguza ukali wa maisha pamoja na kuweza kubuni njia nyengine za kujiajiri.

12. **Mheshimiwa Spika;** Vile vile, ARKUU imeweka mikakati imara ya kuimarisha sekta mbali mbali zinazochangia katika kukuza Ajira. Miongoni mwa Mikakati inayowekwa ni pamoja na kufanya mapitio ya Sera na Sheria za Ajira na Uwekekzaji; Kuandaa Mpango Kazi wa Tatu wa Miaka Mitano wa Kuzalisha Ajira; Kuandaa Mswada wa Sheria ya Kuzalisha Ajira; Kufanya Mapitio ya Mfumo wa Taarifa za Soko la Ajira; Kuimarisha Uwekezaji; Kuandaa programu za kukuza Ajira kwa Vijana na kuimarisha upatikanaji wa takwimu za Ajira ambazo zitasaidia kutambua changamoto zilizopo katika maeneo mbalimbali.

13. **Mheshimiwa Spika;** Pia, Afisi ina jukumu la kuratibu upatikanaji wa ajira za ndani na nje kupitia Wakala wa Ajira katika Sekta binafsi. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 upatikanaji wa Ajira rasmi za ndani umeongezeka kwa asilimia 10.2 kutokana na Mikataba inayothibitishwa kutoka ajira 5,700 mwaka 2021/2022 hadi 6,348 mwaka 2022/2023 katika Sekta ya Skuli Binafsi, Hoteli na Viwanda. Aidha, upatikanaji wa ajira nje ya nchi umekuwa kwa asilimia 60 kutoka ajira 431 mwaka 2021/2022 hadi ajira 1,080 kwa mwaka wafedha 2022/2023. Ukuaji huu unatokana na kuimarika kwa Sekta ya Uwekezaji nchini; hali ya Amani na utulivu; kuimarika kwa Diplomasia ya nchi na mataifa mbali mbali na kuweka mikakati ya kusimamia Wakala Binafsi wa Ajira nchini **Kiambatanisho nambari 1(a na b) kinahusika**.

14. **Mheshimiwa Spika;** Aidha, Sekta ya Kazi na Ajira imeweza kuimarika kutokana na kuongezeka kuthibitishwa mikataba ya kazi kwa Wafanyakazi Wazalendo kwa asilimia 0.5 Kutoka mikataba 6,316 kwa mwaka 2021/2022 hadi Mikataba 6,352 kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Vile vile, Sekta ya Uwekezaji ni moja ya Sekta inayochangia katika ukuaji wa Sekta ya Ajira nchini kwa kufanikiwa kuongeza ajira kwa asilimia 48.5 kutoka ajira 6,729 mwaka 2018/2020 hadi ajira 13,067 mwaka 2020/2023. Kiambatanisho nambari 1(c) kinahusika.

15. **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ina lengo la kuinua kipato cha mwananchi, mjasiriamali na mfanyabiashara kwa kuwawezesha kupitia mafunzo, mikopo na masoko. Sekta hii imetiliwa mkazo katika Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050 katika Nguzo ya 1 ya Mabadiliko ya Kiuchumi; Mkakati wa Maendeleo wa Zanzibar 2021-2026 ambao umeweka mikakati ya kuimarisha shughuli za uwezeshaji Wananchi kiuchumi hasa katika maeneo ya miundombinu ya uwezeshaji, mafunzo, ushirika, mitaji, mikopo, ubunifu, ubora, masoko na viwanda vidogo na vya kati pamoja na Ilani ya Chama cha Mapinduzi Ibara 142 na 143.

16. **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Uwezeshaji katika kukuza mitaji ya Wajasiriamali kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imefanikiwa kutoa mikopo 2,177 kutoka mikopo 286 iliyotolewa mwaka 2021/2022, hii ni sawa na ongezeko la asilimia 86.8. Hali hii imetokana na Serikali ya Awamu ya Nane ya Dkt. Hussein Ali Mwinyi kuipa kipaumbele Sekta hii kwa kuiweka kuwa ni miongoni mwa Vipaumbele vyake. Kiambatanisho nambari 1(d) kinahusika. Pia,

Ongezeko hili limechangiwa na Serikali ya Awamu ya Nane kuunda Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi chini ya Sheria Nambari 02 ya mwaka 2022 ambao mbali na mambo mengine inaunganisha mifuko ya uwezeshaji na mifuko mengine kama vile Mfuko wa Khalifa ili kuweza kunufaisha wananchi wengi zaidi; Kuwepo kwa Mkopo wa INUKA unaosimamiwa na CRDB Benki na Fedha za Mikopo za Halmashauri. Aidha, Serikali inaimarisha Sekta ya Ushirika ili iweze kuleta ufanisi kwa kutoa huduma za kifedha, kutoa ajira, kunyanyua pato la mwananchi na uchumi wa nchi. Sekta hii inashajiisha uundaji wa vyama vya ushirika ambapo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imesajili jumla ya vyama 1,822 ikilinganishwa na vyama 1,844 kwa mwaka 2021/2022.

17. **Mheshimiwa Spika,** Aidha, Afisi imepiga hatua katika utoaji wa mafunzo kwa wajasiriamali katika maeneo ya ufugaji wa nyuki, usarifu wa matunda na mboga mboga, utengenezaji wa vifaa vya sola, masoko, ujasiriamali na mafunzo ya uokaji. Idadi ya wanufaika imeongezeka kwa asilimia 6 kutoka wajasiriamali 1,230 kwa mwaka 2021/2022 hadi kufikia 1,308 kwa mwaka 2022/2023 **Kiambatanisho nambari 1(e) kinahusika**. Aidha, suala la masoko kwa bidhaa za Wajasiriamali ni moja ya kipaumbele cha Wakala wa Uwekezaji Wananchi Kiuchumi. Mbali ya mafunzo ya Utafutaji masoko, Serikali inawaunganisha wajasiriamali na masoko mbali mbali kupitia maonesho yakiwemo maonesho ya Afrika mashariki, Sabasaba na Maonesho ya Mapinduzi ambapo idadi ya Wajasiriamali waliounganishwa na masoko imeongezeka kwa asilimia 79 kutoka wajasiriamali 46 mwaka 2021/2022 hadi kufikia wajasiriamali 221 mwaka 2022/2023.

18. **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Awamu ya Nane imedhamiria kuimarisha Sekta ya Uwekezaji ili iweze kuwa ni miongoni mwa Sekta zinazochangia katika ukuaji wa uchumi nchini. Usajili wa Miradi ya Uwekezaji umekuwa kwa asilimia 61.2 kutoka miradi 90 iliyosajiliwa kuanzia Machi 2018 hadi Oktoba 2020 kulinganisha na miradi 232 iliyosajiliwa kuanzia Oktoba 2020 hadi Machi 2023. **Kiambatanisho nambari 1(f) kinahusika**. Hii imechangiwa na kuimarisha utoaji wa huduma jumuishi za uwekekzaji, kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo nchini pamoja na kukifungua kisiwa cha Pemba katika shughuli za Uwekezaji kwa kuweka vivutio maalum kwa uwekezaji mkakati.

19. **Mheshimiwa Spika,** Ongezeko hili pia linaonekana katika usajili wa Miradi ya Uwekezaji ambapo kwa kipindi cha mwaka 2021/2022 jumla ya miradi 62 imewekezwa ukilinganisha na miradi 74 iliyowekezwa mwaka 2022/2023 hii ni sawa na ongezeko la asilimia 16.2. Vile vile, miradi 3 ya PPP ipo katika hatua za mwisho za uchambuzi. Utolewaji wa Vibali vya kazi kwa Wafanyakazi wa Kigeni umepungua kwa asilimia 33 kutoka vibali 1,863 mwaka 2021/2022 hadi vibali 1,248 mwaka 2022/2023. Hii ni kutokana na kuweka mikakati ya kupunguza wageni kuja kufanyakazi nchini kwa zile kazi ambazo wazawa wana ujuzi nazo ili nafasi za kazi hizo zijazwe na Wazawa.

20. **Mheshimiwa Spika,** Pia, Sekta ya Uwekezaji ina mchango mkubwa katika kukuza pato la taifa na uchumi wa nchi. Mtaji wa Miradi ya Uwekezaji imekuwa kwa asilimia 77.8 kutoka Dola za Kimarekani 784,947,180 mwaka 2018/2020 hadi Dola za Kimarekani 3,542,570,968

mwaka 2020/2023. Ukuaji huu umechangiwa na kuweka mazingira mazuri ya kisera na kisheria, kuimarisha huduma jumuishi za uwekezaji, kuweka mfumo wa kieletroniki unaorahisisha utoaji wa huduma, kuwepo ardhi ya akiba kwa uwekezaji, kuimarisha miundo mbinu ya uwekezaji katika Maeneo Huru ya Uwekezaji na Uwekezaji wa Visiwa.

## 3.0 MAFANIKIO, CHANGAMOTO NA UTATUZI WA CHANGAMOTO

## 3.1 MAFANIKIO

**21. Mheshimiwa Spika;** Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023, Afisi imepata mafanikio yafuatayo:-

1. Imeratibu upatikanaji wa ajira 7,428 kwa Vijana (nje na ya nchi 1,080 na ndani ya nchi 6,348 katika Nchi za Oman, Saudi Arabia, Qatar, Kuwait na UAE.

2. Imetoa Mafunzo ya vitendo kwa njia ya kujitolea (internship) katika fani ya ualimu, utalii, ushoni na ufundi wa magari kwa vijana 50 (wanawake 29 na wanaume 21) kutoka Wilaya ya Mkoani, Chake-Chake, Wete na Michweni. Programu hiyo imefanyika kwa wahitimu wa fani za Hotelia, Ufundi Magari, Ushoni na Ualimu.

3. Imefanya ukaguzi wa Usalama na Afya Kazini kwenye sehemu za kazi 234 (135 Unguja na 99 Pemba) na imesajili sehemu za kazi 76 (59 Unguja na 17 Pemba). Imefanikiwa kufanya ukaguzi kazi katika Taasisi 243 (Unguja 164 na Pemba 79) na imethibitisha Mikataba 6,348 (Unguja 5,559 na Pemba 789).

4. Imefanikiwa kuongeza kima cha chini cha Mshahara kwa Sekta Binafsi kutoka Shilingi 300,000 hadi 347,000 na kutoka Shilingi 180,000/- hadi 250,000/-.

5. Afisi kupitia Kamisheni ya Kazi, imeruhusu wafanyakazi wa kigeni 1,248 kufanya kazi nchini kwa kuwapatia vibali vya kazi.

6. Imesajili Miradi 74 ya Uwekezaji ambayo inakadiriwa kuwekeza jumla ya Dola za kimarekani Milioni Mia Nne Arobaini na Nne, Laki Tisa Sabini na Saba Elfu, Hamsini na Nne ($444,977,054) ambayo inatarajiwa kutoa ajira zipatazo 2,228 kwa wananchi;

7. Imefanikiwa kufanya uwekezaji katika Visiwa 16 Unguja na Pemba wenye mtaji wa Dola za Kimarekani Milioni Mia Tatu Tisini na Tisa na Laki Tano ($399,500,000).

8. Imetoa mikopo 2,177 yenye thamani ya Shilingi Bilioni Kumi na Nne, Milioni Ishirini na Saba, Thamanini na Tano Elfu, Mia Tano na Senti Ishirini na Nane (TSh.14,027,085,506.28). Unguja Shilingi Bilioni Tisa Milioni Thalathini na Tisa, Thamanini na Mbili Elfu, Mia Nane Thalathini (Tsh.9,339,082,830) na Pemba Bilioni Nne Milioni Mia Sita Thamanini na Nane, Elfu Mbili, Mia Sita Sabini na Mbili, Senti Ishirini na Nane (Tsh.4,688,002,672.28) na imewanufaisha Wajasiriamali 8,311 (Unguja 5,301 na Pemba 3,010).

9. Imesaini Makubaliano na Benki ya Equity na Tanzania Postal Benki (TPB) kutoa mikopo kwa Wananchi kupitia Fedha za Mfuko wa Khalifa. Programu hiyo hadi sasa imetoa mikopo ya jumla ya Shilingi Bilioni Moja Milioni Mia Tisa Hamsini na Tano tu (TSh. 1,955,000,000) ambapo kwa Unguja ni Bilioni Moja Milioni Mia Saba

na Kumi na Tano tu (TSh. 1,715,000,000) na Pemba ni Milioni Mia Mbili Arobaini Elfu tu (TSh. 240,000,000). Mikopo hiyo imetekeleza miradi 16 (Unguja 14 na Pemba 2) ambayo inategemewa kutoa ajira 336 (Unguja 184 na Pemba 152).

10. Imekusanya marejesho ya mikopo Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Nane na Thamanini, Laki Moja Sabini na Tano Mia Moja Arobaini na Nane na Senti Thamanini na Moja (TSh 3,880,175,148.81) ambayo sawa na asilimia 27.6 ya fedha zilizotolewa kipindi hiki.

11. Imekusanya Jumla ya shilingi Milioni Mia Tano Tisini na Tano, Laki Moja Tisini na Tatu Elfu, Mia Moja Kumi na Nne na senti Nne (Tsh 595,193,114.04) fedha za asilimia 10 za Mamlaka za Serikali za Mitaa. Afisi imefanya mazugumzo na Benki ya Equity na Tanzania Postal Benki (TPB) kwa ajili ya ushirikiano wa kuzitoa fedha hizo za Halmashauri na Miongozo ya kutolewa fedha hizo imeshaandaliwa kwa kushirikiana na.

12. Imewaunganisha wajasiriamali 221 (wanaume 51 na wanawake 170) kuhudhuria katika maonesho mbali mbali ikiwemo maadhimisho ya siku ya wanawake duniani yaliyofanyika katika viwanja vya Mapinduzi Squre ili kuuza biashara zao na kuzitangaza katika soko.

13. Imetoa mafunzo kwa Wajasiriamali 1,308 (Wanawake 1,011 na Wanaume 297) katika fani ya Uokaji mikate, vifaa vya umeme wa jua, kutengeneza sumu yanyuki na royal jelly, kuimarisha bidhaa na masoko, ujasiriamali, taratibu za mikopo, fursa za ajira na masoko mtandao (E-Marketing).

14. Imesajili vyama vya ushirika Elfu Moja, Mia Nane na Ishirini na Mbili (1,822) ambapo Unguja ni Elfu moja na thelathini na sita (1,036) na Pemba ni Mia saba na themanini na sita (786), kati ya hivyo SACCOS 2 na vyama vya uzalishaji na utoaji huduma 1,820.Vyama hivi vinafanya shughuli za uanikaji wa dagaa, kilimo, Utalii, huduma za simu na mtandao na kazi za mikono.

15. Imekamilisha uandaaji wa Mpango Mkakati wa Afisi ambao utaongoza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya Afisi kwa miaka mitano; imekamilisha uandaaji wa Agenda za Utafiti za Afisi na Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Afisi.

16. Imeandaa Wasifu wa Miradi (Project Profile) kwa Afisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji ambayo imekusanya miradi 14 inayotarajiwa kutekelezwa na Afisi kwa kipindi cha miaka mitatu.

17. Imekamilisha uandaaji wa Mpango wa Rasilimali Watu wa Afisi ambao utasaidia kutambua mahitaji ya watendaji, kupandishwa cheo, mafunzo n.k.

18. Imetatua changamoto za Wananchi kutoka hoja 181 kwa mwaka 2022 hadi hoja 31 kwa mwaka 2023 kupitia Mfumo wa Sema na Rais Mwinyi. Hii inadhirisha kuimarika kwa ufanisi wa kiutendaji.

19. Imefanikiwa kuanzisha Fao la Upotevu wa Ajira kwa kushirikiana na ZSSF.

## 3.2 CHANGAMOTO

**22. Mheshimiwa Spika,** Mbali ya mafanikio yaliyopatikana, kuna changamoto mbali mbali zimejitokeza katika utekelezaji nazo ni kama zifuatazo:-

1. Upungufu wa Wafanyakazi wataalam hasa katika Idara ya Usalama na Afya Kazini (OSH) na Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (ZEEA) na katika masuala ya utafiti, ufuatiliaji na tathmini, kuchambua miradi ya PPP na IT.
2. Ufinyu wa bajeti ambao hauendani na mahitaji ya utekelezaji wa majukumu ya Afisi ambao pia unapelekea upungufu wa vifaa na vyombo vya usafiri.
3. Uendelezaji wa miundombinu ya barabara katika eneo huru la uwekezaji Micheweni umechukuwa muda mrefu kukamilika, jambo ambalo limepunguza kasi ya uharaka kwa kutumika eneo hilo kwa uwekezaji.
4. Idadi kubwa ya maombi ya mikopo kulingana na fedha zilizopo za utoaji wa mikopo na kasi ya urejeshaji wa mikopo hiyo.
5. Wafanyakazi katika Sekta Binafsi kutopewa Mikataba na Waajiri wao, hali amabyo inawakosesha kupata haki na Mafao yao.

## 3.3 UTATUZI WA CHANGAMOTO

**23. Mheshimiwa Spika**, Kutokana na changamoto zilizopo Afisi imejaribu kuzitatua kama ifuatavyo:-

1. Afisi imewasilisha maombi ya Wafanyakazi wataalamu wa fani na maeneo mbali mbali zenye upungufuna inaendelea kufanya mawasiliano na Afisi ya

Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma kwa kupata nafasi hizo kwa mujibu wa 'Nominal Role' na imefanikiwa kupata nafasi sabini (70) kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

2. Afisi imewasilisha maombi ya vyombo vya usafiri ikiwemo gari 6 (4 katika mpango wa manunuzi wa mwaka 2021/2022 na 2022/2023 na gari 2 kutoka fedha za Uviko). Pia, imefanya majadiliano na Afisi ya Rais, Fedha na Mipango ili kuingiziwa bajeti ya kutosha kutekeleza shughuli zilizopangwa na ununuzi wa vitendea kazi. Aidha, imeandaa maandiko ya miradi 14 na kuiwasilisha kwa Washirika wa Maendeleo ili kuweza kusaidia utekelezaji wa baadhi ya majukumu ya Afisi.

3. Afisi kwa kushirikiana na Kamati ya Bajeti imeamua kufanya Kikao cha pamoja na Mkandarasi kujadiliana kuhusu changamoto ya ucheleweshaji wa ujenzi wa miundombinu hiyo na hatua za kuchukua. Aidha, Mkandarasi UBB ameahidi kukamilisha kazi hiyo katika mwezi wa Aprili, 2023.

4. Afisi imeifanyia kazi maeneo ya fedha nyengine za mikopo ikiwemo fedha za Halmashauri asilimia 10 na fedha za SMIDA ili kuweka miongozo mizuri ili baadhi ya waombaji waweze kupatiwa fedha hizo. Vile vile, Wakala inaendelea na mikakati na ufuatiliaji wa urejeshaji wa fedha za mikopo ili ziweze kuzungushwa kwa wengine. Aidha, Wakala inakamilisha tathmini ya maombi pamoja na kuandaa mkakati wa ukopeshaji kwa lengo la kupata fedha kupitia taasisi za kifedha. Aidha, Afisi imewasiliana na Mabenki kama EQUITY, TADB, PBZ, BOA, CRDB na AMANA na imewasilisha

maombi ya ziada kwa Tume ya Mipango kwa ajili ya kupata fedha za maombi ya ziada.

5. Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekekzaji kupitia Kamisheni ya Kazi inaendelea na ukaguzi katika Sekta Binafsi ambapo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imefanikiwa kukagua taasisi 243 (Unguja 164 na Pemba 79) na kusimamia upatikanaji wa Mikataba kwa wafanayakazi wote.

## 4.0 UTEKELEZAJI WA MALENGO YA AFISI YA RAIS, KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

**24. Mheshimiwa Spika;** Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ilijiwekea malengo yafuatayo:-

1. Kukuza na kusimamia Uwekezaji kwa Maendeleo ya Nchi;
2. Kubuni fursa za ajira nchini na kusimamia upatikanaji wa ajira za staha hasa katika Sekta Binafsi;
3. Kusimamia utekelezaji wa Mikataba, Sheria na Kanuni za Kazi za Kitaifa, Kikanda na Kimataifa na kuimarisha mahusiano mazuri ya Kazi miongoni mwa Serikali, Sekta Binafsi, Waajiri na Vyama vya Wafanyakazi;
4. Kuimarisha Usalama na Afya kazini;
5. Kukuza na kusimamia Maendeleo ya Vyama vya Ushirika;
6. Kuimarisha na kukuza Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;
7. Kukuza na kuimarisha mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta binafsi;

8. Kuratibu uandaaji na utekelezaji wa Sera, Sheria, Programu na Tafiti zinazohusiana na masuala yaKazi, Ajira, Uwekezaji, Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi na Uwezeshaji;
9. Kuimarisha uratibu, mashirikiano, ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za Afisi pamoja na kuelimisha jamii juu ya shughuli za Afisi kupitia Mfumo wa TEHAMA; na
10. Kuimarisha ufanisi wa kiutendaji na maslahi ya Wafanyakazi wa Afisi.

**25. Mheshimiwa Spika;** Afisi inatekeleza majukumuyake kupitia Mfumo wa Bajeti ya PBB na ina mafungu mawili tofauti ya matumizi ambayo ni fungu A07 (Kazi na Uwezeshaji) ambalo lina Programu Kuu 3 na Programu Ndogo 9 na fungu A08 (Uchumi na Uwekezaji) lenye Programu Kuu 2 na Programu Ndogo 4 kama zinavoonekana katika **Kiambatanisho nambari 2 kinahusika**.

**26. Mheshimiwa Spika;** Utekelezaji wa Malengo na Programu hizi umezingatia Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2020-2025; Dira ya Maendeleo 2050; Mkakati wa Maendeleo wa Zanzibar 2021/2026, Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia 2030, Afrika tuitakayo 2063, Muongozo wa Uwekezaji Zanzibar, pamoja na Mpango Mkakati wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji.

# 5.0 MUHTASARI WA MAPATO NA MATUMIZI KWA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 KWA FUNGU A07 (KAZI NA UWEZESHAJI) NA FUNGU A08 (UCHUMI NA UWEKEZAJI)

## 5.1 MUHTASARI WA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

### 5.1.1 FUNGU A07 (KAZI NA UWEZESHAJI)

27. **Mheshimiwa Spika;** Afisi ya Rais, Kazi Uchumina Uwekezaji katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023, kupitia fungu A07 (Kazi na Uwezeshaji) ilitarajiwa kukusanya mapato ya Shilingi Bilioni Mbili na Milioni Mia Moja (Tshs.2,100,000,000) kupitia vianzio vya ada za usajili na ukaguzi wa vyama vya ushirika, ada ya ukaguzi wa mikataba ya ajira nje ya nchi, adaya ukaguzi wa maeneo ya kazi na vibali vya kazi. Kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi 2023, Afisi ilitarajiwa kukusanya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Sita Kumi na Mbili na Laki Mbili (TSh.1,612,200,000). Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2023. Afisi ilifanikiwa kukusanya jumla ya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Nne Thamanini na Nne, Laki Tano Arobaini na Moja, Mia Nne Thamanini na Tisa (Tsh.1,484,541,489) ambayo sawa na asilimia 92.1 ya makadirio ya makusanyo kwa miezi 9 na asilimia 70.7 ya makusanyo kwa mwaka.**(Kiambatanisho nambari 3 kinahusika)**.

## 5.2 MUHTASARI WA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

### 5.2.1 MUHTASARI WA MATUMIZI KWA FUNGU A07 (KAZI NA UWEZESHAJI)

28. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kupitia fungu A07 (Kazi na Uwezeshaji) ilikadiriwa kutumia jumla ya Shilingi Bilioni Thalathini na Nne, Milioni Mia Nane Sabini, Laki Moja na Ishirini Elfu (Tsh.34,870,120,000). Afisi baada ya kuzihaulisha Shilingi Bilioni Nane na Milioni Mia Moja (Tsh.8,100,000,000) kwenda SMIDA kutekeleza Mradi wa Ujenzi wa Vituo Jumuishi vya Wajasiriamali pamoja na kuingiziwa Shilingi Milioni Mia Tatu Ishirini na Nne, Laki Sita Arobaini na Tisa, Mia Tatu Sabini na Nane (Tsh.324,649,378) za kukidhi malipo ya Mishahara, Afisi ilibakiwa na Shilingi Bilioni Ishirini na Saba, Milioni Tisini na Nne, Laki Saba Sitini na Tisa Elfu, Mia Tatu Sabini na Nane (Tsh.27,094,769,378). Kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Afisi ilikadiriwa matumizi ya Shilingi Bilioni Ishirini na Nne, Milioni Mia Sita Tisini na Tisa, Laki Nne Tisini na Tatu Elfu na Sabini na Tano (Tsh.24,699,493,075).

29. **Mheshimiwa Spika,** Kati ya fedha hizo Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tisa Tisini na Nne, Laki Tano Hamsini na Saba Elfu, Mia Sita Arobaini na Tatu (Tsh.1,994,557,643) ni kwa ajili ya Mishahara; Shilingi Milioni Mia Sita Thamanini na Nane, Laki Nne Thamanini na Sita Elfu na Mia Nne (Tsh.688,486,400) kwa ajili ya Ruzuku ya Mishahara; Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Saba Thalathini na Saba, Laki Mbili Arobaini na Sita Elfu, Mia Tisa Thalathini na

Mbili (Tsh.1,737,246,932) ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida; Shilingi Milioni Mia Saba Sabini na Tisa, Laki Mbili Elfu Mbili na Mia Moja (Tsh.779,202,100) ni kwa matumizi ya Ruzuku na Shilingi Bilioni Kumi na Tisa na Milioni Mia Tano (Tsh.19,500,000,000) kwa kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

30. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia tarehe 31 Machi 2023, fedha zote zilizoingizwa kwa matumizi ni Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Saba Tisini na Mbili, Elfu Sita, Mia Nne Arobaini na Tatu (TSh.3,792,006,443) ambayo ni sawa na asilimia 15.4 ya utekelezaji wa Program zote kwa kipindi hicho. Kati ya fedha hizo Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tisa Tisini na Nne, Laki Tano Hamsini na Saba Elfu, Mia Sita Arobaini na Tatu (Tsh.1,994,557,643) ni kwa ajili ya Mishahara ambayo sawa na asilimia 100; Shilingi Milioni Mia Sita Thamanini na Nane, Laki Nne Arobaini na Sita Elfu na Mia Nne (Tsh.688,486,400) kwa ajili ya Ruzuku ya Mishahara ambayo ni sawa na asilimia 100; Shilingi Milioni Mia Nane Tisini na Tatu, Laki Tisa Sitini na Sita na Mia Nne (Tsh.893,966,400) ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambayo sawa na asilimia 51.5; Shilingi Milioni Mia Mbili Kumi na Nne, Laki Tisa Mia Tisa Tisini na Sita Elfu (Tsh.214,996,000) ziliingizwakwa matumizi ya Ruzuku ambayo sawa na asilimia 27.6 na hadi Machi 31, 2023 hakuna fedha iliyoingizwa kwa kutekeleza Miradi ya Maendeleo **Kiambatanisho nambari 4(a) kinahusika**.

31. **Mheshimiwa Spika,** Kati ya fedha hizo Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Moja Tisini na Saba, Laki Sita Thamanini na Nane Elfu na Mia Tano (TSh.1,197,688,500) ni kwa

ajili ya kutekeleza Programu ya usimamizi wa Sheria za Kazi, Ukaguzi Kazi na Kazi za Staha kwa wote;Shilingi Bilioni Ishirini, Milioni Mia Tano Sitini na Sita (TSh.20,566,000,000) kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Tisa Thalathini na Tano, Laki Nane na Elfu Nne, Mia Tano Sabini na Tano (TSh.2,935,804,575) ni kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Rais, Kazi Uchumi na Uwekezaji.

**32. Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Mwezi Machi,2023 jumla ya Shilingi Milioni Mia Nane Hamsini na Nane, Laki Tatu Elfu Tisa na Mia Nne (TSh.858,309,400) zilitumika kwa ajili ya kutekeleza Program ya Usimamizi wa Sheria za Kazi, Ukaguzi Kazi na Kazi za Staha kwa Wote ambayo ni sawa na asilimia 71.7 ya fedha kwa Program hiyo. Shilingi Milioni Mia Tisa Tisini na Nane, Laki Tano Arobaini Elfu, Mia Moja na Tisini (TSh.998,540,190) zilitumika kwa kutekeleza Programu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ambayo ni sawa na asilimia 4.9 na Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tisa Thalathini na Tano, Laki Moja Hamsini na Sita, Mia Nane Hamsini na Tatu (TSh.1,935,156,853) zilitumika kutekeleza Program ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji sawa na asilima 65.9 ya fedha za Program hiyo kwa kipindi hicho. **Kiambatanisho nambari 4(b) kinahusika**.

### 5.2.2 MUHTASARI WA MATUMIZI KWA FUNGU A08 (UCHUMI NA UWEKEZAJI)

33. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2022/2023, kupitia fungu A08 (Uchumi na Uwekezaji) ilikadiriwa matumizi ya jumla ya Shilingi Bilioni Ishirini, Milioni Thamanini na Tisa, Elfu Sita, Mia Mbili na Ishirini na Saba (TSh.20,089,006,227). Kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi 2023, Afisi ilikadiriwa matumizi ya Shilingi Bilioni Kumi na Tano, Milioni Mia Tatu Ishirini na Mbili, Laki Tisa Tisini na Mbili Elfu, Mia Moja Sitini na Nane (TSh.15,322,992,168). Kati ya fedha hizo Shilingi Milioni Mia Sita na Nane, Laki Sita Tisini na Nane na Sabini na Tano (Tsh.608,698,075) ni kwa ajili ya Mishahara; Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Mbili Hamsini na Nane, Laki Tatu Ishirini na Mbili, Mia Mbili Hamsini (Tsh.1,258,322,250) ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida; Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Moja Thalathini, Laki Tisa Sabini na Moja Elfu, Mia Nane Arobaini na Tatu (Tsh.2,130,971,843) ni Ruzuku ya Mishahara na Shilingi Bilioni Kumi na Moja, Milioni Mia Tatu Ishirini na Tano (Tsh.11,325,000,000) kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

34. **Mheshimiwa Spika,** Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni Kumi na Tatu, Milioni Mia Nane Hamsini na Tisa, Laki Moja Kumi na Moja Elfu, Mia Tano Arobaini na Tatu (TSh.13,859,111,543,) ni kwa ajili ya kutekeleza Programu Kuu ya Kuimarisha Uwekezaji na Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi na Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Nne Sitini na Tatu, Laki Nane Thamanini Elfu, Mia Tatu Ishirini na Tano (TSh.1,463,880,325) kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji.

**35. Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2023, fedha zilizoidhinishwa kwa matumizi kwa fungu A08 ni Shilingi Bilioni Nne, Milioni Mia Sita Ishirini na Sita, Laki Tatu Kumi na Tano Elfu, Mia Sita Hamsini na Moja (TSh.4,626,315,651) ambayo ni sawa na asilimia 30.19 ya utekelezaji wa Programu zote kwa kipindi hicho. Kati ya fedha hizo Shilingi Milioni Mia Tano Hamsini na Nane, Laki Tatu Sitini Elfu; Mia Nane na Kumi (Tsh.558,360,810) zilitumika kwa Mishahara ambayo sawa na asilimia 91.73; Shilingi Milioni Mia Tatu Sabini na Nane, Laki Sita Thamanini na Sita Elfu na Mia Saba (Tsh.378,686,700) zilitumika kwa Matumizi ya Kawaida ambayo sawa na asilimia 30.9; Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Moja Tisini na Sita, Laki Tisa Thamanini na Tano Elfu, Mia Tisa Tisini na Moja (Tsh.2,196,985,991) zilitumika kwa Ruzuku ambayo sawa na asilimia 103.10 na Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Nne Tisini na Mbili, Mia Mbili Thamanini na Mbili Elfu, Mia Moja Hamsini (Tsh.1,492,282,150) zilitumika kwa kutekeleza Miradi ya Maendeleo ambayo sawa na asilimia 13.18

**36. Mheshimiwa Spika,** Kati ya fedha hizo Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Nane Hamsini na Moja, Laki Nane Ishirini na Sita Elfu, Mia Nne Thalathini na Moja (TSh.3,851,826,431) ziliingizwa kwa matumizi ya Programu ya Kuimarisha Uwekezaji na Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ambayo sawa na asilimia 27.7 ya makadirio na Shilingi Milioni Mia Saba Sabini na Nne, Laki Nne Thamanini na Tisa Elfu, Mia Mbili Ishirini (TSh.774,489,220) zilitumika kutekeleza Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji ambazo sawa na asilimia 52.91 ya makadirio.**Kiambatanisho nambari 5 a na 5b kinafafanua**.

## 6.0 UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA FUNGU A07 (KAZI NA UWEZESHAJI)

## 6.1 PROGRAMU KUU PA0702: USIMAMIZI WA SHERIA ZA KAZI, UKAGUZI KAZI NA KAZI ZA STAHA KWA WOTE

**Matokeo ya Muda Mrefu:** Kuwepo kwa Sehemu za Kazi zinazokidhi Viwango vya Usalama na Afya.

37. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii Kuu kwa mwaka wa Fedha 2022/2023 ilitengewa kiasi cha Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Moja Tisini na Saba, Laki Sita Thamanini na Nane Elfu na Mia Tano (Tsh.1,197,688,500) mpaka kufikia mwezi Machi, 2023 imeidhinishiwa kiasi cha Shilingi Milioni Mia Nane Hamsini na Nane, Laki Tatu Elfu Tisa na Mia Nne (TSh.858,309,400) (Matumizi ya Kawaida 169,823,000 na Mishahara 688,486,400) sawa na asilimia 71.7 ya utekelezaji wa programu zake ndogo.

### 6.1.1 Programu Ndogo SA070201: Uratibu wa Upatikanaji wa Ajira za Staha.

38. **Mheshimiwa Spika;** Programu Ndogo (SA070201) ya Uratibu na Upatikanaji wa Ajira za Staha ina lengo la Kuimarisha Ajira za Staha. Kwa kipindi cha Julai2022 hadi Machi 2023, Programu imeidhinishiwa kiasi cha Shilingi Milioni Thamanini, Laki Sita Hamsini na Tano Elfu (TSh.80,655,000) hadi kufikia mwezi Machi, 2023 imeidhinishiwa matumizi ya kiasi cha Shilingi Milioni Thalathini na Nane, Laki Mbili Arobaini Elfu (TSh.38,240,000) sawa na asilimia 47.4. Programu imetekeleza yafuatayo:-

1. Inaendelea kuratibu Programu za kukuza ujuzi kwa Vijana ili waweze kujiajiri na kuajiriwa, kwa upande wa Programu ya Mafunzo Kazi Jumla ya Vijana 36 (Wanaume 23 na Wanawake 13) wanaendelea na mafunzo hayo ambapo Vijana hao wanajifunza fani ya Hotelia. Program hii inafanyika kwa mashirikiano na Chuo Kikuu cha Taifa – Taasisi ya Utalii Maruhubi (SUZA- IoT).

2. Imeratibu upatikanaji wa Ajira za nje ya Nchi kwa Vijana 1,080 (Wanaume 428 na Wanawake 652) kwa kazi za Ulinzi, Kazi za Majumbani, Udereva, Vibarua nk. katika Nchi za Oman, Saudi Arabia, Qatar, Kuwait, UAE nk. Aidha, jumla ya ajira rasmi za ndani 6,348 (Wanaume 4,142 na Wanawake 2,206) za sekta binafsi zimepatikana zinazojumuisha kazi za Mahoteli, Skuli Binafsi, Hospitali Binafsi, Kampuni za mawasiliano, ujenzi nk.

3. Imeratibu Mafunzo Kazi ya muda mfupi kwa Vijana Wasio na Ajira, Elimu na hawapo katika Mafunzo (NEET) 87 (Wanaume 43 na Wanawake 44). Mafunzo hayo yametolewa katika Skuli ya Sekondari ya Ufundi ya Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) na yalikuwa katika fani ya Ushoni, Ufundi Seremala, Ufundi Mafriji na Vipoza hewa.

4. Imeratibu shughuli za Uwakala Binafsi wa Ajira kwa kuzipatia leseni taasisi mbili ambazo ni Baitul Khalij iliopo Fuoni na A and F Company Limited iliopo Malindi ili kuungana na taasisi kongwe katika kuwasaidia Vijana kupata ajira. Aidha, Programu imefanya ukaguzi kwa Taasisi tatu za Uwakala Binafsi wa Ajira ili kuangalia hali halisi ya utekelezaji wa majukumu yao

kwa mujibu wa sheria. Taasisi zilizokaguliwa ni Hilmi Manpower Agency, Blue Agency Company Limited na Global Manpower and Patners Agency.

5. Inaendelea kukamilisha Mapitio ya Mpango wa Utekelezaji wa Ajira kwa Vijana ambapo Programu kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani imeshafanya hatua kadhaa ikiwemo kukutana na wadau muhimu wa Mpango huo unaolenga kuchangia uzalishaji zaidi wa fursa za ajira Nchini.
6. Imeshiriki mikutano muhimu ya kujadili Utekelezaji wa Mkataba wa Makubaliano wa kuwapeleka Watanzania Nchini Qatar kwa ajili ya kufanya kazi. Katika utekelezaji wa Mkataba huo, Programu kwa kushirikiana na Taasisi za Uwakala imeandaa Mpango Kazi maalum wa kuhakikisha Vijana wa Kitanzania wananufaika na fursa zilizopo Nchini Qatar na wanaelewa taratibu na Sheria za nchi wanazokwenda.
7. Imeratibu shughuli za ajira nje ya nchi kwa kukutana na Wadau pamoja na kuweka Miongozo ya kulisimamia kwa pamoja suala hilo.
8. Imefanya mafunzo ya ukusanyaji wa takwimu za Ajira wa Wilaya Unguja na Pemba.

39. **Mheshimiwa Spika;** Programu ya Uratibu wa upatikanaji wa Ajira za Staha kwa mwaka wa fedha 2023/24, imepanga kutekeleza yafuatayo:-

1. Itaendelea kuratibu upatikanaji wa ajira za ndani 10,000 na ajira nje ya nchi 1,500.
2. Itaendeleza Programu za kukuza ujuzi kwa Vijana 55 Wasio na Ajira na Hawapo katika Mafunzo yoyote (NEET Programs);

3. Itaendelea kuufanyia mapitio na kuimarisha Mfumo wa Taarifa za Soko la Ajira ili kuendana na wakati wa sasa hasa katika upatikanaji wa taarifa na takwimu za ajira za ndani na nje ya Nchi;
4. Itaimarisha mashirikiano na wadau wa nje na ndani katika kutafuta fursa za ajira kwa Vijana;
5. Itaendeleza programu za kujenga uzoefu wa kufanya kazi (Internship) kwa Vijana 55 wahitimu wa fani mbali mbali ili kuwajengea uwezo wa kujiamini katika kazi;
6. Itaendelea kutoa elimu kuhusu masuala ya ajira kupitia majukwaa tofauti ikiwemo Makongamano, vipindi vya redio na televisheni n.k;
7. Itaratibu utekelezaji wa Mpango wa Ajira kwa Vijana III (Zanzibar Youth Employment Action Plan III) unaolenga kuzalisha fursa za ajira kwa wingi katika sekta tofauti.

**40. Mheshimiwa Spika;** Ili Programu ya Uratibu wa Upatikanaji wa Ajira za Staha iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2023/24, naliomba Baraza lako kuidhinisha ruzuku ya jumla Shilingi Milioni Mia Mbili (TSh.200,000,000) kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida.

### 6.1.2 Programu Ndogo SA070202: Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini.

**41. Mheshimiwa Spika;** Programu Ndogo (SA070202) ya Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini ina lengo la Kuimarisha masuala ya Usalama na Afya katika sehemu za kazi. Kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Programu imetengewa kiasi cha Shilingi Milioni Thamanini

na Nane, Laki Mbili Sabini na Tano Elfu (TSh.88,275,000). Hadi kufikia mwezi Machi, 2023 imepatiwa kiasi cha Shilingi Milioni Arobaini na Tano, Laki Tisa Ishirini Elfu (TSh.45,920,000) sawa na asilimia 52.0. Program imetekeleza yafuatayo:-

1. Imefanya usajili wa sehemu za kazi 76 (59 Unguja na 17 Pemba) ili kuzitambua na kuweka taarifa zao kwenye daftari la usajili wa sehemu za kazi ukilinganisha na taasisi za kazi 62 zilizosajiliwa mwaka jana. Pia, imetoa vyeti 76 vya kukidhi matakwa ya sheria baada ya kukamilisha usajili wa eneo la kazi. Hii inarahisisha shughuli za ukaguzi kwa kutambua mapema mazingira ya kazi zao, hatari na kutoa ushauri mapema.
2. Imefanya ukaguzi wa sehemu za kazi 234 (135 Unguja na 99 Pemba) ili kuangalia hali ya usalama na afya katika maeneo hayo. Ushauri ulitolewa juu ya kurekebisha kasoro zilizobainika. Ufuatiliaji uliofanywa baada ya ukaguzi, umeonesha kuwa kasoro nyingi zimerekebishwa baada ya kufuatwa ushauri uliotolewa. Ukaguzi kwa mwaka huu wa fedha umeongezeka kutoka maeneo 209 mwaka 2021/2022 hadi maeneo 234 mwaka 2022/2023.
3. Imefanya uchunguzi wa matukio ya ajali na maradhi yatokanayo na kazi katika sehemu 9 za kazi ikilinganishwa na sehemu 7 za mwaka 2021/2022 zilizoripotiwa kutokea kwa ajali hizo wakati wafanyakazi wakiendelea na kazi. Wafanyakazi 2 walifariki kwa kuangukiwa na ukuta.

4. Katika kukuza uelewa wa masuala ya usalama na afya kazini, Programu imeandaa na kurusha hewani vipindi kumi na mbili (12) vya redio vinane (8) na vipindi vinne (4) vya televisheni kupitia vyombo mbali mbali vya habari vya binafsi na umma. Vile vile, Programu imetoa mafunzo kwa wawakilishi 200 (100 Unguja na 100 Pemba) wa masuala ya usalama na afya kazini kutoka kwenye Wizara na Taasisi za Umma ili waweze kufahamu majukumu yao na wajibu wao. Aidha, imetoa mafunzo kwa Taasisi saba (7) za Serikali.

5. Imewajengea uwezo watendaji wake kwa kuweza kuhudhuria mikutano na makongamano mbali mbali ya mashirikiano Kitaifa, Kikanda na Kimataifa juu ya Masuala ya Usalama na Afya Kazini na uratibu wa shughuli za usalama na afya kazini unaendelea.

**42. Mheshimiwa Spika,** Programu ya Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini kwa mwaka wa fedha 2023/24 itatekeleza yafuatayo:-

1. Itakagua Sehemu za Kazi 240 na kusajili 120 kuhusu usalama na afya kazini kwa ajili ya kuzitambua na kuweka mpangilio wa kuzikagua;

2. Itaimarisha utekelezaji wa Sheria Nambari 8 ya mwaka 2005 ya Usalama na Afya Kazini;

3. Itatoa elimu kwa wawakilishi wa usalama na afya kazini 200;

4. Itakuza uelewa wa Waajiri, Wafanyakazi na jamii kwa jumla juu ya Sheria na masuala ya Afya na Usalama Kazini;

5. Itapima Afya za Wafanyakazi asilimia 30 (Sekta Binafsi 20% na Sekta ya Umma 10%);
6. Itafanya tathmini ya maradhi na ajali katika sehemu za kazi;
7. Itaimarisha uwezo wa Idara ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake ipasavyo;
8. Itachunguza ajali zinazotokana na kazi; na
9. Kuimarisha mashirikiano na uratibu wa masuala ya Usalama na Afya kazini.

43. **Mheshimiwa Spika;** Ili programu ya Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2023/24, naliomba Baraza lako kuidhinisha ruzuku ya Shilingi Milioni Mia Moja na Tisini (TSh.190,000,000) kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida.

### 6.1.3 Programu Ndogo SA070203: Usimamizi wa Viwango vya Kazi vya Kitaifa na Majadiliano ya Pamoja Kazini

44. **Mheshimiwa Spika;** Programu Ndogo (SA070203) ya Usimamizi wa Viwango vya Kazi vya Kitaifa na Majadiliano ya Pamoja Kazini ina lengo la kuhakikisha kunakuwepo utekelezaji mzuri wa Sheria za Kazi katika Sekta Binafsi na Sekta ya Umma. Kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Programu ilikadiriwa matumizi ya kiasi cha Shilingi Bilioni Moja, Milioni Ishirini na Nane, Laki Saba Hamsini na Nane na Mia Tano (TSh.1,028,758,500); hadi kufikia mwezi Machi, 2023 imepangiwa matumizi ya kiasi cha Shilingi Milioni Mia Saba, Sabini na Nne, Laki Moja Arobaini na Tisa na Mia Nne (TSh.774,149,400) (Ruzuku 85,663,000 na Ruzuku ya Mishahara 688,486,400) sawa na asilimia 75.3 ya utekelezaji.

**45. Mheshimiwa Spika;** Programu imetekeleza shughuli kuu zifuatazo:-

1. Imefanya ukaguzi kazi kwa Taasisi 243 (Unguja 164 na Pemba 79), kwa kuangalia utekelezaji wa sheria za kazi Nchini. Ukaguzi huo unafanyika ili kusimamia ipasavyo utekelezaji wa Sheria za Kazi kwa sekta binafsi hapa Zanzibar. Hata hivyo, idadi ya taasisi zilizokaguliwa mwaka 2022/2023 zimepungua (17.3%) ambapo mwaka 2021/2022 ilikuwa ni taasisi 294. Hii imetokana na ufinyu wa bajeti, hivyo kupelekea Maafisa Kazi kutoweza kufikia baadhi ya Taasisi zilizopangwa.

2. Katika kuhakikisha utekelezaji wa Sheria za Kazi na ulipaji wa kima cha chini cha mishahara cha TSh. (300,000/180,000) kwa toleo la mwaka 2017 katika Sekta Binafsi. Ukaguzi uliofanyika ulibaini kuwa Taasisi 15 (12 Unguja na 3 Pemba) kati ya 243 zilizokaguliwa hazilipi kima hicho cha chini cha mshahara. Taasisi hizo zilipewa maelekezo na kutakiwa kulipa kima hicho. Taasisi 4 zote Unguja zilileta maombi ili zithibitishwe kuwa Taasisi ndogo ambazo hazikuwa na uwezo wa kulipa kima cha Shilingi 300,000/- baada ya tathmini ziliruhusiwa kulipa kima cha chini cha 180,000/-. Taasisi 11 zinaendelea kufanyiwa ufuatiliaji na zimepewa muda maalum wa kurekebisha kasoro hiyo. Endapo muda utaisha bila ya kutii maagizo na maelekezo waliyopewa hatua za kisheria zitachukuliwa ili kuhakikisha zinalipa kima sahihi.

3. Vile vile, kwa uwezo aliopewa chini ya Sheria ya Ajira nam. 11 ya mwaka 2005, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji ameshatowa amri ya kulipwa kima kipya cha mshahara baada ya

kutangazwa katika Gazeti rasmi la Serikali la tarehe 24 Machi, 2023 lililochapishwa kwa toleo nam. 43 ambacho kitaanza kutumika rasmi mnamo mwezi wa Mei, 2023 kwa ufafanuzi ufuatao:-

a. Wafanyakazi wenye hadhi ya kuwa na Mikataba ya maandishi mshahara umeongezeka kutoka Tsh. 300,000 hadi TSh.347,000.

b. Wafanyakazi wenye hadhi ya kuwa na Mikataba ya maandishi kwa Taasisi ndogo mshahara umeongezeka kutoka TSh.180,000 hadi TSh.250,000/-.

c. Wafanyakazi wenye hadhi ya kuwa na Mikatabaya masharti ya kutwa wenye ujuzi (daily paid skill labourers) mshahara utakuwa ni TSh.30,000 kwa siku.

d. Wafanyakazi wenye hadhi ya kuwa na Mikataba ya masharti ya kutwa wasio na ujuzi (daily paid unskill labourers) mshahara utakuwa ni TSh.25,000 kwa siku.

e. Wafanyakazi wa ndani wanaoishi katika nyumba ya mwajiri mshahara umeongezeka kutoka TSh.80,000/- hadi TSh.100,000/- kwa mwezi.

f. Wafanyakazi wa ndani wanaokwenda na kurudi ambao hawaishi katika nyumba ya mwajiri mshahara umeongezeka kutoka TSh. 80,000/- hadi TSh. 120,000/- kwa mwezi.

g. Wafanyakazi wa kigeni watatakiwa kulipwa kima kisichopunguwa Dola za Kimarekani $1000.

4. Imewapatia Vibali vya Kazi jumla ya Wafanyakazi wa Kigeni 2,248. Kati ya hao 169 Walipata msamaha wa Mheshimiwa Waziri, 177 Waliopata msamaha wa ZIPA yaani (Exemption ZIPA), Vibali vipya 757, Vibali vilivyoongezewa muda 794 na vya muda mfupi 351. Vibali vyote hivi ni vya Wafanyakazi wageni kutoka katika Mataifa ya Afrika ya Kusini, Kenya, Britain, Zambia, Ujerumani, Yemen, Marekani, Sudan, Canada n.k kuweza kufanya kazi Nchini na wanafanyakazi kwenye sekta Binafsi na Sekta za Umma ambazo ni Mahoteli, Skuli, Utalii, Sehemu za Ujenzi, NGO, Sehemu za Afya n.k.

5. Vile vile, imethibitisha Mikataba ya kazi kwa Wafanyakazi wazalendo (locals) 6,412 (Unguja 5,563 na Pemba 849) ili kuhakikisha inaendana na Sheria za Kazi. Mkoa wa Kaskazini Unguja Mikataba 1,632, Kusini Unguja Mikataba 1,531 na Mjini Magharibi Mikataba 2,400, Mkoa wa Kaskazini Pemba Mikataba imethibitishwa Mikataba 450 na Mkoa wa Kusini Pemba Mikataba 399.

6. Kupitia Kitengo cha Usuluhishi na Uamuzi wa Migogoro ya Kazi – Migogoro iliyowasilishwa ni 149, kati ya hiyo iliyomalizika kwa hatua ya usuluhishi 57, inayoendelea katika hatua ya usuluhishi ni 39, inayoendelea katika hatua ya Uamuzi ni 37 na iliyofutwa kwa sababu za kutofika wawasilishaji wa migogoro husika na waliowasilisha mgogoro nje ya muda bila ya uwepo wa sababu za msingi ni 16.

7. Imefanya ukaguzi katika Vyama 6 ambavyo ni ZAPSWU sehemu ya SUZA na Maruhubi (Chuo cha Utalii), COTWU-Z Afisi kuu, ZATU Afisi kuu, ZAFICOWU Tawi

la Kazi la Kampuni ya SGA Security Company, Security Master Co-operation, ZUPHE Afisi kuu, na TUICO (Z) Afisi kuu. Ukaguzi huo umebaini kuwa vyama vyote hivyo vinafanya kazi zake kulingana na Katiba za Vyama vyao zinavyoelekeza ikiwemo kufanya vikao vya chama kikatiba, kuhifadhi kumbukumbu za chama na kuwasilisha ripoti za mwaka kwa Mrajis.

8. Aidha, Programu imepokea malalamiko 3 yanayohusu Vyama vya Wafanyakazi dhidi ya Waajiri na Wanachama dhidi ya Chama chao ambapo chama kinachohusika na Wafanyakazi wa Viwanda (TUICO –Z) ambapo malalamiko yao yalipatiwa ufumbuzi.

9. Jumla ya taasisi 32 (14 Unguja na 18 Pemba) zilipatiwa elimu ya taratibu za Sheria na Kanuni za Kazi, haki na Wajibu wa Wafanyakazi na Waajiri. Pia, vilirushwa hewani vipindi 129 vya kuelimisha jamii, katika vyombo mbali mbali vya Habari vikiwemo; ZBC Redio, ZBC TV, Habari FM, Kati FM, AdhanaFM, Assalam FM, Mtegani FM, na Bahari FM. Lengo hasa la utoaji wa elimu ni kuwapa uelewa Waajirina Wafanyakazi juu ya Sheria za Kazi, haki, wajibu pamoja na stahiki zao wanapokuwa katika maeneo yao ya kazi.

**46. Mheshimiwa Spika;** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Programu ya Usimamizi wa Viwango vya Kazi vya Kimataifa na Majadiliano ya Pamoja, mbali na majukumu mengine itatekeleza yafuatayo:-

1. Itafanya ukaguzi kwa Taasisi 600 (Unguja 500 na Pemba 100);

2. Itathibitisha mikataba ya kazi kwa Wafanyakazi wazalendo 5,000;

3. Itakagua Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri 14;
4. Itatoa elimu ya Sheria za Kazi kwa taasisi 45;
5. Itarusha vipindi 75 kupitia vyombo vya habari;
6. Itaendelea kutoa vibali 2,000 kwa wageni wanaokuja kufanya kazi nchini; na
7. Itaendelea kufanya ziara na kuwatoa watoto 30 (Unguja 10 na Pemba 20) wanaojishughulisha na ajira na kuwarejesha skuli kwa Unguja na Pemba.

**47. Mheshimiwa Spika;** Ili Programu ya Usimamizi wa Sheria za Kazi, Ukaguzi kazi na Kazi za Staha kwa wote itekeleze majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2023/2024, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya Ruzuku ya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tatu Arobaini na Nane na Laki Nne (TSh.1,348,400,000) (Ruzuku ya Kawaida 262,900,000 na Mishahara 1,085,500,000 )kwa ajili ya kazi za kawaida na mishahara

## 6.2 PROGRAMU KUU PA0703: UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

**Matokeo ya Muda Mrefu:** Kila Mzanzibari anafanya Shughuli za Kiuchumi za Kumuwezesha Kumudu Mahitaji yake ya Msingi.

**48. Mheshimiwa Spika,** Programu hii Kuu kwa kipindicha Julai 2022 hadi Machi 2023 cha mwaka wa Fedha 2022/2023 iliidhinishiwa kiasi cha Shilingi Bilioni Ishirini, Milioni Mia Tano Sitini na Sita (Tsh.20,566,000,000) mpaka kufikia mwezi Machi, 2023 imepatiwa matumizi ya kiasi cha Shilingi Milioni Mia Tisa Tisini na Nane, Laki Tano Arobaini Elfu, Mia Moja Tisini (TSh.998,540,190) (Matumizi ya Kawaida 268,951,737 na Mishahara

729,588,453) sawa na asilimia 4.9 ya utekelezaji programu zake ndogo.

### 6.2.1 Programu ndogo SA070301: Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

**49. Mheshimiwa Spika;** Programu Ndogo (SA070301) ya Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ina lengo la kuwawezesha wananchi kupata mitaji na mikopo nafuu ya kufanya shughuli za uzalishaji ili kujiajiri na kuinua kipato chao. Kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Programu imeidhinishiwa kiasi cha Shilingi Milioni Mia Mbili na Sabini (TSh.270,000,000); hadi kufikia mwezi Machi, 2023, imepatiwa matumizi ya kiasi cha Shilingi Milioni Mia Mbili Hamsini na Mbili, Laki Moja Hamsini na Mbili Elfu, Mia Nane Hamsini na Tatu (TSh.252,152,853) (Matumizi ya Kawaida 45,173,000 na Mishahara 206,979,853) sawa na asilimia 93.4. Programu ya Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa kipindi cha mwaka 2022/2023, imetekeleza yafuatayo:-

1. Imefanya vikao na Mabenki mbali mbali kama CRDB, DTB, PBZ, KCB, Benki ya Amana, Equity Bank, BOA, TCB na kujadiliana nao juu ya njia bora za kushirikiana na kuwahamasisha kuyawezesha makundi mbali mbali kwa kuwapatia mitaji na mikopo yenye masharti nafuu, ambapo kwa sasa Programu inashirikiana na Benki ya CRDB kwa upande wa fedha za Uviko 19 na Benki ya Equity kwa upande wa mfuko wa Khalifa.

2. Imekusanya fedha jumla ya Shilingi Milioni Mia Tatu Sabini, Laki Mbili Themanini na Tisa Elfu, Mia Saba Themanini na Moja, Senti Tisini na Tatu (Tsh. 370,289,781.93) Unguja na Pemba. Unguja ni Shilingi Milioni Mia Mbili na Sabini na Moja, Laki Nne Kumi

na Moja Elfu, Mia Moja Sabini, senti Kumi na Tatu (Tsh.271,411,170.13) na Pemba Shilingi Milioni Tisini na Nane, Laki Nane Sabini na Nane Elfu, Mia Sita na Kumi na Moja na Senti Themanini (TSh. 98,878,611.80) zikiwa ni asilimia 10 za mapato ya Halmashauri kwa ajili ya kutoa mikopo kwa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu (kwa mgawanyo wa asilimia 4 kwa Wanawake, asilimia 4 kwa Vijana na asilimia 2 kwa Watu Wenye Ulemavu).

Miongozo ya kutolewa fedha hizo imeshaandaliwa kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kupitia Makatibu Tawala wa Wilaya zote za Unguja na Pemba pamoja na Wakurugenzi wa Halmashauri/ Mabaraza ya Miji. Fedha hizo zitatoka kupitia Wilaya husika ambapo orodha ya vikundi vya Vijana, Wanawake na Watu Wenye Ulemavu itaandaliwa na kuwasilishwa katika Ofisi za Wakala ambapo kwa kushirikiana na watendaji wa Wilaya, masuala ya tathmini yatafanywa kabla ya maombi kuwasilishwa Benki ili kupatiwa fedha hizo. Utoaji wa fedha za Mfuko huo unatarajiwa kuanza kazi mwaka wa fedha 2023/2024.

3. Kupitia mradi wa Mboga na Matunda, mfuko umetoa mikopo 191 Unguja na Pemba yenye thamani ya Shilingi Milioni Mia Moja Thamanini na Tisa na Laki Nne (Tsh.189,400,000). Kati ya fedha hizo, Pemba imetolewa mikopo 120 yenye thamani ya shilingi Milioni Mia Moja na Kumi tu (Tsh.110,000,000) na Unguja imetolewa mikopo 71 yenye thamani ya shilingi Milioni Sabini na Tisa na Laki Nne (Tsh.79,400,000).

4. Imetoa mikopo 1,986 kupitia fedha za INUKA yenye thamani ya shilingi Bilioni Kumi na Tatu, Milioni Mia Nane na Thalathini na Saba, Laki Sita na Themanini na Tano, Mia Tano na Sita, senti Ishirini na Nane (TSh. 13,837,685,506.28) Unguja na Pemba. Unguja mikopo 983 yenye thamani ya Shilingi Bilioni Tisa, Milioni Mia Mbili na Hamsini na Tisa, Laki Sita Thamanini na Mbili, Mia Nane na Thalathini (TSh. 9,259,682,830) na Pemba ni Mikopo 1,003 yenye thamani ya Shilingi Bilioni Nne, Milioni Mia Tano Sabini na Nane, Elfu Mbili Mia Sita Sabini na Sita, Senti Ishirini na Nane (Tsh. 4,578,002,676.28). Mikopo hiyo imewanufaisha wananchi 8,311; (Unguja 5,301 na Pemba 3,010) wanaojishughulisha na shughuli mbali mbali zikiwemo; Bodaboda, Kilimo, Ufugaji ukiwemo wa nyuki, Uchongaji wa mbao, uchomaji wa vyuma, uuzaji wa vyakula na kazi za mikono.

**5.** Mikopo yote ya Program ya INUKA tokea ilivyoanzishwa Machi, 2022 imefikia shilingi Bilioni Kumi na Saba, Milioni Mia Sita Sabini na Mbili, Laki Tatu na Elfu Mbili, Mia Moja Thalathini na Sita senti Ishirini na Nane (Tsh.17,672,302,136.28) zilizoidhinishwa Unguja na Pemba. Unguja, zimetolewa Shilingi Bilioni Kumi, Milioni Mia Sita Kumi na Sita, Laki Tisa na ElfuNane, Mia Mbili Thamanini (Tsh.10,616,908,280) na Pemba Shilingi Bilioni Saba, Milioni Hamsini na Tano, Laki Tatu Tisini na Tatu Elfu, Mia Nane Hamsini na Sita, Senti Ishirini na Nane (Tsh. 7,055,393,856.28).Fedha hizi zimewanufaisha jumla ya wananchi 18,103, Unguja wananchi 9,314 (Wanawake 5,849 na Wanaume 3,465) na Pemba 8,789 (Wanawake 5,424 na Wanaume 3,365) **Kiambatanisho Nambari 6 kinahusika.**

6. Imeratibu Programu ya Maendeleo ya wajasiriamali inayotekelezwa kupitia ruzuku ya Mfuko wa Khalifa na mchango wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Programu hiyo hadi sasa imetoa mikopo ya jumla ya Shilingi Bilioni Moja Milioni Mia Tisa Hamsini na Tano tu (Tsh.1,955,000,000) ambapo Unguja ni shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Saba na Kumi na Tano tu (Tsh.1,715,000,000) na Pemba Shilingi Milioni Mia Mbili na Elfu Arobaini tu (Tsh.240,000,000). Mikopo hiyo imetumika kutekeleza miradi 16 (Unguja 14 na Pemba 2) inayotarajiwa kuzalisha ajira 184 Unguja na Pemba (Wanaume 131 na Wanawake 53).

7. Imeratibu utoaji wa mkopo kutoka Wizara inayohusika na Uchumi wa Buluu ambapo wananchi wamefaidika kwa kukopeshwa boti za uvuvi na boti za kubebea mwani ambapo jumla ya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Nane Arobaini na Saba, Laki Tatu Sitini Elfu, Thamanini na Sita, Senti Thamanini (Tsh.1,847,360,086.80) zimetumika. Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tatu na Moja, Laki Moja Kumi na Sita Elfu, Mia Nne na Kumi (Tsh.1,301,116,410)kwa ajili ya boti za Uvuvi (Unguja ni Shilingi Milioni Mia Saba Ishirini na Nane, Laki Sita na Ishirini na Tano Elfu, Mia Moja Thamanini na Tisa, Senti Sitini (Tsh.728,625,189.60) na Pemba ni Shilingi Milioni Mia Tano Sabini na Mbili, Laki Nne Tisini na Moja Elfu, Mia Mbili Ishirini, Senti Arobaini (Tsh.572,491,220.40).

   Shilingi Milioni Mia Tano Arobaini na Sita, Laki Mbili Arobaini na Tatu Elfu, Mia Sita Sabini na Sita, Senti Themanini (Tsh.546,243,676.80) kwa ajili ya Boti za Mwani (Unguja Shilingi Milioni Ishirini na Nane, Laki Saba Arobaini na Tisa Elfu, Mia Sita Sitini na Saba,

Senti Ishirini (Tsh.28,749,667.20) na Pemba Shilingi Milioni Mia Tano Kumi na Saba, Laki Nne Tisini na Nne Elfu na Shilingi Tisa, Senti Sitini (Tsh.517,494,009.60). Programu hii imewanufaisha wananchi 603; Unguja 326 (Wanaume 227 na Wanawake 99) na Pemba 277 (Wanaume 187 na Wanawake 90).

8. Imekusanya marejesho ya mkopo kupitia fedha za mifuko zilizotolewa kama ifuatavyo:-

   a) Kwa upande wa fedha za Mfuko wa Uwezeshaji ambazo mikopo yake ilitoka kabla ya kuanzishwa Walaka wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, jumla ya Shilingi Milioni Thamanini na Saba Laki Mbili Ishirini na Tatu Elfu Mia Tano (Tsh.87,223,500) zimerejeshwa, ikiwa Unguja ni jumla ya Shilingi Milioni Arubaini na Mbili Laki Tano Thalathini na Saba Elfu (Tsh.42,537,000) na Pemba ni Shilingi Milioni Arubaini na Nne, Laki Sita Thamanini na Sita Elfu na Mia Tano (Tsh.44,686,500).

   b) Kwa upande wa fedha za INUKA tokea mradi huo uanze umefanikiwa kukusanya marejesho ya jumla ya Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Nane Thamanini, Laki Moja Sabini na Tano Elfu, Mia Moja Arobaini na Nane, Senti Thamanini na Moja (Tsh.3,880,175,148.81) ikiwa Unguja ni Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Mbili na Nane, Laki Nne na Elfu Nne, Mia Saba Tisini, senti Sabini na Sita (Tsh.2,208,404,790.76) na Pemba ni Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Sita Sabini na Moja Laki Saba Sabini, Mia Tatu Hamsini na Nane, Senti Tano (TSh 1,671,770,358.05) sawa na asilimia 21.9 ya fedha zote zilizotolewa **Kiambatanisho nambari 7 kinahusika**.

c) Kwa upande wa fedha za Khalifa Fund, Mradi bado haujakusanya marejesho kutokana na wakopaji kupatiwa muda wa nafuu (grace period) wa kipindi cha miezi sita na wengine mpaka mashine zao za uzalishaji zitakapowasili na kuanza kazi.

9. Ili kuhakikisha usimamizi mzuri na ufanisi wa fedha za mikopo, Afisi imeandaa Mfumo wa kuratibu Mfuko wa Uwezeshaji unaojulikana kama 'Yes.id' chini ya Wakala wa Mitandao ya Serikali (E-Gaz) ambao kwa sasa Mfumo huo upo katika hatua ya majaribio. Aidha, changamoto zinazotokana na utumiaji wa Mfumo huo zimewasilishwa katika Taasisi inayohusika na Mifumo ya Serikali (E-Gov) kwa ajili ya marekebisho.

10. Imewapa mafunzo Masheha kuhusu wajibu wao katika kusimamia rasilimali za fedha za Serikali, watu na nyenzo katika maeneo yao kama ilivyo katika Sheria Nambari 8 ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2014 katika kifungu Nambari 8(1), uwepo wa Programu ya Mikopo ya INUKA na Fedha za Halmashauri (4.4.2) pamoja na taratibu zake na kuwataka wawe waadilifu katika kujaza fomu wanazopelekewa, taratibu na mahitaji wanayotakiwa kukamilisha waombaji wa mikopo ambayo inapitia kwao kwanza.

11. Ilishiriki kikamilifu katika ziara za Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi zilizofanyika katika Wilaya zote za Unguja na Pemba, mwezi Julai, 2022 ambapo alikabidhi Hundi za Mikopo kwa Vikundi mbali mbali vya Wajasiriamali wakiwemo Waendesha Boda Boda, Wazalishaji, Wauza Mbao, Vijana na Watu wenye Ulemavu. Pia, ilitembelea Maonesho ya Wajasiriamali,

kukagua bidhaa zao pamoja na kufungua tawi jipya la Benki ya CRDB ambalo limekuwa msaada mkubwa katika uratibu na utoaji wa fedha za Programu ya INUKA kisiwani Pemba.

50. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Programu ya Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi imepanga kutekeleza yafuatayo:-

1. Kuendelea kutoa mikopo 3,000 yenye masharti nafuukwa vikundi vya uzalishaji na Mjasiriamali mmoja mmoja katika sekta za kiuchumi;
2. Kuhakikisha kuwa mikopo inayotolewa inatumiwa ipasavyo na inarudishwa kwa wakati uliopangwa;
3. Kuwaunganisha Wajasiriamali 24,900 na Wafanyabiashara 100 na Taasisi za kifedha;
4. Kusimamia marejesho ya mikopo asilimia 95% ya mikopo.
5. Kuratibu utekelezaji wa shughuli za Wakala wa Viwanda Vidogo Vidogo na vya Kati;
6. Kuimarisha uwekaji na usimamizi wa kumbukumbu za wateja kwa kutumia Mfumo wa Kielektrionik ambaokwa sasa upo katika hatua za matayarisho;
7. Kuendelea na juhudi za kutunisha fedha kwa kuandaa miradi miwili ili Mfuko uendelee kuwasaidia wajasiriamali wengi zaidi;
8. Kuimarisha mashirikiano na uratibu wa shughuli za mikopo nafuu hapa Nchini;
9. Kuimarisha uwezo wa watendaji ili kuongeza ufanisi wa kazi;

10. Kufanya Mapitio ya Muongozo wa Usimamizi waMikopo ili uende sambamba na mabadiliko ya Sera naSheria mpya; na

11. Kuimarisha uratibu na taasisi za fedha Nchini.

**51. Mheshimiwa Spika;** Ili Programu ya Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2023/24, naliomba Baraza lako kuidhinisha ruzuku ya Shilingi Bilioni Tisa, Milioni Mia Moja na Nne, Laki Tisa Hamsini na Mbili Elfu (Tshs.9,104,952,000) (Ruzuku 1,046,100,000, Mishahara 928,246,000, Maendeleo SMZ 4,500,000,000 na Washirika wa Maendeleo 2,540,606,000).

**6.2.2. Programu Ndogo: SA070302: Usimamizi na Uimarishaji wa Vyama vya Ushirika.**

**52. Mheshimiwa Spika;** Programu hii ina lengo la kusimamia Mageuzi ya Mfumo wa Vyama vya Ushirikaili viwe imara, endelevu, vinavyoendeshwa kiujasiriamali na vinavyokidhi mahitaji ya wanachama, kiuchumi na kijamii. Pia, inachangia kukuza ajira na pato la Taifa. Kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Programu ilikadiriwa matumizi ya kiasi cha Shilingi Milioni Mia Nne na Kumi (TSh.410,000,000) hadi mwezi Machi, 2023 imepatiwa matumizi ya kiasi cha Shilingi Milioni Mia Nnena Tisa, Laki Nane Thamanini na Saba na Shilingi Moja (TSh.409,887,001) (Matumizi ya Kawaida 77,305,751na Mishahara 332,581,250) sawa na asilimia 100 ya makadirio. Programu kwa kipindi cha Julai, 2022- Machi, 2023 ilitekeleza yafuatayo:-

1. Imesajili vyama vya ushirika 1,822 (Unguja 1,036na Pemba 786); kati ya hivyo SACCOS 2 na vyama

vya uzalishaji na utoaji huduma 1,820. Lengo ni kusajili vyama 303, ongezeko hili ni mara sita ya lengo lililopangwa. Hii ni kutokana na kuwepo kwa fursa za mikopo ya UVIKO 19 inayotolewa kupitia vyama vya ushirika. Shughuli za vyama vilivyosajiliwa zilikua ni Biashara ndogo ndogo, ufugaji wa ngo'mbe, kuku, uuzaji wa mbao, biashara ya duka, upambaji na uchoraji, uchongaji, kudarizi, uvuvi, kilimo mchanganyiko na ufundi gereji.

2. Aidha, kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 jumla ya SACCOS 15 na Kampuni 2 za Bima ambazo zinatoa huduma za Bima kwenye vyama vya ushirika zimekata leseni na harakati za kusajili chama kikuu mwanvuli cha uvuvi zinaendelea.

3. Imekagua hesabu za Vyama vya Ushirika 390 (Unguja 81 na Pemba 309). Matokeo yameonesha kuwepo kwa changamoto za uhaba wa elimu juu ya uendeshaji na usimamizi, baadhi ya vyama vya uzalishaji haviandai bajeti wala mipango kazi na uhaba wa elimu juu ya usimamizi wa fedha na utunzaji wa kumbukumbu. Kutokana na changamoto hizo, programu imetoa elimu, mafunzo na ushauri juu ya changamoto zilizobainika ili kuimarisha utendaji wa vyama.

4. Imefuatilia uendeshaji wa shughuli za vyama vya ushirika kwenye maeneo ya utunzaji wa vitabu, ufuatwaji wa sheria na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa vyama 292 (Pemba 235 na Unguja 57). Lengo ni kuvifikia vyama 600. Utekelezaji huu ni sawa na asilimia 49. Hii ni kutokana na kuongeza nguvu kwenye usajili wa vyama. Changamoto kuu zilizobainika zilikua ni kutokufuatwa kwa sheria ndogo (By - laws),

kutoitishwa mikutano kwa utaratibu, elimu ndogo juu ya uendeshaji wa vyama kwa viongozi na mitaji midogo ya vyama. Idara inazifanyia kazi changamoto hizo.

5. Imetoa mafunzo ya dhana ya ushirika, muundo, uendeshaji, uongozi na utawala bora kwenye vyama vya ushirika, Ujasiriamali, ufafanuzi wa Sera, Sheria na kanuni za Ushirika pamoja na Utunzaji wa kumbu kumbu na miamala ya fedha kwenye madaftari kwa washiriki 3,861 (Wanawake 1,900; Wanaume 1,961) kutoka vyama 1,893 (Unguja 1,047 na Pemba 839) walipatiwa mafunzo hayo. Lengo ilikua ni kuwafikia wanachama na viongozi 3,000, kiwango cha utekelezaji ni asilimia 129%.

6. Imeandaa vipindi vitatu (2 ZBC redio na 1 ZBCTV) vilivyoeleza mafanikio ya awamu ya nane ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na ufafanuzi wa ukomo wa madeni kwa vyama vinavyopata mikopo kutoka Taasisi za fedha.

7. Kwa kushirikiana na wadau wengine ambao ni Kampuni ya Bima (NIC), Benki ya CRDB, Chuo kikuu cha Ushirika Moshi, ilitoa mafunzo ya ujasiriamali, usimamizi wa fedha, masoko, umuhimu wa bima kwenye vyama vya ushirika na umuhimu wa elimu na Taaluma kwa vyama vya ushirika kwa wanachama381 (Wanawake 202 na Wanaume 179) kutoka vyamavya ushirika 60. Mafunzo haya yaliongeza uelewa wakuwa na bima kwenye vyama vyao.

8. Imeratibu ziara tatu za mafunzo ambapo Hai Rural Teacher SACCOS kutoka Mkoa wa Kilimanjaro walitembelea Vyama viwili ambavyo ni Furahia Wanawake na Mtule AMCOS kwa Zanzibar na Makuli SACCOS Zanzibar walitembelea Bandari SACCOS ya Dar-es-Salaam na Maafisa wawili wa Ushirika wanaotekeleza mradi wa Youth Living Coastal Area (YLCA) walitembelea Wilaya ya Korogwe na Handeni Mkoa wa Tanga kwa lengo la kubadilishana uzoefu wa kiutendaji, mbinu za kujenga uwezo wa kuwawezesha Vijana katika kazi zao pamoja na mahusiano mema baina ya vyama vya ushirika vya Tanzania Bara na Zanzibar.

9. Imesimamia uendeshaji wa mafunzo kwa wanachama 288 (Wanawake 154 na Wanaume 134) na Mabaraza 11 ya wanaushirika katika Wilaya zote za Unguja na Pemba.

10. Imeadhimisha Siku ya Ushirika Duniani, kilele cha maadhimisho hayo kilifanyika tarehe 2/07/2022. Uwanja wa Gombani Wilaya ya Chake Chake Mkoa wa Kusini Pemba. Maadhimisho hayo yaliambatana na shughuli za kufanya usafi katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba, kongamano la wanaushirika na ziara za mafunzo. Ujumbe ulikua ni "Ushirika Kujenga Dunia iliyo Bora".

11. Imeviunganisha vyama vya Ushirika 590 (Unguja 574 na Pemba 16) kwenye Taasisi za Fedha ambazo ni Benki ya CRDB, Benki ya PBZ na Benki ya Equity kwa lengo la kuwawezesha kufungua akaunti za ushirika katika Benki hizo ili kurahisisha upatikanaji wa mikopo pia kuwa na uhifadhi wa fedha za wanachama.

12. Imesimamia Mikutano 15 ya vyama vya ushirika iliyodhinisha Bajeti na Mipango kazi, kusimamia uchaguzi wa viongozi wao, kuthibitisha wanachama wapya na kuwatoa wanachama waliokosa sifa, kuwahamasisha wanachama kuchangamkia fursa za mkopo zilizopo Nchini ili kuimarisha mitaji yao.

13. Imeshiriki kutatua migogoro iliyojitokeza katika vyama vitatu vya ushirika, vyama vyenyewe ni Bandari Tax SACCOS, Blue Cooperative na Nahusika Cooperatives. Aidha Vyanzo vya Migogoro hiyo ni ukiukwaji wa sheria ndogo ndogo zinazoongoza vyama vyao. Migogoro hiyo imesuluhishwa na vyama husika vinaendelea na shughuli zao.

14. Imeratibu ushiriki wa maonesho mawili ya Biashara yaliyofanyika Viwanja vya Maisara na Tamasha la Kizimkazi yaliyofanyika Wilaya ya Kusini Unguja kwa washiriki 24 (Wanawake 22 na Wanaume 2) kutoka vyama vya ushirika 12.

15. Imeandaa mikataba miwili ya mashirikiano (MoU) kati ya Chuo kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU) na Tume ya Ushirika Tanzania Bara (TCDC). Mkataba na MoCU umeshasainiwa na unaendelea kufanyiwa kazi, aidha rasimu ya mkataba na TCDC umeshapelekwa katika Ofisi zao zilizopo Dodoma kwa hatua za ukamilishaji na kutiwa saini. Lengo la Mikataba hiyo ni kuimarisha mashirikiano mazuri ya kiutendaji kati ya Idara na Taasisi hizo ili kuchochea mabadiliko na maendeleo endelevu ya sekta ya ushirika Nchini.

16. Imekamilisha zoezi la uhakiki wa vyama vya ushirika, wenye lengo la kupata taarifa za Vyama vya Ushirika, idadi yake, wanachama waliopo, thamani ya mitaji, mahitaji ya mafunzo, madaraja stahiki ya vyama hivyo na ajira binafsi zilizopo. Matokeo ni kwamba zoezi limefikia katika hatua za mwisho na ripoti itapatikana katika robo ya Aprili – Juni, 2023.

**53. Mheshimiwa Spika,** Programu kwa mwaka wa fedha 2023/24, imepanga kutekeleza yafuatayo:-

1. Kusajili vyama vya ushirika 600;
2. Kufanya ukaguzi wa hesabu za vyama vya ushirika 550 na ukaguzi wa kawaida kwa vyama 600;
3. Kuandaa Mpango wa Mafunzo kwa vyama vya ushirika pamoja na Miongozo yake na Vitini vya kufundishia;
4. Kutoa mafunzo kwa wanachama na Viongozi 3,000;
5. Kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa Wafanyakazi 10;
6. Kutoa Mafunzo ya ndani kwa Maafisa Ushirika na Maafisa Ushirika wakaguzi 40 Unguja na Pemba.

**54. Mheshimiwa Spika;** Ili Programu ndogo ya Usimamizi na Uimarishaji wa Vyama vya Ushirika iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2023/2024, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya Shilingi Milioni Mia Nane Sabini na Tatu, Mia Tatu Sabini na Nne Elfu (Tsh.873,374,000) (Matumizi ya kawaida 391,000,000 na Mishahara 482,374,000).

### 6.2.3. Programu Ndogo SA070303: Uratibu na Uendelezaji wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

55. **Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo (SA070303) ina lengo la kukuza Hadhi ya kiuchumi kwa Vijana, Wanawake, Watu Wazima na makundi maalum katika jamii na ina jukumu la kubuni na kuratibu Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Programu inasimamia uendeshaji wa Kituo cha Kulea na Kukuza Wajasiriamali kilichopo Mbweni; Kituo cha Wanawake cha Kutengeneza Vifaa vya Umeme wa Jua kilichopo Kinyasini na Vituo viwili vya usarifu wa Asali kimoja kipo Kizimbani - Unguja na kimoja kipo Pujini - Pemba.

56. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Programu ilikadiriwa matumizi ya kiasi cha Shilingi Milioni Mia Tatu Thamanini na Sita (TSh.386,000,000) kwa matumizi mengineyo; hadi kufikia mwezi Machi, 2023 imepatiwa matumizi ya kiasi cha Shilingi Milioni Mia Tatu Thalathini na Sita, Laki Tano, Mia Tatu Thalathini na Sita (TSh.336,500,336) (Matumizi ya Kawaida 146,472,986 na Mishahara 190,027,350) sawa na asilimia 87.2 kwa matumizi mengineyo. Aidha, iliidhinishiwa kiasi cha Shilingi Bilioni Kumi na Tisa na Milioni Mia Tano (19,500,000,000) kwa Miradi ya Maendeleo ambapo bado Afisi hazijaingiziwa fedha hizo. Programu hii kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 imetekeleza yafuatayo:-

1. Kupitia Kituo cha Kulea na Kukuza Wajasiriamali imetoa mafunzo ya aina mbali mbali kwa wananchi 119 (Wanaume 14 na Wanawake 105) katika fani ya matunda na mboga mboga; Uokaji na mafunzo elekezi kwa wajasiriamali.

2. Kituo cha Wanawake cha Kutengeneza vifaa vya Umeme wa Jua kimetoa mafunzo kwa Wafugaji wa Nyuki na Umeme wa jua 46 (Wanawake 40 na Wanaume 6). Pia, kimetekeleza yafuatayo:-

    i. Kimepokea vifaa vya umeme wa jua kutoka Barefoot College Interantional kwa ajili ya kupatiwa Solar Mama ambao walipatiwa mafunzo kwa ajili ya kuvifanyia kazi katika vijiji vyao.

    ii. Kimegawa vifaa vya ufugaji nyuki kwa wafugaji 28 wa Pele Tumbatu, ambavyo vilidhaminiwa kutoka Kijiji cha Watoto SOS na kufanya ufuatiliaji kwa wafugaji waliopatiwa vifaa hivyo.

    iii. Kilitafuta fursa za masoko kwa mazao yanayozalishwa Barefoot College ikiwemo Asali kwa kuipeleka Villa Maua Matemwe, na katika maonesho ya 9 ya Biashara yaliyofanyika Maisara, Zanzibar.

3. Pia, Programu imetoa mafunzo kwa wananchi 386 (Wanawake 318 na Wanaume 68) Unguja katika fani za utafutaji wa masoko ndani na nje ya nchi, namna bora ya kuendesha na kukuza bidhaa zao, E - marketing na stadi za maisha, fursa zinazotolewa na Wakala, ujasiriamali katika fani zinazohusiana na Technolojia ya Habari na fursa za ajira katika Sekta ya Ujasiriamali. Aidha, iliwapa mafunzo Wajasiriamali 491 (wanawake 325 na wanaume 166) Pemba katika fani za ujasiriamali, ushoni, kilimo, biashara, uwekaji wa kumbu kumbu, masoko, upatikanaji wa mitaki na mikopo, viwango na nembo ya ubora.

4. Imeratibu utekelezaji wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kupitia Asasi za kiraia na imeanza kupokea taarifa za utekelezaji wa kazi zao ambapo hadi sasa imepokea taarifa kutoka Asasi 3 zinazoonesha jumla ya wananchi 308 (Wanawake 223 na Wanaume 85) waliowezeshwa kwa njia ya mafunzo mbali mbali kwa kipindi cha mwaka 2022/2023 yakiwemo Uandishi wa katiba za Vikundi na Mafunzo ya Kibiashara, Stadi za Maisha na Ujasiriamali na Utengezaji wa Sabuni.

5. Kupitia Fedha za Ahueni ya Uviko 19, Wakala umenunua vifaa vya ufugaji wa nyuki na kugaiwa katika vikundi 34 vya wajasiriamali waliopatiwa mafunzo na makabidhiano rasmi ya vifaa hivyo kwa Wakuu wa Mikoa yalifanywa na Makamu wa Pili wa Rais Mheshimiwa. Hemed S. Abdulla, Makamo wa Pili wa Rais, tarehe 27/12/2022 katika Ukumbi wa Mhe. Idrissa Abdulwakil - Kikwajuni. Vifaa hivyo vimetolewa kwa njia ya mikopo ambapo kila mhusika atalipa mkopo huo kupitia uuzaji wa mazao ya asali atakayovuna kupitia kikundi chake. Aidha, imeweza kuzindua Vituo vya kuchakata asali, 1 Kizimbani - Unguja na 1 Pujini - Pemba vilivyojengwa kupitia mradi huo.

6. Imefanya ziara mbali mbali za ufuatiliaji wa wajasiriamali ili kuona maendeleo na changamoto zao. Ziara hizo ni kama ifuatavyo:-

   i. Ziara za tathmini ya mahitaji ya umeme wa jua kwa vijiji vilivyounganishwa na visivyounganishwa na umeme wa jua ili kuweza kuimarisha utoaji wa huduma ya umeme huo vijijini. Tathmini hiyo imeonesha kuwa vijiji 2 kati ya 12 havihitaji tena

umeme wa jua baada ya kufikiwa kikamilifu na huduma ya umeme wa ZECO. Vijiji hivyo ni Bambi, kwa Unguja na kijiji cha Mkia wa Ng'ombe.

ii. Ziara ya ufuatiliaji ya kina mama waliopatiwa vifaa vya ufugaji wa nyuki katika vijiji vya Makoongwe na Kandwi Kusini na imeonekana kuwa kunachangamoto ya uwepo wa maua kutokana na hali ya jua kali linaloendelea.

iii. Ilifanya zoezi la tathmini ya vikundi vilivyopatiwa mafunzo ya Ufugaji wa nyuki (kupitia Mradi wa Uviko 19) na imegundulika kwamba baadhi ya wafugaji wa nyuki (200) wanahitaji kupatiwa taaluma ya ziada ya vitendo ili waweze kufanya kazi hiyo kwa ufanisi zaidi.

iv. Imefanya ufuatiliaji na tathmini ya vikundi 36vya Wilaya nne (4) za Pemba vyenye idadi ya wanachama 213 vilivyopatiwa mikopo ya INUKA Tathmini inaonesha kuwa kuna baadhi ya vikundi vinaendelea vizuri kwa kuimarisha shughuli zao na kuongeza uzalishaji na viko ambavyo vinakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo ukosefu wa soko la uhakika, uhaba wa taaluma kwa shughuli wanazozifanya, kukosa alama za ubora katika bidhaa zao na fedha walizopatiwa hazikutosheleza kufikia malengo yao.

7. Imeendelea kushajiisha Vyuo vikuu kuingiza somo la ujasiriamali katika Mitaala yao. Vyuo hivyo ni Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume pamoja na Chuo Kikuu cha Zanzibar (Z.U). Wakala ilikubaliana na wawakilishi wa vyuo hivyo kutengeneza hadidu rejea ya kuanzisha Kamati ya kusimamia suala hilo.

8. Imesaidia Wajasiriamali 77 kuwaunganisha na fursa za masoko kwa bidhaa zao Unguja ambapo Wajasiriamali 22 (Wanawake 15 na Wanaume 2) walishiriki maonesho ya Jua Kali nchini Uganda, Wajasiriamali 10 (Wanawake 7 na Wanaume 3) walishiriki maonesho ya 9 ya biashara -Maisara, na Wajasiriamali 45 (Wanawake 43 na Wanaume2) walishiriki maonesho ya maadhimisho ya sikuya Mwanamke Duniani yaliyofanyika viwanja vya Mapinduzi Squre na Pemba, wajasiriamali 144, ambapo Wajasiriamali 71 (32 Wanawake na 39 Wanaume) walishiriki maonesho ya chakula na Wajasiriamali 73 wanawake walishiriki katika Kongamano.
9. Imeratibu usimamizi wa Miradi ya Maendeleo ya Ujenzi wa Vituo vya Kulea na Kukuza Wajasiriamali Kizimbani Unguja na Pujini Pemba ambapo ujenzi huu upo katika hatua ya Zabuni ya kumtafuta Mkandarasi wa kuandaa Michoro na Makisio. Pia, inaendelea kuratibu Ujenzi wa Vituo 3 vya Huduma za Kibiashara na Ujasiriamali ambavyo vinatarajiwa kujengwa Tumbe Mashariki, Kiongole na Kusini Unguja navyo vipo katika hatua ya kumpata Mkandarasi.

**57. Mheshimiwa Spika,** Pia, Programu imeimarisha utendaji wa kazi zake kwa kufanya yafuatayo:-

1. Kutangaza huduma zake za Uwezeshaji ikiwemo; muenendo wa utoaji wa Mikopo kwa Wajasiriamali na Wafanyabiashara na kuvitangaza vituo vya mafunzo kupitia Vipindi vya Televisheni na Redio, zikiwemo FM redio, Bahari FM, Spice FM, ZBC na Assalamu pamoja na Mitandao ya Kijamii.

2. Kuingia makubaliano (MoU) na "Barefoot International" kwa ajili ya uendeshaji wa Kituo cha Wanawake cha Mafunzo ya umeme wa jua. Aidha, imeingia Makubaliano ya pamoja na SMIDA na Equity Bank kwa ajili ya usimamizi wa fedha za mkopo Khalifa Fund.
3. Kuzindua Bodi ya Wakurugenzi ambayo imeundwa kwa mujibu wa kifungu cha 8 cha Sheria namba 2 ya mwaka 2022 ya Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Bodi hii inasimamia Wakala katika kazi zake ili iweze kuleta mafanikio yaliyokusudiwa. Aidha, imefanya vikao viwili vya Bodi hiyo na kutoa maelekezo mbali mbali ya kufanyiwa kazi ikiwemo; uimarishaji wa Muongozo wa Utoaji wa Mafunzo kwa Wajasiriamali.
4. Kuandika maandiko ya miradi na inaendelea na mazungumzo na Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya kusaidia miradi ya uwezeshaji, ikiwemo; USAID kwa mradi wa Inua Vijana, Tanzania Association of Microfinance Institutions (TAMFI) kwa mradi wa Uwezeshaji katika eneo la Maji safi, Taka na Nishati jadidifu, Youth Challenge International (YCI) kwa mradi wa kuinua Vijana Wanawake.

**58. Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Programu imejipanga kutekeleza yafuatayo:-

1. Kuendelea kutoa Mafunzo kwa Wajasiriamali kulingana na mahitaji (ZTBI 200, Barefoot 30, Vituo vya Asali 200);

2. Kuratibu usimamizi wa vituo vya kulea na kukuza Wajasiriamali, Barefoot na Vituo vya kusarifu asali;
3. Kufanya ufuatiliaji kwa wanufaika wa Mafunzo;
4. Kutoa Mafunzo kwa Wajasiriamali;
5. Kuandaa na kutekeleza Miradi 3 ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;
6. Kuratibu Taasisi zinazotoa huduma za Ujasiriamali na Uwezeshaji;
7. Kuwaunganisha Wajasiriamali 350 (250 Ungunja na 150 Pemba) na Taasisi za viwango;
8. Kuwaunganisha Wajasiriamali 350 (250 Ungunja na 150 Pemba) na fursa za masoko;
9. Kufanya Tamasha la maonesho la Wajasiriamali.

**59. Mheshimiwa Spika;** Ili Programu ndogo (SA070303) ya Uratibu na Uendelezaji wa Program za Wananchi Kiuchumi iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2023/2024, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya Shilingi Milioni Mia Nane Sabini na Nane, Arobaini na Nane Elfu (Tshs.878,048,000) (Matumizi ya kawaida 600,000,000 na Mishahara 278,048,000).

## 6.3 PROGRAMU KUU PA0703: UENDESHAJI NA URATIBU WA AFISIYA RAIS,KAZI,UCHUMINAUWEKEZAJI.

**Matokeo ya Muda Mrefu:** Kukuza Uwezo wa Afisi kutekeleza majukumu yake katika masuala ya Kazi, Uchumi na Uwekezaji.

**60. Mheshimiwa Spika,** Programu hii Kuu kwa kipindicha Julai 2022 hadi Machi 2023 cha mwaka wa Fedha 2022/2023, ilikadiriwa matumizi ya kiasi cha Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Tisa Thalathini na Tano, Laki Nane Elfu Nne, Mia Tano Sabini na Tano (Tsh.2,935,804,575) mpaka kufika mwezi Machi, 2023 imeidhinishiwa matumizi ya kiasi cha Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tisa Thalathini na Tano, Laki Moja Hamsini na Sita, Mia Nane Hamsini na Tatu (TSh.1,935,156,853) (Matumizi ya kawaida 670,187,663 na Mishahara 1,264,969,190) sawa na asilimia 65.9 ya utekelezaji programu zake ndogo.

### 6.3.1 Programu ndogo SA070301: Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Afisi.

**Lengo:** Kuratibu uandaaji na utekelezaji wa Sera, Sheria, Mipango, Bajeti, Tafiti na Mashirikiano ya Afisi na Taasisi nyengine ndani na nje ya nchi.

**61. Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo SA070301 ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Afisi inaratibu Uandaaji na Utekelezaji wa Sheria za Kazi, Upatikanaji wa Ajira za Staha na Uwekezaji na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Programu kwa robo tatu (Julai, 2022 – Machi, 2023) ilikadiriwa matumizi ya Shilingi Milioni Mia Nne na Sitini, Laki Nane Arobaini na Sita, Laki Tatu na Sitini (TSh.460,846,360) na imeingiziwa jumla ya Shilingi

Milioni Mia Mbili Sitini na Nane, Laki Saba Kumi na Saba, Mia Nne Hamsini na Sita (TSh.268,717,456) (Matumizi ya kawaida 71,717,411 na Mishahara 197,000,045) sawa na asilimia 58.3 ya makadirio.

62. **Mheshimiwa Spika,** Programu kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023), imetekeleza shughuli zifuatazo:

1. Imekamilisha mapitio ya Sera ya Ajira ya mwaka 2009 na kuanza mchakato wa kuandaa Rasimu ya Sera mpya ya Ajira 2023 ambapo Rasimu ya awali iko tayari kwa kuwasilishwa kwa wadau wa taasisi mbali mbali kuiimarisha ikiwemo taasisi ya UTATU ili kuweza kupata maoni yao ambayo yatasaidia katika kuimarisha rasimu hiyo. Sera hiyo imefanyiwa marekebisho kutokana na kuwa ni ya muda mrefu na mabadiliko ya kiuchumi na kijamii yanayotokea kitaifa, kikanda na kimataifa ikiwemo Malengo Endelevu ya Maendeleo (Agenda 2030), Agenda 2063, Dira 2050, Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar 2021-2026 na Ilani ya Uchaguzi 2020 – 2025.

2. Inaendelea kuratibu mchakato wa kuifanyia marekebisho Sheria ya Ajira nambari 11 ya mwaka 2005 baada ya kupata maoni ya Tume ya Kurekebisha Sheria na baadhi ya wadau pamoja na kuangalia changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa Sheria hiyo. Maeneo yaliyozingatiwa katika Mswada wa Sheria ni pamoja na kuongeza muda wa vibali vya kazi kwa miaka miwili iendane na vibali vya ukaazi; kuwatambua na kuwawekea utaratibu wanafunzi wanaofanya mazoezi ya kazi; zimeanzishwa adhabu za papo kwa papo; Diaspora kupewa hadhi ya kutambuliwa na kutolipa vibali vya kazi na mabadiliko

ya malipo ya vibali vya kazi kutoka dola za kimarekani 300 hadi 1,000 na kupunguza malipo ya vibali kwa wanafunzi kutoka dola za kimarekani 300 hadi 100. Mswada unapelekwa katika Bodi ya Ushauri wa Masuala ya Kazi ili kuipitia na kupata maoni na hatimae kuwasilishwa katika ngazi za maamuzi.

3. Inaendelea kuratibu mchakato wa kuandaa Kanuni za utekelezaji wa Sheria za Kazi ambapo rasimuza Kanuni 4 zimeshatayarishwa ikiwemo kanuni ya Utaratibu wa Wanafunzi wanaofanya mazoezi yakazi; kanuni ya adhabu za papo kwa papo na kanuni Mzanzibari anaeoa au kuolewa na Mgeni kufanya kazi bila ya kulipa. Pia, Kanuni 3 za Usalama na Afya Kazini (Kanuni Kiongozi, Kanuni ya Huduma ya Mwanzo na Kanuni ya kutoa taarifa ya ajali na maradhi katika sehemu za Kazi) zinaendelea kuandaliwa.

4. Imeandaa Wasifu wa Miradi ya Afisi (Project Profile) kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Afisi. Jumla ya maandiko ya miradi 17 yameandaliwa na kuanza kuwasilishwa Tume ya Mipango kwa hatua ya kupatiwa fedha za utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Miradi hiyo ni pamoja na Mradi wa Kuziwezesha familia ili kuondosha ajira za Watoto, Kutengeneza makaa kwa kutumia takataka, kuanzisha kiwanda cha vifungashio, kujenga kituo cha kuchunguza na kutibu magonjwa yatokanayo na kazi, kujenga vituo vya kulea na kukuza wajasiriamali, vituo vya hudumaza biashara na kuimarisha mfumo wa takwimu na taarifa za ajira nchini.

5. Imeratibu ukamilishaji wa Ujenzi wa Vituo vya uzalishaji wa bidhaa zinazotokana na mazao ya nyuki. Vituo hivyo vimejengwa katika kijiji cha Kizimbani - Unguja na Pujini - Pemba ambavyo pamoja na mambo mengine vitatumika kuzalisha bidhaa zinazotokana na nyuki, kutoa mafunzo ya ufugaji wa kisasa wenye tija kwa wafugaji nyuki, kusimamia ubora wa bidhaa za mazao ya nyuki ikiwemo mnyororo wa thamani.

6. Imekamilisha uandaaji wa Agenda za Utafiti za Afisi ambapo Agenda hizo zimeshapitiwa katika Kamati ya Uongozi na tafiti zilizoainishwa zimeanza kutekelezwa na zimeainishwa katika Mpango Kazi wa mwaka wa fedha 2023/2024.

7. Programu kwa kushirikiana na Idara ya Ushirika na Kamati ya Wataalamu inaendelea na kazi ya kuandaa muongozo wa mageuzi ya sekta ya Ushirika Zanzibar ili iweze kuimarisha ufanisi na uzalishaji wa Vyama vya Ushirika. Tayari Kamati imewasilisha taarifa ya awali (Inception report) ya tathmini ya mageuzi ya sekta ya Ushirika Zanzibar. Pia, imekamilisha zoezi la tathmini ya vyama vya ushirika.

8. Imefanya Tathmini ya Programu ya Mafunzo ya muda mfupi katika Skuli za Ufundi na Vyuo vya Elimu ya Amali kwa Vijana wasio na ajira, wasio katika Elimu na wasio katika mafunzo ya aina yoyote (NEET) kwa mwaka 2021 na 2022. Tathmini imejumuisha Wanafunzi kutoka Wilaya zote 11 za Unguja na Pemba. Jumla ya Vijana 82 (Wanawake 34 sawa na 41.4% na Wanaume 48 sawa na 58.54%) (26 waliomaliza 2021 na 56 waliomaliza 2022) wamefanyiwa tathmini. Asilimia 98 ya wanafunzi waliohojiwa wameonesha

kunufaika na mafunzo yaliyotolewa kupitia Program ya 'NEET', ambapo asilimia 24 wamejiajiri, asilimia 27 wameongeza ujuzi, asilimia 23 wameweza kujiongezea kipato na asilimia 24 wamepata taaluma za nadharia ya ufundi na ujasiriamali. Pia, tathmini hiyo pamoja na mambo mengine, imebaini kuwa asilimia 96.34% ya wahojiwa wote ni wanafunzi waliomaliza elimu ya sekondari, hii inaonesha uwepo wa wimbi kubwa la Vijana ambao hawajapata mafunzo au ujuzi wowote na wanahitaji kufaidika na programu hii.

9. Imeandaa Muhtasari (policy brief) wa Utafiti wa Kuwatambua na Kuwawezesha Vijana Nguvu kazi Zanzibar uliofanyika mwaka 2018. Muhtasari huu pamoja na mambo mengine umeainisha aina ya nguvu kazi na sehemu ilipo, mikakati ya kuwawezesha Vijana wa Zanzibar pamoja na fursa za ajira zilizopo. Mikakati hiyo ni pamoja na kuimarisha Mitaala ya Vyuo vya Amali ili iweze kwenda sambamba na soko la Ajira la ndani na nje ya nchi kwa kuweka miundombinu bora na vifaa kwa Vijana kuweza kukuza na kuendeleza ujuzi wao ili waweze kujitegemea. Pia, Kuweka somo la Ujasiriamali maskulini na katika Vyuo Vikuu, kuongeza Miradi na Programu za kukuza ujuzi hasa kwa Vijana, pamoja na kuwaunganisha vijana na fursa mbali mbali ikiwemo mikopo, mafunzo, masoko, ubunifu na fursa za ajira katika sekta ya kilimo, utalii na uvuvi.

10. Imekamilisha uandaaji wa Mpango Mkakati wa Afisi kutokana na Mabadiliko mbali mbali yaliyotokea na mabadiliko ya Muongozo wa utayarishaji Mpango Mkakati kutoka Tume ya Mipango.

11. Imeratibu utayarishaji wa ripoti mbalimbali za utekelezaji zikiwemo, ripoti ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020 – 2025, ripoti zilizowasilishwa katika Kamati mbali mbali za Baraza la Wawakilishi, ripoti ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (2021-2026), ripoti ya Ufuatiliaji wa vipaumbele vya Mheshimiwa Rais (PDB) na ripoti maalum zilizohitajika kwa vipindi tofauti zinazohusiana na utekelezaji wa shughuli za Afisi katika taasisi mbali mbali.

12. Imelipia gharama za safari za ndani ya nchi kwa wafanyakazi 5 (Wanaume 2 na Wanawake 3) walioshiriki katika vikao na shughuli za Afisi zinazohusiana na masuala ya Kazi na Uwezeshaji Pemba, Dar es Salam na Dodoma.

13. Inaendelea kuelimisha jamii kupitia Vyombo vya Habari (Redio, Televisheni, Magazeti, Facebook, Twitter na Tovuti ya Afisi) nchini kuhusiana na utekelezaji wa shughuli za Afisi, imeandaa na kurushwa hewani habari Themanini (80), vipindi Kumi na Tano (15) vimerushwa hewani kupitia Televisheni na Redio; Makala Nane (8) na Stori 19 zimeandaliwa. Vipeperushi Thelathini (30) vimeandaliwa na kutumwa katika mitandao ya kijamii ya Afisi. Pia, imeunda na imezindua Kamati ya Uhariri wa taarifa na habari za Afisi.

14. Aidha, imeanzisha Mfumo wa Kielektroniki wa kusajili Wafanyakazi na kuimarisha Tovuti ya Afisi pamoja na kuimarisha upatikanaji wa huduma za 'internet' kuimarisha ufanisi wa utendaji wa kazi za Afisi, Mfumo wa E - Office na Manunuzi.

15. Imefanya Mapitio ya Mfumo wa Taarifa za Ajira (Labour Management Information System) ili uweze kuratibu upatiakanaji wa takwimu za Ajira zinazozalishwa katika Sekta Binafsi na Sekta ya Umma pamoja na Sekta isiyo rasmi, kuzitambua fursa za ajira ndani na nje ya nchi pamoja na kuwaunganisha Vijana kuzitumia fursa hizo, kuwatambua wahitimu wa vyuo na kada zao kwa ajili ya kurahisisha soko la ajira nchini hasa katika miradi mbali mbali ya kimkakati na uwekezaji. Aidha, kwa kushirikiana na Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali na Tawala za Mikoa, imeandaa nyenzo za kukusanya takwimu za Ajira kupitia Wilayani.

16. Imekamilisha uandaaji wa Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Afisi kwa kuainisha shabaha na viashiria vya utekelezaji vitavyosaidia kupima utekelezaji wa Programu na Miradi ya Afisi.

17. Imefanya Ufuatiliaji kwa vikundi 12 vya wanufaika wa Mikopo ya Fedha za Ahueni ya Uviko 19 kupitia Benki ya CRDB katika Wilaya ya Kusini na Kati katika Shehia ya Kitogani, Kibuteni, Kijini, Charawe, Ndijani Mseweni na Chwaka na Wilaya ya Kaskazini A na Kaskazini B katika Shehia ya Chaani Kubwa, Chutama, Mahonda, Mkokotoni na Fujoni ambapo matokeo ya Ufuatiliaji huo yameonesha kuwa asilimia 86 ya vikundi hivyo vinaendesha vizuri shughuli zao kutokana mikopo hiyo. Asilimia 90 ya vikundi hivyo vimesharejesha mikopo yao kwa awamu 9 katika awamu 12. Pia, Kikundi cha Kitogani cha Wakulima wa Mboga mboga kimeajiri Vijana 2 wa kiume kuwasaidia katika shughuli zao za kilimo. Mbali na mafanikio hayo, ufuatiliaji umegundua baadhi ya changamoto wanazokabiliana

nazo ambazo zimepelekea kuzorota kwa Shughuli zao za uzalishaji zikiwemo kutokufikiwa na Umeme wa Gridi ya Taifa katika maeneo ya Kilimo Kitogani, ukosefu wa maji na uwepo wa wadudu waharibifu na jua kali linaloathiri mazao. Mapendekezo na changamoto zilizojitokeza zimewasilishwa katika taasisi husika kwa ajili ya kufanyiwa kazi.

63. **Mheshimiwa Spika,** Programu kwa mwaka wa fedha 2023/24, imepanga kutekeleza yafuatayo:-

1. Kuchapisha Sera ya Ajira;
2. Kufanya mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Ushirika na Sera ya Ajira;
3. Kufanya mapitio ya Sheria ya Ushirika ya mwaka 2018;
4. Kuandaa Sera ya 'Local Content";
5. Kuandaa Sera ya TEHAMA ya Afisi;
6. Kufanya tafiti 2 (Masoko ya Wajasiriamali na Ajira katika Sekta Binafsi) kwa mujibu wa Agenda za Utafiti;
7. Kuratibu utekelezaji wa Programu na Miradi ya Afisi;
8. Kufanya ufuatiliaji na tathmini wa shughuli za Afisi;
9. Kuratibu uandaaji wa ripoti (Ilani, PDB, Hotuba, PBB, MTEF) mbali mbali kwa mujibu wa mahitaji;
10. Kuimarisha upatikanaji wa takwimu za shughuli mbali mbali za Afisi na Kuimarisha Mashirikiano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa.

64. **Mheshimiwa Spika,** Ili Programu ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2023/24, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya Shilingi Milioni Mia Nne Thamanini na Tisa, Laki Nne Hamsini na Nne Elfu (Tshs.489,454,000) (Matumizi ya kawaida 235,150,000 na Mishahara 254,304,000).

### 6.3.2 Programu Ndogo SA070502: Utawala na Uendeshaji.

65. **Mheshimiwa Spika;** Programu ya Utawala na Uendeshaji ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Uendeshaji na Utumishi na kukuza uwezo wa Afisi kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Programu iliidhinishiwa Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Mbili Sitini na Nane, Laki Tisa Sabini na Tisa, Mia Sita Arobaini (Tsh.1,268,979,640) hadi kufika Machi 2023 iliingiziwa matumizi ya Shilingi Milioni Mia Nane Hamsini na Tano, Laki Tisa Sabini na Tatu Elfu, Mia Tano na Saba (855,973,507) (Matumizi ya kawaida 335,724,152 na Mishahara 520,249,355) sawa na asilimia 67.5. Programu kwa mwaka wa fedha 2022/2023, imetekeleza shughuli zifuatazo:-

1. Imesimamia malipo ya Safari 35 za ndani za kikazi kwa Viongozi na Maafisa wa Afisi kwenda Pemba na Dar es salaam, aidha imefanya matengenezo ya gari 7 za Viongozi na Idara pamoja na kusimamia ununuzi wa mafuta kwa ajili ya ufuatiliaji wa kazi mbali mbali. Vile vile, inaendelea kugharamia malipo ya huduma za Umeme, Maji, Magazeti na imefanya matengenezo ya vifaa na miundombinu ya Afisi.
2. Imefanya ununuzi wa vifaa vya kuandikia na thamani.

Pia, imefanya ununuzi wa vifaa vya usafi, ukarabati wa Afisi ikiwemo kuweka taa za kusaidia ulinzi katika uzio wa Jengo la Afisi na imefanya ununuzi wa TV mbili. Aidha, Afisi imenunua viburudishaji kwa ajili ya vikao mbali mbali vya Afisi pamoja na mafunzo.

3. Imelipa jumla ya Shilingi 2,100,000 kwa ajili yaposho la likizo kwa Wafanyakazi 21 (Wanaume 14 na Wanawake 7). Pia, imewapatia ubani wafanyakazi 5 (Wananwake 4 na Mwanamme 1) waliofiwa na baba zao kwa kiasi cha Tsh. 3,000,000 na waliofariki 3 (Wanaume 2 na Mwanamke 1) kwa kiasi cha Tsh. 900,000 malipo hayo yalifanyika kwa mujibu wa taratibu za Utumishi wa Umma.

4. Imewapatia mafunzo ya muda mfupi ya ndani ya nchi ambapo jumla ya wafanyakazi 9 (Wanaume 5 na Wanawake 4), wafanyakazi hao ni Katibu Muhtasi, Afisa IT, Afisa Kumbukumbu, Afisa Utumishi, Afisa Ununuzi, Afisa Habari na Wahasibu. Vile vile, Idara imeweza kuwapatia mafunzo ya ndani kuhusu kanuni na taratibu za Utumishi wa Umma jumla ya Wafanyakazi 100 (35 Wanaume na Wanawake 65).

5. Imesimamia maslahi ya Wafanyakazi ikiwemo mishahara mipya na posho.

6. Imekamilisha Mpango wa Rasilimali Watu wa kipindi cha miaka mitano na imekamilisha mfumo wa Afisi mtandao (E- office na Keywords). Pia, inaendelea na kuboresha Mkataba wa Utoaji Huduma kwa Wateja kwa kukusanya maoni ya wateja wake wanaowahudumikia.

7. Imegharamia vikao 11 vya Bodi ya Zabuni, aidha

kwa kushirikana na Afisi ya msajili wa hazina kutoka Afisi ya Rais, fedha na Mipango ikiwa ni pamoja na kuvitambua vifaa chakavu kwa lengo la kuvifanyia taratibu za kuhaulisha kwa mujibu wa taratibu zilivyo.

8. Imeratibu ushiriki wa Afisi kikamilifu katika maadhimisho ya miaka 59 ya Mapinduzi ya Zanzibar.
9. Imeratibu vikao 11 vya Bodi ya Zabuni na Ukaguzi wa Ndani.
10. Imeratibu Mfumo wa Sema na Rais Mwinyi na kuzifanyia kazi hoja 31 na imefanya mapitio ya Mkataba wa Utoaji wa Huduma kwa Wateja.
11. Imefanikiwa kuazisha jarida la kazi, uwezeshaji na uwekezaji ambalo linatoa taarifa za Afisi za kila kipindi cha miezi mitatu.

**66. Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kupitia Program ya Utawala na Uendeshaji imepanga kutekeleza yafuatayo:-

1. Itaendelea kusimamia Maslahi ya Wafanyakazi kama vile malipo ya mishahara, posho la likizo, malipo ya saa za ziada (50) na malipo ya ubani kwa wafiwa;
2. Itaandaa na kufuatilia malipo ya viinua mgongo kwa Wastaafu 15;
3. Itaendelea kutoa mafunzo ya ndani 200, zoezi la Upimaji Utendaji kazi kwa Wafanyakazi (289) kwa kila mwaka, kuimarisha mazingira ya Afisi nje na ndani;
4. Itafanya mapitio ya Mpango wa Mafunzo na Mpango wa Rasilimali watu;

5. Itasimamia ununuzi wa Genereta la Dharura, pikipiki 2 za maringi matatu kwa ajili ya ufuatiliaji wa shughuli za kila siku.

67. **Mheshimiwa Spika,** ili Program Ndogo ya Utawala na Uendeshaji iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2023/2024, naliomba Barazalako kuidhinisha jumla ya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Thalathini na Tatu, Laki Nane Thamanini na Tatu Elfu (Tshs.1,033,883,000) (Matumizi ya kawaida 417,550,000 na Mishahara 616,333,000).

### 6.3.3 Programu Ndogo SA070503: Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Afisi Pemba.

68. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Afisi Pemba ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Afisi Pemba ambayo inahusisha Idara ya Uendeshaji na Utumishi pamoja na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Programu iliidhinishiwa jumla ya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Mbili na Tano, Laki Tisa Sabini na Nane, Mia Tano Sabini na Tano (Tsh.1,205,978,575) hadi kufika mwezi Machi 2023, iliingiziwa matumizi ya Shilingi Milioni Mia Nane na Kumi, Laki Nne Sitini na Tano Elfu, Mia Nane na Tisini (Tsh.810,465,890) (Matumizi ya kawaida 262,746,100 na Mishahara 547,719,790 ) sawa na asilimia 67.2. Programu kwa kipindi cha miezi tisa (Julai, 2022 – Machi, 2023) imetekeleza yafuatayo:-

1. Imesimamia maslahi ya wafanyakazi kwa kulipa fedha za likizo kwa watendaji 35 (Wanawake 16 na Wanaume 19) na kulipa posho la masaa ya ziada

kwa Wafanyakazi 36 (Wanawake 7na Wanaume 29), kulipia huduma ya mazishi kwa mfanyakazi mmoja aliyefariki dunia, kulipia fedha za ubani wafanyakazi 4 (Wanawake 2 na Wanaume 2) waliofiliwa na watu wao wa karibu na kulipia fedha za matibabu kwa wafanyakazi 2 (Mwanamke 1 na Mwanamme 1).

2. Imelipia gharama za safari za ndani ya nchi kwa wafanyakazi ili kushiriki katika vikao na shughuli mbali mbali za Afisi Unguja na Tanzania Bara. Kadhalika Afisi imewajengea uwezo wafanyakazi 9 (Wanawake 5 na Wanaume 2) kwa mafunzo ya muda mfupi ya kompyuta na utunzaji wa kumbukumbu, wafanyakazi 2 Wanaume katika kada ya udereva na wafanyakazi 2 Wanawake katika mafunzo ya awali (induction course).

3. Imeandaa makala maalum (documentary) kueleza mafanikio waliyoyapata wananchi katika kipindi cha awamu ya nane kupita programu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Pia, imefanya ununuzi wa kompyuta 2, TV 2, friji, seti ya kamera kwa ajili ya waandishi wa habari, zulia, vifaa vya kuandikia, vifaa vya usafi, mafuta, magazeti ya kila siku, kulipia gharama za umeme, maji, simu, pamoja na huduma za mtandao. Pia, imelipia bima vipando 2 na kulipia gharama za matengenezo ya gari, vespa na pikipiki pamoja na kufanya malipo ya huduma za usafi kwa kampuni inayotoa huduma za usafi Afisini.

4. Imefanya ufuatiliaji na tathmini kwa lengo la kuimarisha utendaji wa shughuli za Afisi. Ufuatiliaji huo ulifanyika kwa taasisi binafsi ambazo ziliripotiwa kuwa na kasoro katika ufuataji wa sheria za kazi.

Ufuatiliaji huo ulitoa matokeo mazuri na kujiridhisha kuwa taasisi hizo zimerekebisha kasoro zao na sasa zinafuata kanuni na sheria za kazi ikiwemo sheria ya Ajira na sheria ya Usalama na Afya Kazini.

5. Imefanya ufuatiliaji kwa vyama vya ushirika kuangalia mafanikio na changamoto zinazowakabili. Kiujumla vyama vya ushirika vinaendelea na shughuli zake vizuri licha ya kuweko changamoto katika masuala ya utunzaji wa kumbukumbu na urejeshaji wa mikopo kwa wakati. Pia, kwa baadhi ya vyama, Afisi imegundua kuwa wanachama wanapohama katika vyama hivyo, hawafuati taratibu za ushirika kama zilivyoanishwa katika katiba zao na baadae anarudi kudai haki ambapo hajaitumikia. Hali hii inasababisha migogoro miongoni mwa wanaushirika.

6. Imeratibu na kufuatilia maendeleo ya Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa kufanya ziara maalum iliyofanyika katika Wilaya zote Kisiwani Pemba ili kuangalia mafanikio na changamoto kwa wanufaika wa fedha za IMF ahueni ya UVIKO 19 na wajasiriamali wanaofuga nyuki ambao wamepatiwa vifaa vya kisasa vya ufugaji wa nyuki. Kwa kiasi kikubwa wanufaika wengi wanaendelea na biashara zao vizuri baada ya kupata mafunzo mbambali ya ujasiriamali, utunzaji wa kumbukumbu na elimu ya masoko kupitia Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.
7. Imewapatia wajasiriamali elimu mahsusi kwa mujibu wa sekta zao ili kutatua changamoto mbali mbali zinazowakabili kwa mfano maradhi yanayokabili katika vipando, wadudu na uhaba wa uzalishaji. Kutokana

na mafunzo hayo, wajasiriamali wanaendesha shughuli zao kitaalamu zaidi. Kadhalika, mafunzo hayo yametolewa kwa sekta za ufugaji nyuki na ushoni. Kwa upande wa wajasiriamali wanaofuga nyuki, wajasiriamali wamehamasika katika ufugaji huo, kwani wameonesha nia ya kuondokana na ufugaji wa mazoea nakufuga kisasa kwa ajili ya kupata tija.

8. Imeratibu kikao kimoja kwa ajili ya kujadili hali halisi ya mwenendo wa Mikopo ya Ahuweni ya UVIKO inayotolewa na Benki ya CRDB kwa wajasiriamali wa Pemba. Kikao hichi kiliendeshwa kwa mashirikiano na Afisi za Wakuu wa Mikoa, Wilaya na Benki ya CRDB kwa lengo la kujadili mbinu na mikakati shirikishi itakayosaidia mikopo kutolewa na kurejeshwa kwa wakati ili kuwanufaisha wajasiriamali waliowengi zaidi.
9. Imeratibu kikao kimoja cha siku mbili (2) kwa ajili ya kuwajengea uwezo watendaji katika kuandaa maandiko ya miradi ambapo jumla ya watendaji20 (Wanawake 8 na Wanaume 12) walishiriki. Pia, imeratibu kikao kimoja cha siku mbili kwa ajili ya uandaaji wa bajeti ya mwaka 2023/2024, jumla ya watendaji 20 (Wanawake 7 na Wanaume 13) walishiriki.

10. Imetayarisha ripoti mbalimbali ikiwemo, ripoti ya utekelezaji wa kazi za Afisi, utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya CCM 2020 - 2025 na ripoti maalum kutokana na maagizo ya viongozi. Aidha, kwa kushirikiana na Afisi ya Rais Ikulu imeratibu kikao cha siku moja kwa ajili ya kutoa mafunzo ya mfumo wa Sema na Rais (SNR) kwa ajili ya kuwajengea uwezo

watendaji wetu kuhusiana na mfumo huo. Jumla ya watendaji 27 (Wanawake 11 na Wanaume 16) walishiriki.

11. Imeratibu na kusimamia tathmini kuhusu mchango wa Mfuko wa Uwezeshaji ulivyowanufaisha wajasiriamali wanajishughulisha na mboga mboga na matunda ikiwemo kilimo cha mboga mboga na matunda, uuzaji na usarifu. Tathmini imefanyika kwa Shehia 60 za kisiwa cha Pemba ambapo imewafikia wajasiriamali 240 wanaojishughulisha na kilimo cha mboga mboga na matunda. Tathmini hii hadi kufikia mwezi Machi, 2023 iko katika hatua ya uchambuzi wa taarifa.

69. **Mheshimiwa Spika;** Program kwa mwaka wa fedha 2023/24, imepanga kutekeleza yafuatayo:-

1. Itaendelea kusimamia utekelezaji wa sera, sheriana miongozo mbalimbali ikiwemo maslahi ya wafanyakazi kwa kulipa mishahara kwa wafanyakazi 73, malipo ya safari 40, malipo ya masaa ya ziada kwa wafanyakazi 47, likizo wafanyakazi 40, huduma ya mazishi wafanyakazi 10, matibabu wafanyakazi 5;
2. Itatoa mafunzo ya ndani (Takwimu, Ufuatiliaji na tathmini na Uandishi wa miradi) kwa wafanyakazi 30;
3. Itasimamia mafunzo ya muda mrefu na mfupi wanyakazi 10 na mafunzo ya awali kwa wafanyakazi wapya 15;
4. Italipia gharama za maji, umeme na huduma ya usafi na itafanya manunuzi ya mafuta, vifaa vya kuandikia, vifaa vya usafi, kumpyuta 4, photokopi 2 na kukata bima na kufanya matengenezo vyombo vya usafiri 28

(Gari, pikipiki na vespa);

5. Itafanya tafiti 1 (Ajira za Watoto);
6. Itarusha hewani vipindi 6 na kuandaa makala moja kuhusiana na shughuli za Afisi;
7. Itaandaa taarifa za utekelezaji ikiwemo MTEF 2024-2025, PDB, PBB, Ilani, Hotuba ya Bajeti;
8. Itafanya shughuli za ufuatiliaji na tathmini za Afisi pamoja na kuripoti utekelezaji wake.

70. **Mheshimiwa Spika;** Ili Program ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Afisi Kuu Pemba iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2023/24, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya Shilingi Milioni Mia Tisa Thalathini na Sita na Laki Moja (TSh.936,100,000) (Matumizi ya kawaida 350,000,000 na Mishahara 586,100,000) kwa ajili ya matumizi kazi za kawaida na mishahara.

## 7.0 UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA FUNGU A08 (UCHUMI NA UWEKEZAJI)

### 7.1 PROGRAMU KUU: PA0801 KUIMARISHA UWEKEZAJI NA MASHIRIKIANO BAINA YA SEKTA YA UMMA NA SEKTA BINAFSI

**Matokeo ya muda mrefu:** Usimamizi na Ushajihishaji wa Mali za Umma kwa kuziweka katika Mfumo wa Mashirikiano kwa wote.

71. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii Kuu kwa kipindicha Julai 2022 hadi Machi 2023 cha mwaka wa Fedha 2022/2023 ilikadiriwa kiasi cha Shilingi Bilioni Kumi na

Tatu, Milioni Mia Tano Hamsini na Tisa, Laki Moja Kumi na Moja, Mia Tano Arobaini na Tatu (Tsh.13,859,111,543) mpaka kufikia mwezi Machi, 2023 imeidhinishiwa matumizi ya kiasi cha Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Nane Hamsini na Moja, Laki Nane Ishirini na Sita, Mia Nne Thalathini na Moja (TSh.3,851,826,431) (Matumizi ya kawaida 78,234,000, Mishahara 2,281,310,281 na Maendeleo 1,492,282,150) sawa na asilimia 27.7 ya utekelezaji programu zake ndogo.

### 7.1.1 Programu ndogo SA080101: Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

**72. Mheshimiwa Spika;** Program ya Kuimarisha Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ina lengo la Kukuza, kuratibu na kuimarisha Mashirikiano Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi katika sekta za kiuchumi na kijamii pamoja na kutekeleza miradi mbali mbali ya Maendeleo.

**73. Mheshimiwa Spika;** Kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Programu iliidhinishiwa Shilingi Milioni Mia Nne na Tatu, Laki Moja Arobaini Elfu (Tsh.403,140,000) hadi kufika mwezi Machi 2023, iliingiziwa matumizi ya Shilingi Milioni Mia Moja Sitini na Mbili, Laki Tano Hamsini na Nane, Mia Mbili na Tisini (Tsh.162,558,290) (Matumizi ya lawaida 78,234,000 na Mishahara 84,324,290) sawa na asilimia 40.32. Programu kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imetekeleza shughuli zifuatazo:-

1. Imepitia na kuchambua maombi ya miradi iliyowasilishwa na wawekezaji binafsi. Kwa kipindi cha miezi tisa (9) Kampuni ishirini na mbili (22) kutoka ndani na nje ya nchi ziliwasilisha maombi ya

miradi itakayotekelezwa kwa mfumo wa PPP. Miradi iliyochambuliwa imehusisha Miundombinu, Nishati, sekta ya Afya, Uchumi Buluu, sekta ya huduma za kijamii na sekta ya Kilimo.

2. Inaendelea kufanya mazungumzo na uchambuzi wa kitaalam kwa mradi wa Nyumba ya Kitalii (Domino) na mradi wa ujenzi wa bandari ya abiria katika eneo la Maruhubi ambao kwa sasa wapo katika hatua ya uandaaji wa upembuzi yakinifu kamilifu (Full feasibility study).
3. Imeandaa taarifa za miradi (project profile) ambazo zinatoa taarifa na fursa za miradi ya sekta tofauti ambayo yanahitaji kuwekezwa Zanzibar kwa mujibu wa vipaumbele vilivyoainishwa katika Programu za wizara. Taarifa hizo za miradi zipo katika hatua ya kuandaliwa dhana za miradi na kuziwasilisha kwa wawekezaji.
4. Imeandaa muongozo wa usimamizi wa miradi ya Mashirikiano baina ya Sekta za Umma na Sekta Binafsi, muongozo huo unaonesha utaratibu wa miradi ya PPP ikihusisha uibuwaji hadi utekelezaji wa mradi husika, jambo ambalo litawarahisishia wawekezaji (Private sectors) na Mamlaka za utekelezaji (IA's) utaratibu wa utekelezaji wa miradi ya PPP.
5. Imetoa elimu kupitia vipindi vya redio ya ZBC na televisheni ya Zanzibar kwa lengo la kuwaelimisha wananchi juu ya dhana nzima na utekelezaji wa miradi ya PPP na fursa zinazopatikana kupitia miradi hio.

6. Imeanza maandalizi ya uboreshaji wa tovuti ya PPP ambapo kwa sasa Idara tayari imeshaandaa hadidu rejea kwa ajili ya kumpata mtaalamu wa kuiboresha tovuti hiyo.

**74. Mheshimiwa Spika;** Program Ndogo ya Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kwa mwaka wa fedha 2023/24 itatekeleza yafuatayo:-

1. Itaratibu miradi ya PPP (Kupitia maandiko ya awali, upembuzi yakinifu awali, upembuzi yakinifu kamili na vikao vya wadau);
2. Itasimamia utekelezaji wa Miradi 3 (Mradi wa Mkonga baharini, Mradi wa ujenzi wa Kituo kikubwa cha kuhifadia taarifa na Mradi wa Zanzibar Digital Free zone Hub);
3. Itafanya Mijadala Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi;
4. Itashiriki mijadala na maonesho yanayohusu miradi ya PPP;
5. Itaandaa ripoti za utekelezaji wa miradi ya PPP na mungozo wa miradi iliyoasisiwa na Taasisi binafsi;
6. Itazitembelea Mamlaka za utekelezaji pamoja na maeneo yaliyotengwa au kuibuliwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya PPP; na
7. Itajenga uwezo wafanyakazi wa PPP na Mamlaka za Utekelezaji kuhusu mambo ya (Model za Kifedha, Mazingira, Manunuzi, Tathmini na Ufuatiliaji).

**75. Mheshimiwa Spika;** Ili Programu Ndogo ya Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2023/24, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla Shilingi Milioni Mia Nne Thamanini na Nne, Sabini na Sita Elfu (TSh.484,076,000) (Matumizi ya kawaida 355,000,000 na Mishahara 129,076,000) kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na mishahara.

### 7.1.2 Programu ndogo SA080102: Maendeleo ya Ukuaji wa Uchumi kupitia Uwekezaji.

**76. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina lengo la kushajiisha Uwekezaji ndani na Nje ya Nchi na kuweka mazingira mazuri ya kisera, kisheria na uimarishaji wa huduma mbali mbali zitakazoimarisha Uwekezaji Nchini. Kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Programu ilikadiriwa matumizi ya Shilingi Bilioni Kumi na Tatu, Milioni Mia Nne Hamsini na Tano, Laki Tisa Sabini na Moja, Mia Nane Arobaini na Tatu (Tshs.13,455,971,843) (Ruzuku ya Mishahara TSh.2,130,971,843 na Miradi ya Maendeleo TSh.11,325,000,000).

**77. Mheshimiwa Spika,** Hadi mwezi Machi 2023, Programu ilifanikiwa kuidhinishiwa matumizi ya Shiningi Bilioni Tatu, Milioni Mia Sita Thamanini na Tisa, Laki Mbili Sitini na Nane, Mia Moja Arobaini na Moja (Tshs.3,689,268,141). Kati ya fedha hizo Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Moja Tisini na Sita, Laki Tisa Thamanini na Tano, Mia Tisa Tisini na Moja (TSh.2,196,985,991) kwa ajili ya ruzuku ya Mishahara ambayo sawa na asilimia 103 na Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Nne Tisini na Mbili, Laki Mbili Thamanini na Mbili, Mia Moja na Hamsini (TSh.1,492,282,150) ni kwa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ambayo sawa

na asilimia 13.18. Kwa mwaka wa fedha 2022/203, Programu imetekeleza yafuatayo:-

1. Inaendelea kuweka mazingira mazuri ya kisera na kisheria ili kuimarisha uwekezaji wa ndani na nje ambao utaweza kuongeza pato la Taifa, kukuza ajira, uchumi wa Nchi pamoja na kuleta maendeleo endelevu yatakayo imarisha ustawi wa wananchi bila ya kuharibu mazingira, silka, mila na tamaduni nzuri za Wazanzibari.
2. Inaendelea kuimarisha utoaji wa huduma kwa Wawekezaji kwa kuimarisha kituo cha utoaji wa huduma za pamoja "One Stop Center" ili kuweza kufanya kazi zake kwa ufanisi. Pia, imeimarisha utoaji wa huduma kwa kutumia Mfumo wa Kielektroniki ambapo huduma zote za Uwekezaji zitapatikana kwa njia ya Mtandao. Mfumo huu utaziunganisha taasisi zote zilioko chini ya kituo cha utoaji wa huduma za pamoja "One Stop Center".
3. Inaendelea na zoezi la kutafuta Wawekezaji kwenye visiwa ambapo hadi sasa visiwa 16 vimeshakodishwa vyenye mtaji wa Dola za Kimarekani Milioni Mia Tatu na Tisini na Tisa na Laki Tano (399,500,000) na vinatarajiwa kuzalisha ajira mbali mbali kwa wananchi wetu. Katika kuendelea na zoezi la kusimamia uwekezaji katika visiwa vidogo, jumla ya visiwa vitatu (Pamunda, Bawe na Changuu) vimeanza ujenzi wa maeneo yao ya uwekezaji;
4. Inaendelea kuimarisha miundombinu ya Uwekezaji kupitia Maeneo Huru ya Micheweni, Fumba na Amani. Ujenzi wa miundo mbinu katika Eneo Huru la Micheweni unaendelea ambapo Barabara ya kilomita 13.5 inaendelea na ujenzi, miundombinu ya maji

inaendelea kuwekwa pamoja na miundombinu ya umeme iko tayari, lengo likiwa kukifungua kisiwa cha Pemba kwa shughuli za uwekezaji. Aidha, inaendelea na kuweka utaratibu wa namna ya kutumia Ardhi ya Akiba iliyotengwa kwa Uwekezaji ili kurahisisha upatikanaji wa Ardhi kwa wawekezaji nchini.

5. Imefanikiwa kulipa fidia wananchi 217 katika Maeneo Huru ya Fumba na Micheweni kupisha uimarishaji wa Miundombinu na uwekezaji katika maeneo hayo ambayo ni Shilingi Bilioni Moja, Milioni MiaMoja Tisini na Sita, Laki Tisa Arobaini na Moja Elfu (Tsh.1,196,941,000).
6. Imefanikiwa kusajili miradi ya uwekezaji 74 ambayo inatengeneza mtaji wa makisio ya Dola za Kimarekani Milioni Mia Nne Arobaini na Nne, Laki Nne Sabini na Saba Elfu na Hamsini na Nne (444,477,054) na inatarajiwa kutengeneza jumla ya ajira 2,228 kwa wananchi.
7. Imeshiriki katika makongamano na maonesho mbalimbali Tanzania ili kukuza uwekezaji Zanzibar. Maonesho hayo ni pamoja na maonesho ya bidhaa za Viwanda, Kongamano la Tanzania na Iran lililofanyika Dar es salaam, kongamano la MIGA lililofanyika Dar es Salaam na kongamano la Wanawake la AfCFTA lililofanyika Dar es Salaam.

8. Ilishiriki katika ziara za uenezi kimataifa ikiwemo nchini Marekani na China. Kwa upande wa ndani ya Zanzibar, Programu ilishiriki katika kongamano la kumuezi Hayati Benjameni Mkapa, Zanzibar na Iran, Zanzibar na Italy, Silicon Zanzibar Initiative, Zanzibar

European Investment Forum, Tanzania Football Summit, Italy-Zanzibar Business and Invetsment Forum, Maonesho ya Kizimkazi Festival, kongamano la Siku ya Utalii Duniani, pamoja na kongamano la wafanyabiashara wa Kimarekani.

9. Imeshiriki katika makongamano na maonesho manne ambayo ni; kongamano la "Agribusiness Trade mission Investment summit", Business Fact-Finding Mission to Tanzania and Zanzibar. Makongamano yote haya yametumika katika kutangaza Uwekezaji Zanzibar; Bara na nje ya Zanzibar kwa lengo la kuongeza idadi ya Wawekezaji Nchini;

10. Imetengeza na kufanya ukarabati wa miundo mbinu muhimu ya maeneo ya uwekezaji ambapo Matengenezo na Ujenzi wa mfumo wa mitaro ya maji ya mvua na maji taka katika maeno ya Amani na Maruhubi ambapo ujenzi rasmi utaanza rasmi fedha za maendeleo zitakapoingizwa. Aidha, kazi ya kutekeleza mpango mpya wa matumizi ya Ardhi Fumba imefanyika kwa kuanza keweka mipaka katika vijiji vilivyopo maeneo ya uwekezaji Fumba

11. Imekamilisha uandaaji wa Muongozo wa Uwekezaji Zanzibar unaoonesha wasifu wa Sekta na Fursa za Uwekezaji zilizopo nchini ambapo Mfumo na Muongozo huo ulizinduliwa katika maadhimisho ya Siku ya Uwekezaji Zanzibar na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi.

12. Inaendelea na zoezi la kufanya Utafiti wa Mitaji Binafsi ya wageni (PCF) mzunguko wa 14, ambapo taarifa za wawekezaji na uwekezaji zilizokusanywa tayari

zimeanza kuingizwa katika mfumo wa uchambuzi wa taarifa kwa lengo la kuandaa ripoti ya Utafiti huo;

13. Imewajengea uwezo watendaji wa Idara mbali mbali kuhusiana na maeneo yao ya kazi ili kuimarisha ufanisi wa kazi.

**78. Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Programu itatekeleza yafuatayo:-

1. Itatangaza fursa za Uwekezaji Zanzibar;
2. Itapokea na kusajili miradi ipatayo 100 ambayo itatengeneza mtaji wa dola za Kimarekani zipatazo milioni 500 na kuleta ajira zipatazo 2,000 kwa wananchi;
3. Itaendelea na zoezi la kutangaza fursa zilizopo katika uwekezaji wa visiwa vidogo vidogo;
4. Itajenga na kuendeleza miundombinu (maji, umeme na barabara) katika Maeneo Huru ya Uchumi (Micheweni, Fumba na Amani n.k) ili kuvutia wawekezaji zaidi;
5. Itaharakisha mchakato wa upatikanaji maeneo yalioanishwa kuwa ni ardhi ya Akiba (land bank) kwa lengo la uwekezaji wa miradi yenye tija;
6. Itaendelea na awamu ya pili ya kufanya muunganiko (Intergration) wa Mfumo wa Kielektroniki wa ZIPA na Mifumo mengine ya Serikali inayohudumia wawekezaji;
7. Itakamilisha Sheria Mpya ya Uwekezaji Zanzibar na Kanuni zake.

**79. Mheshimiwa Spika;** Ili Programu Ndogo ya Maendeleo ya Ukuaji wa Uchumi kupitia Uwekezaji iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha

2023/2024, naliomba Baraza lako kuidhinisha Shilingi Bilioni Sita, Milioni Mia Tatu Thamanini na Saba na Laki Nane (Tsh.6,387,800,000) (Ruzuku ya Mishahara 2,887,800,000 na Maendeleo SMZ 3,500,000,000).

## 7.2 PROGRAMU KUU PA0802: UENDESHAJI NA URATIBU WA AFISI KATIKA UCHUMI NA UWEKEZAJI.

**80. Mheshimiwa Spika,** Programu hii Kuu kwa kipindicha Julai 2022 hadi Machi 2023 cha mwaka wa Fedha 2022/2023 ilikadiriwa kiasi cha Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Nne Sitini na Tatu, Laki Nane Thamanini, Mia Tatu Ishirini na Tano (Tsh.1,463,880,325) mpaka kufikia mwezi Machi, 2023 imeidhinishiwa matumizi ya kiasi cha Shilingi Milioni Mia Saba Sabini na Nne, Laki Nne Thamanini na Tisa, Mia Mbili na Ishirini (TSh.774,489,220) (Matumizi ya kawaida 300,452,200 na Mishahara 474,036,520) sawa na asilimia 52.9 ya utekelezaji programu zake ndogo.

### 7.2.1 Programu ndogo SA080201: Utawala na Uendeshaji.

**81. Mheshimiwa Spika;** Programu Ndogo SA080201 ya Utawala na Uendeshaji ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Uendeshaji na Utumishi na Kukuza uwezo wa Afisi kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Programu ilikadiriwa matumizi ya Shilingi Milioni Mia Tisa Sabini na Tisa, Laki Nane Thamanini na Nane, Mia Tano Sabini na Tano (Tshs.979,488,575) na ilifanikiwa kuidhinishiwa matumizi ya Shiningi Milioni Mia Sita Arobaini na Sita, Laki Tisa Ishirini Elfu, Mia Saba Ishirini (TSh.646,920,720) ambayo sawa na asilimia 66.6 ya makadirio. Programu imetekeleza shughuli zifuatazo:-

1. Imesimamia malipo ya safari 24 za ndani za kikazi kwa Viongozi wa Afisi kwenda Dar es salaam, Pemba, Dodoma na Arusha. Pia, imefanya matengenezo ya gari 4 za Viongozi na imesimamia ununuzi wa mafuta kwa ajili ya ufuatiliaji wa kazi za Afisi na imefanya matengenezo ya Afisi ya Mhasibu Mkuu A08.
2. Imefanya ununuzi wa vifaa vya kuandikia, samani za Afisi na vifaa vya usafi.
3. Imewapatia mafunzo ya muda mfupi ya ndani ya Nchi wafanyakazi 7 (Wanawake 5 na Wanaume 2) ambao ni Afisa Kumbukumbu (1), Katibu Muhtasi (3), Afisa IT (1), Wahasibu (2).
4. Imewapatia posho la likizo Wafanyakazi 5 (Wanaume 2 na Wanawake 3) wanaostahiki posho hilo.Pia, imefanya malipo ya simu kwa wafanyakazi wanaoratibu Mfumo wa Sema na Rais (SNR) na malipo ya saa za ziada kwa wafanyakazi 6 (Wanawake 5 na Mwanamme 1) walioshiriki kuandaa Mpango wa Rasilimali Watu.
5. Imeratibu na kugharamia vikao vitatu (3) vya kitengo cha ununuzi na vikao (2) kupitia kitengo cha ukaguzi wa ndani.
6. Imekamilisha Mpango wa Rasilimali Watu wa kipindi cha miaka mitano,

82. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Utawala na Uendeshaji kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 itatekeleza yafuatayo:-

1. Itaendelea kusimamia Maslahi ya Wafanyakazi kama vile malipo ya mishahara, posho la likizo, malipo ya saa za ziada na malipo ya ubani kwa wafiwa;

2. Itaendelea kutoa mafunzo ya ndani kwa Wafanyakazi 150, zoezi la Upimaji Utendaji kazi kwa Wafanyakazi kwa kila mwaka,
3. Itaiimarisha mazingira ya Afisi nje na ndani;
4. Itaandaa Mpango wa Mafunzo na Mpango wa Rasilimali watu;
5. Itasimamia ununuzi wa vifaa vya Afisi.

**83. Mheshimiwa Spika,** Ili Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2023/24, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla Shilingi Milioni Mia Nane Thalathini na Tano, Laki Tano Ishirini na Tisa Elfu (TSh.835,529,000) (Matumizi ya kawaida 322,300,000 na Mishahara 513,529,000) kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na mishahara.

### 7.2.2 Programu Ndogo SA080201: Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Afisi

**84. Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo SA080202 ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Afisi kwa robo tatu (Julai, 2022 – Machi, 2023) Programu ilikadiriwa matumizi ya Shilingi Milioni Mia Mbili Thalathini na Tisa, Laki Tisa Tisini na Tisa Elfu (Tsh.239,999,000) na ilifanikiwa kuidhinishiwa matumizi ya Shiningi Milioni Arobaini na Nane, Laki Nne na Elfu Kumi (TSh.48,410,000) kwa ajili ya Matumizi ya kawaida ambayo sawa na asilimia 20.1 ya makadirio. Programu kwa kipindi cha Julai 2022, hadi Machi, 2023 imetekeleza shughuli zifuatazo:-

1. Inaendelea kufanya mapitio ya Sera ya Uwekezaji ya Zanzibar ya mwaka 2005 ambapo imeanza

kwa kufanya Tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Uwekezaji ya mwaka 2005 imekamilika na matokeo yake yamezingatiwa katika uaandaaji wa Sera mpya ya Uwekezaji. Tayari Rasimu ya kwanza ya Sera ya Uwekezaji 2023 imekamilika na ipo katika hatuaya kupata maoni ya wadau, Kamati ya Uongozi na hatimae kuwasilishwa katika vikao vya maamuzi.

2. Inaendelea kufanya mapitio na kuandaa Sheria na Kanuni za Uwekezaji Wananchi Kiuchumi ambapo Mswada wa Sheria umezingatia masuala ya wajibu wa muwekezaji kuchangia katika huduma za jamii, wadau wa ndani kunufaika na fursa zinazopatikana katika miradi ya uwekezaji, suala la ardhi ya akiba ya Uwekezaji, kupunguza kiwango cha mtaji wa kuwekeza na mazingatio maalum kwa Diaspora katika uwekezaji.
3. Imekamilisha uratibu wa uandaaji wa Muongozo wa Uwekezaji Zanzibar ambao ulizinduliwa tarehe 10 Machi, 2023 na Rais wa Zanzibar na Mweneyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt Hussein Ali Mwinyi katika ukumbi wa Hotel ya Golden Tulip Airport. Lengo la muongozo huo ni kutoa taarifa za vivutio, fursa na taratibu za Uwekezaji Zanzibar. Muongozo huo pia unapatiakana kwa njia ya kielektroniki. Muongozo umeainisha maeneo na sekta ya vipaumbele vya Serikali katika Uwekezaji.
4. Kwa kushirikiana na UNDP, imekamilisha uandaaji wa 'Documentary ya Uwekezaji inayoonesha fursa na maeneo ya Uwekezaji nchini katika Sekta za Visiwa, Utalii na Uchumi wa Buluu ambayo imeoneshwa kwenye sherehe za Uzinduzi wa Muongozo na Mfumo wa Kielektroniki wa ZIPA.

5. Imefanya manunuzi ya vifaa katika divisheni zake ili kuweza kufanya kazi kwa ufanisi, Pia, imeimarisha masuala ya upatikanaji wa mtandao katika Afisi kwa ajili ya kuboresha utekelezaji wa shughuli mbali mbali za Afisi.
6. Imelipia gharama ya safari za ndani ya nchi kwa wafanyakazi walioshiriki katika kikao cha Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wakilishi kilichofanyika Pemba na kwa Wafanyakazi walioshiriki shughuli mbali mbali za kikazi Tanzania Bara na Pemba.
7. Imekamilisha uandaaji wa Agenda za Utafiti za Afisi ambapo Agenda hizo zimeshapitiwa katika Kamati ya Uongozi na tafiti zilizoainishwa zimeanza kutekelezwa na zimeainishwa katika Mpango Kazi wa mwaka wa fedha 2023/2024.
8. Imeandaa Wasifu wa Miradi ya Afisi (Project Profile) kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Afisi. Jumla ya maandiko ya miradi 3 yameandaliwa na kuanza kuwasilishwa Tume ya Mipango kwa hatua ya kupatiwa fedha za utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Miradi hiyo ni pamoja na Mradiwa Ujenzi wa Afisi Unguja na Pemba; Uimarishajiwa Miundombinu katika Maeneo Huru ya Uwekezaji na Mfumo wa Kielektroniki wa Utoaji wa Huduma za Pamoja ZIPA.
9. Imeratibu utayarishaji wa ripoti mbalimbali za utekelezaji zikiwemo, ripoti ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020 – 2025, ripoti zilizowasilishwa katika kamati mbali mbali za Baraza la Wawakilishi, ripoti ya utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Maendeleo wa Zanzibar (2021-2026) na ripoti maalum

zilizohitajika kwa vipindi tofauti zinazohusiana na utekelezaji wa shughuli za Afisi katika taasisi mbali mbali.

10. Imefanya ziara ya ufuatiliaji na tathmini kwa kutembelea miradi ya uwekezaji kisiwani Pemba ambapo iliangalia maendeleo ya ujenzi wa miundombinu katika Maeneo Huru ya Micheweni na Kiwanda cha uzalishaji maji. Ujenzi wa Miundombinu ulikua unasuasua lakini Afisi kwa kushirikiana na Kamati ya Bajeti imeweza kulitatua suala hilo. Aidha, ucheleweshaji wa fidia kwa wananchi ambapo Afisi iliwasilisha maombi hayo AR-Fedha na Mipango ambapo tayari limefanyiwa kazi na AR- Fedha na Mipango imeanza kuingiza fedha za Maendeleo.

11. Imeratibu ziara ya Mashirikiano Tanzania Bara baina ya Afisi na Kituo cha Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi Tanzania Bara Dodoma ambayo ilimalizikia kituo cha Mabasi Mwendo kasi Dar es Salaam. Ziara hiyo, ilikuja na maazimio ya kukamilisha utekelezaji wa miradi iliyokuwa inafadhiliwa na Benki ya Dunia, kuimarisha muundo wa Taasisi, kuongeza rasilimali watu na fedha, kuandaa mpango wa mafunzo wa pamoja, kuandaa PPP Portal ya pamoja kwa ajili ya kuratibu miradi ya PPP Tanzania Bara na Visiwani, kuandaa mkakati wa kushirikiana na sekta binafsi na kufanya marekebisho ya Sheria na Sera ya PPP.

**85. Mheshimiwa Spika,** Programu kwa mwaka wa fedha 2023/2024, imepanga kutekeleza yafuatayo:-

1. Kuchapisha nakala ya Sera Mpya ya Uwekezaji,

2. Kufanya Mapitio ya Sera ya PPP;
3. Kuandaa Sera ya 'Corporate Social Responsibility';
4. Kufanya tafiti za Afisi kwa mujibu wa Agenda za Utafiti;
5. Kuratibu utekelezaji wa Programu na Miradi ya Afisi;
6. Kufanya ufuatiliaji na tathmini wa shughuli za Afisi;
7. Kuandaa Mkakati wa Uenezi wa Uwekezaji (Investment Promotion Strategy)
8. Kuimarisha upatikanaji wa takwimu za shughuli mbali mbali za Afisi na Kuimarisha Mashirikiano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa.

**86.** **Mheshimiwa Spika**, Ili Programu Ndogo ya Uratibu wa Sera, Mipango na Tafiti za Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2023/24, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla Shilingi Milioni Mia Tatu Thalathini na Tisa, Laki Nane Tisini na Tano Elfu (TSh.339,895,000) (Matumizi ya kawaida 247,300,000 na Mishahara 92,595,000) kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na Mishahara.

### 7.2.3 Programu Ndogo SA080203: Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Afisi Pemba.

**87.** **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Afisi Pemba ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Afisi Pemba ambayo inahusisha Idara ya Uendeshaji na Utumishi pamoja na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Programu ilikadiriwa matumizi ya Shilingi Milioni Mia Mbili Arobaini na Nne, Laki Tatu Tisini na Mbili, Mia Saba

Hamsini (Tshs.244,392,750) na ilifanikiwa kuidhinishiwa matumizi ya Shilingi Milioni Sabini na Tisa, Laki Moja Hamsini na Nane na Mia Tano (TSh.79,158,500) ambayo sawa na asilimia 32.39 ya makadirio. Programu kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 imetekeleza yafuatayo:-

1. Imeandaa makala (documentary) kwa ajili kutangaza fursa za uwekezaji zinazopatikana Kisiwani Pemba. Maeneo muhimu yaliyowekwa katika makala hio ni fukwe, hoteli, misitu, maeneo ya kihistoria, visiwa vidogo vidogo, Maeneo Huru ya Uwekezaji, Eneo la Viwanda Chamanangwe pamoja na utamaduniwa watu wa Pemba. Makala hii itarushwa kupitia vyombo vya habari pamoja na Mtandao wa 'YouTube'ili ziweze kutangazwa fursa za uwekezaji zilizopo kisiwani Pemba.

2. Imefanya makongamano manne (4) kwa Vijana wa Wilaya za Chake – Chake, Mkoani, Wete na Micheweni kuhusu Sekta ya Uchumi na Uwekezaji katika kutengeneza fursa za ajira kwa Vijana. Jumla ya washiriki 200 (Wanawake 88 na Wanaume 112) walihudhuria. Washiriki walitokea katika taasisi za vyuo, Baraza la Vijana, jumuia za vijana, vyuo vya amali, wajasiriamali na mameneja na watendaji wa hoteli. Kupitia kongamano hilo, Vijana walijifunzana kuzitambua fursa mbalimbali zinazopatikana katika Sekta ya Uchumi na Uwekezaji zikiwemo ajiraza moja kwa moja na fursa za kusambaza bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali. Aidha, Jukwaa hili lilitumika kuondoa fikra mgando kwa jamii kuwa kufanya kazi katika sekta ya hoteli si uhuni bali ni kazi za heshima na staha kama zilivyo kazi nyengine na

kuachana na fikra za kutegemea kazi kutoka serikalini pekee.

3. Imefanya ufuatiliaji na tathmini kwa lengo la kuimarisha utendaji wa shughuli za Afisi. Pia, ilitayarisha ripoti za ufuatiliaji na tathmini ambazo zinaonesha mafanikio, changamoto na mapendekezo ndani yake. Ufuatiliaji huo ulifanyika katika Hoteli ya Aiana, Hoteli ya Manta Resort, Pemba Lodge na Planet-Ecanara, Maeneo Huru ya Uwekezaji Micheweni, Kiwanda cha Maji Kinyikani, kiwanda cha maji Chamanangwe, ujenzi wa kiwanda cha mwani Chamanangwe na Ujenzi wa hoteli Uvinje.

   Kwa upande wa Hoteli zilizofuatiliwa, matokeo yanaonyesha kuwa, zinaendelea na huduma vizuri na upokeaji wa wageni umeimarika ukilinganishana mwaka jana. Aidha, ufuatiliaji uligundua kuwa uwekezaji wa mahoteli una fursa nyingi kwa wajasiriamali wanaotengeneza bidhaa za asili Kisiwani Pemba kwani wageni wengi wanazipenda. Hivyo, Afisi iliishauri Programu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kuweza kuwahamasisha na kuwasaidia wajasiriamali wenye bidhaa bora zilizotengenezwa kwa malighafi zinazopatikana Kisiwani Pemba kuweza kusambaza bidhaa hizo mahotelini.

4. Kwa upande wa ajira, Sekta ya hoteli ina mchango mkubwa kwa Vijana wetu kwani kwa hoteli hizi ambazo Afisi ilifanya ufuatiliaji zimeajiri Vijana 159 (Wanawake 37 na Wanaume 122) ambao ni wazalendo na wanaotoka katika maeneo ya hoteli husika.

5. Kwa upande wa ujenzi wa hoteli ilioko Uvinje Oxygen

hotel ambayo kwa sasa imebadili umiliki kutoka Oxygen holding na kwenda kwa Daya Investiment mwishoni mwa mwaka 2022, mradi umesita katika hatua ya ujenzi mpaka ufuatiliaji huu unafanyika. Hii ni kutokana na kubadilisha umiliki wa mradi. Miongoni mwa changamoto zilizobainika katika eneo hili ni kutokulipwa mishahara kupitia akaunt za benki, kutopelekwa kwa michango ya ZSSF na kutopatiwa likizo kwa wafanyakazi waliopo. Changamoto hizi tayari zimemepatiwa ufumbuzi baada ya Kamisheni ya kazi kutoa maagizo juu ya kufuatwa kwa sheria za kazi.

6. Imefanya ufuatiliaji katika Maeneo Huru ya Uwekezaji Micheweni ambapo Afisi imeona kuwa miundombinu katika Maeneo hayo inaendelea kuimarishwa ambapo hadi kufikia sasa tayari kumejengwa laini 3 za umeme, barabara yenye urefu wa km 2.4 kwa kiwango cha lami na barabara za ndani zenye urefu wa km 13.5 ambazo ziko katika hatua ya kifusi. Aidha, kwa upande wa maji, utaratibu wa kuwekwa miundombinu ya maji unaendelea kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA).

7. Imefanya ufuatiliaji katika Kiwanda cha Maji (Amos Industry Ltd) kilichopo Kinyikani katika eneo la viwanda Chamanangwe. Viwanda vinaendelea na uzalishaji na kutoa huduma ya uzalishaji wa maji na hivyo kuifanya Pemba kuwa na viwanda viwili vya kuzalisha maji. Kwa upande wa utekelezaji wa sheria za kazi, viwanda hivi vinatekeleza sheria za kazi ipasavyo.

8. Imekusanya maandiko ya miradi ya PPP kutoka

katika taasisi mbalimbali za Serikali. Afisi, imefanya mafunzo ya siku tatu kwa taasisi za umma juu ya utayarishaji wa dhana na concept note kwa miradi inayoendana na PPP. Jumla ya miradi 9 kutoka katika sekta mbali mbali imewasilishwa taarifa muhimu ili Idara ya PPP kwa kushirikiana na taasisi iweze kukamilisha uandishi wa miradi hiyo. Dhana za miradi zilizowasilishwa ni pamoja na Ujenzi wa madiko Pemba, ujenzi wa viwanja vya kufurahishia watoto, Mfumo wa usimamizi wa taka, Ujenzi wa nyumba nafuu Mfikiwa, ujenzi wa matenki ya maji na Kupima Uzito wa magari yanayoingia Bandarini.

9. Imefanya mkutano wa siku moja na wadau wa Mashirikiano baina ya sekta ya Umma na SektaBinafsi kwa ajili ya kuwasilisha dhana za miradiiliyoibuliwa (Project Profile). Aidha, kikao kilijadili namna ya kuunganishwa kwa dhana za miradi ya taka ngumu (solid waste) kwa Baraza la Mji Wete, Barazala Mji Chake - Chake na Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni. Vilevile, kikao hiki kilijadiliana kuundwa kwa timu za wasimamizi wa miradi hio (Project Management Team).

10. Imefanya mikutano na timu tisa (9) za wasimamizi wa miradi pamoja na kufanya ukaguzi wa maeneo ya miradi kwa ajili ya kutoa taaluma ya namna bora ya vigezo na takwimu zinazohitajika katika uandishi wa "detailed concept notes" za miradi hiyo.

11. Kwa kushirikiana na Mamlaka ya Ukuzaji Vitega Uchumi Afisi iliandaa mkutano na wawekezaji wa miradi iliyoekezwa kupitia ZIPA kujadili changamoto wanazokabiliana nazo zinazokwamisha utendaji wao

wa kazi, utoaji wa ripoti za maendeleo ya miradi (QPR), ufuataji wa sheria na miongozo inayotolewa na serikali. Mkutano huu ulibaini changamoto ya ukosefu wa maji inadhoofisha utendaji wao wa kazi. Jitihada za kuwasiliana na ZAWA zilifanywa kwa ajili ya kulishughulikia tatizo hili.

12. Kwa kushirikiana na Mamlaka ya Ukuzaji Vitega Uchumi, Programu imeandaa kituo cha utoaji wa huduma kwa wawekezaji kwa kila mwezi kwa ajili ya kurahisisha na kusogeza huduma kwa wawekezaji walioko Pemba kutatua matatizo yao na kuepusha usumbufu na gharama wanazozipata kwa kufuata huduma hizo makao makuu Unguja. Kituo hiki kinajumuisha maafisa wenye maamuzi kutoka Uhamiaji, Ardhi, Kamisheni ya kazi, Mipango Miji, Benki ya PBZ, Mazingira, TRA, ZRA, Kamisheni ya Utalii. Kituo hiki kimeleta mafanikio makubwa na urahisi wa kufanya shughuli zao wakiwa Pemba.

13. Imeratibu vikao vya kujadili utayarishaji wa Bajeti ya mwaka 2023/2024 (MTEF, PBB na Mpango kazi) na kutayarisha ripoti mbalimbali ikiwemo, ripoti ya utekelezaji wa kazi za Afisi, utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020 - 2025 na ripoti maalum kutokana na maagizo ya viongozi.

14. Aidha, Programu imefanya manunuzi ya kompyuta 3 na printa tatu (3), vifaa vya kielektroniki, chakula na vinywaji, kulipia gharama za umeme, simu, mafuta, matengenezo ya gari na vifaa vya kuandikia. Pia, imelipia gharama za usafiri kwa maafisa waliokwenda Unguja kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kazi za Afisi.

88. **Mheshimiwa Spika;** Programu kwa mwaka wa fedha 2023/24, itatekeleza yafutayo:-

1. Itarusha hewani vipindi 6 na makala moja kutangaza fursa za Uwekezaji Pemba,
2. Itafanya makongamano 4 kuhusu mchango wa Sekta ya Uchumi na Uwekezaji katika kutoafursa za ajira;
3. Itaendelea na utoaji wa taaluma kuhusiana na miradi ya PPP kwa taasisi za umma na binafsi pamoja na kuwajengea uwezo watendaji 80;
4. Itatayarisha dhana za miradi na kuchambua Miradi ya PPP 20 pamoja na kuitangaza Idara ya PPP Pemba;
5. Itaendelea kusimamia utekelezaji bora wa sera, sheria na miongozo mbalimbali kwa kusimamia maslahi ya wafanya kazi kwa kulipa posho ya safari 43, malipo ya masaa ya ziada 5, likizo wafanyakazi 3, huduma ya mazishi wafanyakazi3, matibabu wafanyakazi 3;
6. Itatoa mafunzo ya ndani kwa wanyakazi 35 kuhusiana na sera mipango ya Afisi na mipango ya maendeleo katika maswala ya uchumi na Uwekezaji;
7. Itawapatia mafunzo ya muda mfupi kwa wafanyakazi 4;
8. Italipia gharama za maji, umeme na huduma ya usafi na itafanya manunuzi ya mafuta, vifaa vya kuandikia, vifaa vya usafi na kumpyuta 2; na
9. Itaendelea kuandaa taarifa za utekelezaji na kufanya shughuli za ufuatiliaji na tathmini za Afisi pamoja na kuripoti utekelezaji wake.

89. **Mheshimiwa Spika;** Ili program ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Afisi Kuu Pemba iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwakawa fedha 2023/24 naliomba Baraza lako kuidhinisha Shilingi Milioni Mia Moja Thamanini na Nne na Laki Tisa (Tsh.184,900,000) (Matumizi ya kawaida 150,000,000 na Mishahara 34,900,000) kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida

## 8.0 MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

## 8.1 VIPAUMBELE VYA AFISI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

90. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024, ARKUU imepanga kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

    1. Kukuza Uwekezaji kwa kuweka mikakati ya kutangaza fursa za uwekezaji Pemba, Visiwa vidogo vidogo, Mjimkongwe, Utalii na Uchumi wa Buluu;

    2. Kuimarisha 'ZIPA One Stop Center; kwa kutoa huduma za pamoja za Uwekezaji kwa ufanisi;

    3. Kuimarisha miundombinu ya Uwekezaji katika Maeneo Huru ya Uwekezaji nchini na Ardhi ya Akiba kwa Uwekezaji;

    4. Kukuza na kuimarisha Uwekezaji wa Sekta Binafsi na Sekta ya Umma;

    5. Kukamilisha uandaaji wa Sera na Sheria ikiwemo Sera ya Uwekezaji Zanzibar, Sera ya CSR, Sera ya Maendeleo ya Ushirika, Sera ya PPP, Sera ya 'Local Content',

Sera ya TEHAMA ya Afisi na Sera ya Ajira. Sheria ya Uwekezaji, Sheria ya Ajira, Sheria ya Maendeleo ya Ushirika, Sheria ya Kukuza Ajira Nchini;

6. Kwa kushirikiana na ZSSF kuimarisha Mafao ya Watendaji waliopoteza ajira;

7. Kuratibu upatikanaji wa ajira za staha ndani 10,000 na nje ya nchi 1,500;

8. Kukuza ujuzi wa Vijana 110 kuweza kujiajiri na kuajirika;

9. Kuimarisha Usalama na Afya kazini kwa ununuzi wa vifaa vya uchunguzi wa afya na usalama kazini, kufanya utafiti wa maradhi yanayotokana na kazi, kufanya ukaguzi na kujenga uwezo wa watendaji;

10. Kufanya tafiti 3 (Masoko ya wajasiriamali, Ajira katika Sekta Binafsi na Mchango wa Uwekezaji katika kukuza Uchumi na kuzalisha ajira kwa Wazawa) kwa mujibu wa Agenda za Tafiti za Afisi.

11. Kuimarisha uwezeshaji wananchi kiuchumi kwa kutoa mikopo nafuu 3,000, mitaji na Kujenga miundombinu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;

12. Kuimarisha ubora na masoko ya bidhaa za Wajasiriamali na kutoa mafunzo ya ujasiriamali na biashara;

13. Kuimarisha viwanda vidogo vidogo na vya kati vya Wajasiriamali;

14. Kuleta mabadiliko na mageuzi ya Sekta ya ushirika kwa maendeleo ya jamii na kukuza Uchumi wa nchi;

15. Kuimarisha mashirikiano baina ya Afisi na Taasisi nyengine Kitaifa, Kikanda na Kimataifa;

16. Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za Afisi;

17. Kukuza ujuzi wa watendaji katika kutekeleza majukumu yao; na

18. Kuimarisha ufanisi wa utekelezaji wa shughuli za Afisi.

## 8.2 MUELEKEO WA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024.

### 8.2.1 FUNGU A07 KAZI NA UWEZESHAJI

**91. Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Rais Kazi Uchumina Uwekezaji katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024 kupitia fungu A07 (Kazi na Uwezeshaji) inatarajiwa kukusanya mapato ya Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Saba Thalathini, Laki Moja Sitini na Moja Elfu (TSh.2,730,161,000) kupitia vianzio vyake 6 vikiwemo Ada za Usajili na Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika, Ada ya Ukaguzi wa Mikataba ya Ajira Nje ya Nchi, Ada ya Ukaguzi wa Maeneo ya Kazi na Vibali vya Kazi **(Kiambatanisho nambari 8 kinahusika).**

**92. Mheshimiwa Spika,** Afisi kupitia fungu A07 (Kazi na Uwezeshaji) ili iweze kutekeleza Programu zake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2023/2024, naliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya Shilingi Bilioni Kumi na Nne, Milioni Mia Tisa Sitini na Nne, Laki Mbili Kumi na Moja Elfu (Tsh.14,964,211,000). Kati ya fedha hizo Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Moja Arobaini na Tano na Laki Nne na Elfu Sita (Tsh.3,145,406,000) ni Mishahara; Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tisa Tisini na Tatu na

Laki Saba (Tsh.1,993,700,000) ni kwa ajili ya matumizi ya Kawaida; Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Saba Thamanini na Nne na Laki Tano (Tsh.2,784,500,000) ni Ruzuku ambapo (Tsh.1,699,000,000 ruzuku ya kawaida na Tsh.1,085,500,000 ruzuku ya Mishahara). Pia, Afisi inaliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya Shilingi Bilioni Saba, Milioni Arobaini, Laki Sita na Elfu Sita (Tsh.7,040,606,000) za kutekeleza Miradi ya Maendeleo ambapo Shilingi Bilioni Nne, Laki Tano (Tsh.4,500,000,000) zinatoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Tano Arobaini, Laki Sita na Elfu Sita (Tsh.2,540,606,000) zinatoka kwa Washirika wa Maendeleo.

93. **Mheshimiwa Spika,** Mgawanyo wa matumizi ya fedhahizo kwa Programu za fungu A07 (Kazi na Uwezeshaji) ni kama ufuatao:- Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Saba Thalathini na Nane na Laki Nne (Tsh.1,738,400,000) (Ruzuku ya kawaida 652,900,000 na Ruzuku ya Mishahara1,085,500,000) ni kwa ajili ya kutekeleza Programu Kuu ya Usimamizi wa Sheria za Kazi, Ukaguzi Kazi na Kazi za Staha kwa wote; Shilingi Bilioni Kumi, Milioni Mia Saba Sitini na Sita, Laki Tatu Sabini na Nne Elfu (Tsh.10,766,374,000) (Matumizi ya kawaida 991,000,000, Mishahara 1,688,668,000, Ruzuku 1,046,100,000 SMZ Maendeleo 4,500,000,000 na Washirika wa Maendeleo 2,540,606,000) ni kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Nne Hamsini na Tisa, Laki Nne Thalathini na Saba Elfu (Tsh.2,459,437,000) (Matumizi ya kawaida 1,002,700,000 na Mishahara 1,456,737,000) ni kwa ajiliya kutekeleza Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji **(Kiambatanisho nambari 9 kinahusika)**.

### 8.2.2 FUNGU A08 UCHUMI NA UWEKEZAJI

94. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kupitia fungu A08 (Uchumi na Uwekezaji) ili iweze kutekeleza Programu zake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2023/2024, naliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya Shilingi Bilioni Nane, Milioni Mia Mbili Thalathini na Mbili na Laki mbili (Tsh.8,232,200,000). Kati ya fedha hizo Shilingi Milioni Mia Saba Sabini na Laki Moja (Tsh.770,100,000) ni Mishahara; Shilingi Bilioni Moja, Milioni Sabini na Nne na Laki Tatu (Tsh.1,074,300,000) ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za Kawaida; Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Nane Thamanini na Saba na Laki Nane (Tsh.2,887,800,000) ni kwa ajili ya Ruzuku ya Mishahara na Shilingi Bilioni Tatu na Milioni Mia Tano (Tsh.3,500,000,000) ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

95. **Mheshimiwa Spika,** Mgawanyo wa fedha hizo kwa Programu za Fungu A08 (Uchumi na Uwekezaji) ni kama ufuatao:- Shilingi Bilioni Sita, Milioni Mia Nane Sabini na Moja, Laki Nane Sabini na Sita Elfu (Tsh.6,871,876,000) (Matumizi ya kawaida 355,000,000, Mishahara 129,076,000 na Ruzuku ya Mishahara 2,887,800,000 na Maendeleo SMZ 3,500,000,000) ni kwa ajili ya kutekeleza Programu Kuu ya Kuimarisha Uwekezaji na Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi na Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tatu Sitini, Laki Tatu Ishirini na Nne Elfu (Tsh.1,360,324,000) (Matumizi ya kawaida 719,300,000 na Mishahara 641,024,000) zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji **(Kiambatanisho nambari 10 kinahusika)**.

## 9.0 HITIMISHO

96. **Mheshimiwa Spika;** Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji inatanguliza shukrani zake za dhati kwa mashirikiano mazuri kupitia taasisi mbali mbali zinazofanya kazi pamoja zikiwemo Taasisi za Serikali, Taasisi Binafsi, Washirika wa Maendeleo, Mabenki, Asasi za Kiraia, Wakuu wa Mikoa, Wakuu Wa Wilaya na Jamii kwa ujumla. Afisi inaanza kwa kuwashukuru Washirika wa Maendeleo tunaofanya kazi nao ambao ni ILO, UNDP, FAO, Benki ya Dunia (World Bank), Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, inazishukuru taasisi za kiraia ikiwemo ZATUC, ZANEMA COSTECH, Chuo cha Ushirika Moshi, Milele Foundation na Taasisi zote zinazoshirikiana nasi kwani si rahisi kuzitaja moja moja. Pia, Afisi inazishukuru Taaasisi zote za kifedha ikiwemo Benki ya PBZ, Equity Benki, AMANA Benki, ADB, TABD, DTB, BOA, CRDB Benki na Taasisi zote za Fedha zikiwemo SACCOS kwa mashirikiano yao mazuri na Afisi yetu.

97. **Mheshimiwa Spika;** Aidha, Napenda kuvishukuru vyombo vyote vya habari vinavyoshirikiana nasi katika kuelimisha jamii juu ya shughuli zinazozifanywa na Afisi. Vyombo hivyo vimechangia kwa kiasi kikubwa shughuli za Afisi yetu kujulikana na jamii. Sitaweza kuvitaja kimoja kimoja lakini navishukuru vyote kwa ujumla. Aidha, napenda kuwashukuru wote wanaoshirikiana nasi katika kutekeleza majukumu yetu kwa njia moja au nyengine; nawaomba waendelee kuwa nasi katika kufanikisha malengo ya kuwaletea wananchi maendeleo endelevu. Vile vile, nawashukuru kwa dhati Wanajamii, Wajasiriamali na Wawekezaji wote waliowekeza na

wale wote walioonesha nia ya kuja kuwekeza nchini. Tunawakaribisha sana.

98. **Mheshimiwa Spika,** Napenda kuchukua fursa hii adhimu kuwashukuru Watendaji wote wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kuanzia Katibu Wakuu wa Uchumi na Uwekezaji pamoja na Katibu Mkuu anayesimamia Kazi na Uwezeshaji; Manaibu Makatibu Wakuu, Ofisa Mdhamini Pemba; Mkurugenzi Mtendaji ZIPA; Mkurugenzi Mtendaji ZEEA; Makamishna; Wakurugenzi, Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi zilizopo chini ya Afisi na Watendaji wote kwa mashirikiano makubwa wanayonipa katika kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi. Nakiri mbele yako kwamba mafanikio haya yaliyopatikana ni kwa juhudi zao kubwa wanazifanya katika kufikia malengo tulijiwekea. Nawaomba waimarishe umoja na mshikamano tulionao katika kuwahudumia wananchi wetu na wawekezaji nchini.

99. **Mheshimiwa Spika,** Kwa niaba ya Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji napenda kuchukua fursa hii kwa mara nyengine tena kukushukuru wewe na Wajumbe wote wa Baraza na Kamati ya Uchumi kwa Miongozo, hekima, busara na maoni mnayotupatia katika kuimarisha utendaji wa shughuli zetu za kila siku. Nakuomba wewe na Wajumbe wako kuwa Mabalozi wazuri kwa Wananchi kuwashajiisha na kuhakikisha wananufaikana huduma mbali mbali tunazozitoa ikiwemo fursa za uwezeshaji, uwekezaji, ajira, mikopo na mafunzo ili waweze kuimarisha shughuli zao za kujipatia kipato na kuchangia katika kukuza uchumi wa Nchi. Mwisho napenda kumshukuru Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali.

**100. Mheshimiwa Spika;** Naoamba kutoa Hoja.


……………………………………………..


**MHE. MUDRIK RAMADHAN SORAGA (MBM)**
**WAZIRI WA NCHI, AFISI YA RAIS, KAZI,**
**UCHUMI NA UWEKEZAJI**
**ZANZIBAR.**

## 10.0 VIAMBATANISHO


### Kiambatanisho nambari 1(a na b)

### UKUAJI WA SEKTA YA UWEZESHAJI, UWEKEZAJI NA KAZI





**Kiambatanisho nambari 1(c)**





**Kiambatanisho nambari 1(d)**



**Kiambatanisho nambari 1(e)**




**Kiambatanisho nambari 1(f)**



**Kiambatanisho Nambari 2**

**PROGRAMU KUU NA NDOGO ZA AFISI YA RAIS KAZI UCHUMI NA UWEKEZAJI KWA FUNGU A07 (KAZI NA UWEZESHAJI) NA FUNGU A08 (UCHUMI NA UWEKEZAJI)**

## Jadweli namba 1 - FUNGU A07 (KAZI NA UWEZESHAJI)

| |
|---|
| **PA0702: Programu Kuu ya Usimamizi wa Sheria za Kazi, Ukaguzi Kazi na Kazi za Staha kwa Wote.** |
| SA070201: Programu Ndogo ya Uratibu wa Upatikanaji wa Ajira za Staha. |
| SA070202: Programu Ndogo ya Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini. |
| SA070203: Programu Ndogo ya Usimamizi wa Viwango vya Kazi vya Kimataifa na Majadiliano ya Pamoja Kazini |
| **PA0703: Programu Kuu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.** |
| SA070301: Programu Ndogo ya Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. |
| SA070302: Programu Ndogo ya Usimamizi na Uimarishaji wa Vyama vya Ushirika |
| SA070303: Programu Ndogo ya Uratibu na Uendelezaji wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. |
| **PA0705: Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji.** |
| SA070501: Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Afisi |
| SA070502: Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji |
| SA070503: Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Afisi Pemba |

**Jadweli namba 2: FUNGU A08 (UCHUMI NA UWEKEZAJI)**

| |
|---|
| **PA0801: Programu Kuu ya Kuimarisha Uwekezaji na Mashirikiano Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi** |
| SA080101: Programu Ndogo ya Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi |
| SA080102: Programu Ndogo ya Maendeleo ya Ukuaji wa Uchumi kupitia Uwekezaji |
| **PA0802: Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji.** |
| SA080201: Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji |
| SA080202: Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Afisi |
| SA080203: Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Afisi Pemba |

**Kiambatanisho Nambari 3**

**FUNGU A07 (KAZI NA UWEZESHAJI)**

**MUHTASARI WA MAPATO YALIYOKUSANYWA KWA KIPINDI CHA JULAI 2022 HADI MACHI 2023**

| Kasma | Vyanzo vya mapato | Bajeti ya mwaka | Makadirio ya Miezi Tisa Julai 2022 hadi Machi 2023 | Makusanyo halisi ya Miezi Tisa Julai 2022 hadi Machi 2023 | Asilimia ya Makadirio ya miezi Tisa | Asilimia ya Makadirio ya Mwaka 2022/2023 | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **TZS** | **TZS** | **TZS** | **(%)** | **(%)** | |
| 1422036 | Ada ya Usajili wa Vyama vya Ushirika | 70,000,000 | 52,500,000 | 54,680,000 | **104.2** | **78.1** | Usajili umeongezeka kutokana na kuwepo kwa mikopo ya INUKA chini ya CRDB ambao masharti yake ni lazima Wajasiriamali wawe kwenye kikundi kilichosajiliwa. |
| 1422037 | Ada ya Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika | 50,000,000 | 37,500,000 | 25,763,600 | **68.7** | **51.5** | |
| 1422071 | Ukaguzi wa Usalama na Afya maeneo ya Kazi | 475,000,000 | 361,000,000 | 148,205,000 | **41.1** | **31.2** | Uhaba wa vifaa vya ukaguzi na wataalamu wa kutosha umeshusha makusanyo |
| 1422075 | Ada ya Ukaguzi wa Mikataba ya Ajira Nje ya Nchi | 225,000,000 | 173,500,000 | 90,915,680 | **52.4** | **40.4** | Uhaba wa Bajeti kuweza kuzifikia taasisi zote. |
| 1422011 | Ada ya Vibali vya Kazi kwa Wataalam wa Kigeni | 1,243,200,000 | 959,400,000 | 1,108,987,200 | **115.6** | **89.2** | Vibali vya Kazi vimeongezeka kutokana na kuongezeka kwa miradi ya uwekezaji nchini |
| 1422012 | Ada ya Uhakiki wa Mikataba | 36,800,000 | 28,300,000 | 55,990,000 | **197.8** | **152.1** | Mapato yameongezeka kutokana na kufunguliwa mipaka baada ya kumalizika Korona |
| | **JUMLA** | **2,100,000,000** | **1,612,200,000** | **1,484,541,489** | **92.1** | **70.7** | |

**Kiambatanisho Nambari 4(a)**

**FUNGU A07 (KAZI NA UWEZESHAJI)**

## MUHTASARI WA MATUMIZI YA BAJETI NA MATUMIZI KWA MISHAHARA, RUZUKU, MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA JULAI 2022 – MACHI, 2023

| ENEO | BAJATI YA AWALI MWAKA 2022/2023 | BAJATI BAADA YA UHAULISHO 2022/2023 | MAKADIRIO JULAI 2022 HADI MARCH 2023 | MATUMIZI JULAI 2022 HADI MACHI 2023 | ASILIMIA JULAI 2022 HADI MACHI 2023 | ASILIMIA YA MWAKA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| MISHAHARA | 2,398,900,000 | 2,831,278,308 | 1,994,557,643 | 1,994,557,643 | **100.0** | **70.4** |
| RUZUKU YA MISHAHARA | 800,300,000 | 1,083,058,675 | 688,486,400 | 688,486,400 | **100.0** | **63.6** |
| MATUMIZI MENGINEYO | 3,138,220,000 | 2,818,837,075 | 1,737,246,932 | 893,966,400 | **51.5** | **31.7** |
| RUZUKU YA MATUMIZI (OC) | 932,700,000 | 861,595,320 | 779,202,100 | 214,996,000 | **27.6** | **25.0** |
| MIRADI YA MAENNDELEO SMZ | 27,600,000,000 | 19,500,000,000 | 19,500,000,000 | - | **0.0** | **0.0** |
| **JUMLA KUU** | **34,870,120,000** | **27,094,769,378** | **24,699,493,075** | **3,792,006,443** | **15.4** | **14.0** |

# Kiambatanisho Nambari 4(b)

**FUNGU A07 (KAZI NA UWEZESHAJI)**

**MUHTASARI WA MATUMIZI YA BAJETI NA MATUMIZI KWA KIPINDI CHA JULAI 2022 – MACHI, 2023**

| PROGRAMU | BAGETI YA MWAKA 2022/2023 | MAKADIRIO YA MIEZI TISA (JULAI -MACHI) 2022/2023 | MATUMIZI MENGINEYO (OC) " A" | MATUMIZI YA MISHAHARA "B" | MATUMIZI YA MAENDELEO "C" | JUMLA YA FEDHA ZILIZOINGIZWA JULAI - MACHI 2022/2023 "A+B+C" | ASILIMIA YA FEDHA JULAI - MACHI. 2022/2023 (%) | ASILIMIA YA MWAKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **PROGRAMU KUU YA USIMAMIZI WA SHERIA ZA KAZI** | **1,529,000,000** | **1,740,653,995** | **1,197,688,500** | **169,823,000** | **688,486,400** | **858,309,400** | **71.7** | **49** |
| Programu Ndogo ya Usimamizi wa Viwango vya Kazi vya Kitaifa na Majadiliano ya Pamoja | 1,229,000,000 | 1,467,598,675 | 1,028,758,500 | 85,663,000 | 688,486,400 | 774,149,400 | 75.3 | 53 |
| Programu Ndogo ya Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini | 150,000,000 | 135,915,960 | 88,275,000 | 45,920,000 | - | 45,920,000 | 52,0 | 34 |
| Programu Ndogo ya Uratibu wa Upatikanaji wa Ajira za Staha | 150,000,000 | 137,139,360 | 80,655,000 | 38,40,000 | - | 38,240,000 | 47.4 | 28 |
| **PROGRAMU KUU YA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI** | **29,377,207,000** | **20,766,747,110** | **20,566,000,000** | **268,951,737** | **729,588,453** | **998,540,190** | **4.9** | **05** |
| Programu Ndogo ya Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi | 320,605,000 | 320,605,000 | 27,000,000 | 45,173,000 | 206,979,583 | 252152,853 | 93.4 | 79 |
| Programu Ndogo ya Usimamizi wa Vyama vya Ushirika | 687,2777,000 | 455,849,090 | 410,000,000 | 77,305,751 | 332,581,250 | 409,887,001 | 100.0 | 90 |
| Programu Ndogo ya Uratibu na Uendelezaji wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi | 769,325,000 | 490,293,020 | 386,000,000 | 149,472,989 | 190,027,350 | 336,500,336 | 87.2 | 69 |
| **Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Miradi ya Maendeleo** | **27,600,000,000** | **19,500,000,000** | **19,500,000,000** | - | - | - | 00 | 00 |
| **PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA AFISI YA RAIS, KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI** | **3,963,913,000** | **4,587,368,273** | **2,935,804,575** | **670,187,663** | **1,264,969,190** | **1,935,156,853** | **65.9** | **42** |
| Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti | 658,403,000 | 699,109,980 | 460,846,360 | 71,717,411 | 197,000,045 | 268717456 | 58.5 | 38 |
| Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji | 1,773,313,000 | 2,327,061,93 | 1,268,979,640 | 335,724,152 | 520,249,355 | 855,973,507 | 67.2 | 37 |
| Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za Afisi Pemba | 1,532,197,000 | 1,561,197,000 | 1,205,978,575 | 262,746,100 | 547,719.790 | 810,465,890 | 67.2 | 52 |
| **JUMLA KUU** | **34,870,120,000** | **27,094,769,378** | **24,699,493,075** | **1,108,962,400** | **2,683,044,043** | **3,792,006,443** | **15.4** | **14** |

**Kiambatanisho Nambari 5(a)**

## FUNGU A08 (UCHUMI NA UWEKEZAJI)

## MUHTASARI WA MATUMIZI YA BAJETI NA MATUMIZI KWA MISHAHARA, RUZUKU, MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA JULAI 2022 – MACHI, 2023

| ENEO | BAJATI YA MWAKA 2022/2023 | MAKADIRIO JULAI 2022 HADI MARCH 2023 | MATUMIZI JULAI 2022 HADI MACHI 2023 | ASILIMIA JULAI 2022 HADI MACHI 2023 |
|---|---|---|---|---|
| MISHAHARA | 749,807,475 | 608,698,075 | 558,360,810 | **91.7** |
| RUZUKU YA MISHAHARA | 2,868,543,685 | 2,130,971,843 | 2,196,985,991 | **103.10** |
| MATUMIZI YA KAWAIDA | 1,370,655,067 | 1,258,322,250 | 378,686,700 | **30.09** |
| MIRADI YA MAENNDELEO SMZ | 15,100,000,000 | 11,325,000,000 | 1,492,282,150 | **13.18** |
| **JUMLA KUU** | **20,089,006,227** | **15,322,992,168** | **4,626,315,651** | **30.19** |

## Kiambatanisho Nambari 5(b)

### FUNGU A08 (UCHUMI NA UWEKEZAJI)

### MUHTASARI WA MATUMIZI YA BAJETI NA MATUMIZI KWA KIPINDI CHA JULAI 2022 – MACHI, 2023

| PROGRAMU | BAJATI YA MWAKA 2022/2023 | MAKADIRIO JULAI HADI MARCH 2023 | MATUMIZI MENGINEYO OC | MATUMIZI YA MISHAHARA | MATUMIZI YA FEDHA ZA MAENDELEO | JUMLA OC NA MISHAHARA NA FEDHA ZA MAEDELEO | ASILIMIA JULAI HADI MACHI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Programu Kuu ya Kuimarisha Uwekezaji na Mashirikiano Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi** | **18,519,845,285** | **13,859,111,543** | **78,234,000** | **2,281,310,281** | **1,492,282,150** | **3,851,826,431** | **27.7** |
| Programu Ndogo ya Mashirikiano Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi | 551,301,600 | 403,140,000 | 78,234,000 | 84,324,290 | | 162,558,290 | **40.3** |
| Programu Ndogo ya Kushajiisha Uwekezaji wa ndani na nje ya nchi | 17,968,543,685 | 13,455,971,843 | | 2,196,985,991 | 1,492,282,150 | 3,689,268,141 | **27.4** |
| **Programu Kuu ya Utawala na Uendeshaji** | **1,569,160,942** | **1,463,880,325** | **300,452,200** | **474,036,520** | | **774,489,220** | **52.9** |
| Programu Ndogo ya Usimamizi wa rasilimali na huduma za utawala | 1,023,831,180 | 979.488,575 | 172,884,200 | 474,036,520 | | 646,920,720 | **66.6** |
| Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango Sera na Tafiti | 272,129,000 | 239,999,000 | 48,410,000 | | | 48,410,000 | **20.1`** |
| Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa shughuli Pemba | 273,200,762 | 244,392,750 | 79,158,500 | | | 79,158,500 | **32.3** |
| **JUMLA KUU** | **20,089,006,227** | **15,322,992,168** | **378,686,700** | **2,755,346,801** | **1,492,282,150** | **4,626,315,651** | **30.19** |

**Kiambatanisho Nambari 6**

| FEDHA ZILIZOTOLEWA NA WANUFAIKA KUPITIA FEDHA ZA INUKA MACHI,2022-FEBUARI, 2023 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **WILAYA** | **KIWANGO** | **WANUFAIKA** | | |
| | | **WANAUME** | **WANAWAKE** | **JUMLA** |
| KASKAZINI “A” | 577,065,500.00 | 250 | 547 | 797 |
| KASKAZINI “B” | 510,824,000.00 | 145 | 335 | 480 |
| KATI | 629,673,900.00 | 277 | 588 | 865 |
| KUSINI | 124,600,000.00 | 128 | 275 | 403 |
| MAGHARIB “A” | 1,602,193,000.00 | 507 | 1093 | 1600 |
| MAGHARIB “B” | 3,708,041,000.00 | 843 | 1513 | 2356 |
| MJINI | 3,464,510,880.00 | 1315 | 1498 | 2813 |
| JUMLA UNGUJA | 10,616,908,280.00 | 3,465 | 5,849 | 9,314 |
| MICHEWENI | 1,553,975,579.00 | 777 | 3,223 | 4000 |
| WETE | 1,617,183,946.54 | 707 | 550 | 1257 |
| CHAKECHAKE | 2,099,819,086.74 | 859 | 565 | 1424 |
| MKOANI | 1,784,415,244.00 | 1022 | 1086 | 2108 |
| **JUMLA PEMBA** | **7,055,393,856.28** | **3,365** | **5,424** | **8,789** |
| **JUMLA KUU** | **17,672,302,136.28** | **6,830** | **11,273** | **18,103** |

## Kiambatanisho Nambari 7

**MAREJESHO YA MFUKO WA UWEZESHAJI UNGUJA NA PEMBA JULY, 2022-MARCH,2023**

| WILAYA | JULY | AUGUST | SEPETEMBER | OCTOBER | NOVEMBER | DECEMBER | JANUARY | FEBRUARY | MARCH | TOTAL |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mjini | 1,040,000 | 940,000 | 363,000 | 2,388,000 | 565,000 | 800,000 | 1,290,000 | 410,000 | 460,000 | 8,256,000 |
| Magharibi "A" | 1,200,000 | 1,875,000 | 200,000 | 940,000 | 400,000 | 605,000 | 580,000 | - | 600,000 | 6,400,000 |
| Magharibi "B" | 3,465,000 | 1,130,000 | 970,000 | 550,000 | 910,000 | 400,000 | 1,360,000 | 2,570,000 | 1,300,000 | 12,655,000 |
| Kaskazini "A" | 595,000 | 560,000 | 100,000 | - | - | - | - | 150,000 | - | 1,405,000 |
| Kaskazini "B" | 470,000 | 150,000 | 150,000 | 280,000 | 110,000 | 100,000 | 300,000 | 250,000 | 150,000 | 1,960,000 |
| Kati | 1,545,000 | 2,860,000 | 511,000 | 960,000 | 330,000 | 615,000 | 1,180,000 | 793,000 | 1,397,000 | 10,191,000 |
| Kusini | 840,000 | 50,000 | - | 490,000 | - | - | 290,000 | - | - | 1,670,000 |
| **TOTAL UNGUJA** | **9,155,000** | **7,565,000** | **2,294,000** | **5,608,000** | **2,315,000** | **2,520,000** | **5,000,000** | **4,173,000** | **3,907,000** | **42,537,000** |
| Chake Chake | 2,085,000 | 1,160,000 | 3,465,000 | 1,994,000 | 900,000 | 580,000 | 780,000 | 1,170,000 | 243,000 | 12,377,000 |
| Mkoani | 1,235,000 | 1,887,000 | 1,057,000 | 1,903,000 | 1,558,000 | 705,500 | 420,000 | 785,000 | 1,633,000 | 11,183,500 |
| Wete | 1,719,000 | 834,000 | 1,352,000 | 560,000 | 2,522,000 | 1,177,000 | 1,890,000 | 847,000 | 380,000 | 11,281,000 |
| Micheweni | 340,000 | 1,880,000 | 2,272,000 | 1,928,000 | 980,000 | 1,055,000 | 1,010,000 | 180,000 | 200,000 | 9,845,000 |
| **TOTAL PEMBA** | **5,379,000** | **5,761,000** | **8,146,000** | **6,385,000** | **5,960,000** | **3,517,500** | **4,100,000** | **2,982,000** | **2,456,000** | **44,686,500** |
| **JUMLA KUU** | **14,534,000** | **13,326,000** | **10,440,000** | **11,993,000** | **8,275,000** | **6,037,500** | **9,100,000** | **7,155,000** | **6,363,000** | **87,223,500** |

## Kiambatanisho Nambari 8

**MUHTASARI WA MAKADIRIO YA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024**

| **PEMBA** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **KASMA** | **MAELEZO** | **MAKADIRIO 2023-2024** | **MAKISIO 2024-2025** | **MAKISIO 2025-2026** |
| 1422012 | Uthibitishwaji wa Mikataba ya Kazi | 40,000,000 | 45,000,000 | 49,663,000 |
| 1422036 | Ada ya Uandikishaji wa Vyama vya Ushirika | 60,000,000 | 68,000,000 | 72,000,000 |
| 1422037 | Ada ya Ukaguzi wa Vyama na Huduma | 40,000,000 | 50,000,000 | 62,000,000 |
| 1422071 | Ukaguzi wa Maeneo ya Kazi | 80,000,000 | 90,000,000 | 102,000,000 |
| | **JUMLA PEMBA** | **220,000,000** | **253,000,000** | **285,663,000** |
| **UNGUJA** | | | | |
| **KASMA** | **MAELEZO** | **MAKADIRIO 2023-2024** | **MAKISIO 2024-2025** | **MAKISIO 2025-2026** |
| 1422036 | Ada ya Uandikishaji wa Vyama vya Ushirika | 90,000,000 | 100,000,000 | 115,000,000 |
| 1422037 | Ada ya Ukaguzi wa Vyama na Huduma | 60,000,000 | 70,000,000 | 85,000,000 |
| 1422075 | Ada ya Ukaguzi wa Mikataba ya Ajira za Nje | 130,000,000 | 180,000,000 | 200,000,000 |
| 1422011 | Vibali vya Kazi kwa Wataalamu wa Kigeni | 1,710,161,000 | 1,920,691,000 | 2,110,532,000 |
| 1422012 | Uthibitishwaji wa Mikataba ya Kazi | 100,000,000 | 140,000,000 | 170,000,000 |
| 1422071 | Ukaguzi wa Maeneo ya Kazi | 420,000,000 | 480,000,000 | 520,000,000 |
| | **JUMLA UNGUJA** | **2,510,161,000** | **2,890,691,000** | **3,200,532,000** |
| | **JUMLA KUU** | **2,730,161,000** | **3,143,691,000** | **3,486,195,000** |

# Kiambatanisho Nambari 9

**MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 KWA FUNGU LA A07 (KAZI NA UWEZESHAJI)**

| PROGRAMU | MATUMIZI YA KAWAIDA (OC) | MISHAHARA | RUZUKU | RUZUKU YA MISHAHARA | MAENDELEO SMZ | WASHIRIKA WA MAENDELEO | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Programu Kuu ya Usimamizi wa Sheria za Kazi Ukaguzi Kazi na Kazi za Staha kwa Wote** | **-** | **-** | **652,900,000** | **1,085,500,000** | **-** | **-** | **1,738,400,000** |
| Programu Ndogo ya Uratibu wa Upatikanaji wa Ajira za Staha | - | - | 200,000,000 | - | - | - | **200,000,000** |
| Programu Ndogo ya Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini | - | - | 190,000,000 | - | - | - | **190,000,000** |
| Programu Ndogo ya Usimamizi wa Viwango vya Kazi vya Kitaifa na Majadiliano ya Pamoja | - | - | 262,900,000 | 1,085,500,000 | - | - | **1,348,400,000** |
| **Programu Kuu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi** | **991,000,000** | **1,688,668,000** | **1,046,100,000** | | **4,500,000,000** | **2,540,606,000** | **10,766,374,000** |
| Programu Ndogo ya Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi | - | 928,246,000 | 1,046,100,000 | - | 4,500,000,000 | 2,540,606,000 | **9,014,952,000** |
| Programu Ndogo ya Usimamizi na Uimarishaji wa Vyama vya Ushirika | 391,000,000 | 482,374,000 | - | - | - | - | **873,374,000** |
| Programu Ndogo ya Uratibu na Uendelezaji wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi | 600,000,000 | 278,048,000 | - | - | - | - | **878,048,000** |
| **Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji** | **1,002,700,000** | **1,456,737,000** | **-** | **-** | **-** | **-** | **2,459,437,000** |
| Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango Sera na Tafiti | 235,150,000 | 254,304,000 | - | - | - | - | **489,454,000** |
| Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji | 417,550,000 | 616,333,000 | - | - | - | - | **1,033,883,000** |
| Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba | 350,000,000 | 586,100,000 | - | - | - | - | **936,100,000** |
| **JUMLA KUU** | **1,993,700,000** | **3,145,406,000** | **1,699,000,000** | **1,085,500,000** | **4,500,000,000** | **2,540,606,000** | **14,964,211,000** |

## Kiambatanisho Nambari 10

**MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 KWA FUNGU LA A08 (UCHUMI NA UWEKEZAJI)**

| Programu | MATUMIZI YA KAWAIDA (OC) | MISHAHARA | RUZUKU YA MISHAHARA | MAENDELEO SMZ | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|
| **Programu Kuu ya Kuimarisha Uwekezaji na Mashirikiano Baina ya Sekta Binafsi na Sekta ya Umma** | **355,000,000** | **129,076,000** | **2,887,800,000** | **3,500,000,000** | **6,871,876,000** |
| Programu Ndogo ya Mashirikiano Baina ya Sekta Binafsi na Sekta ya Umma | 355,000,000 | 129,076,000 | | | **484,076,000** |
| Programu Ndogo ya Kushajiisha Uwekezaji wa ndani na nje ya nchi | | | 2,887,800,000 | 3,500,000,000 | **6,387,800,000** |
| **Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji** | **719,300,000** | **641,024,000** | | | **1,360,324,000** |
| Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji | 247,300,000 | 92,595,000 | | | **339,895,000** |
| Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango Sera na Tafiti | 322,000,000 | 513,529,000 | | | **835,529,000** |
| Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba | 150,000,000 | 34,900,000 | | | **184,900,000** |
| **JUMLA KUU** | **1,074,300,000** | **770,100,000** | **2,887,800,000** | **3,500,000,000** | **8,323,200,000** |